23 APRILI, 2026

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

**Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 23 Aprili, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Daniel B. Sillo) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea. Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza maswali na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 171

**Upungufu wa Vifaa vya Maabara Shule za Sekondari**

**MHE. MWANTATU M. KHAMIS** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha Shule za Sekondari zinaondokana na Upungufu wa Vifaa vya Maabara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikitoa fedha za ununuzi wa vifaa vya maabara kwa ajili ya ujifunzaji na ufundishaji wa masomo ya sayansi ili kuwa na wahitimu wenye umahiri unaoendana na zama za sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali imetumia shilingi bilioni 3.51 kununua na kusambaza kemikali na vifaa vya maabara katika shule za sekondari 231. Vilevile, Serikali hivi sasa inaendelea na mchakato wa manunuzi yenye thamani ya shilingi bilioni 13.97 kwa ajili ya vifaa vya maabara vya shule 672.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha za ununuzi wa vifaa vya maabara katika shule za sekondari ili kuboresha mazingira ya kujifunza na ufundishaji wa masomo ya Sayansi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mwantatu, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTATU M. KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ningependa kumwuliza swali lenye kipengele (a) na (b) la nyongeza:-

(a) Kuna mpango gani wa Serikali katika kuhakikisha shule za wasichana zinazojengwa mikoani zinapatiwa vifaa vya maabara vya kutosha pamoja na watu wa maabara?

(b) Kwa kuwa Serikali inaendelea kujenga majengo ya shule za sekondari, je, ni upi mkakati wa Serikali katika kuhakikisha changamoto hii inapatiwa mwarobaini wake?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali kwanza imeweka kipaumbele cha hali ya juu katika ujenzi wa shule za masomo ya sayansi, na katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Serikali imejenga shule za sayansi za mikoa 26 kwa kila mkoa ambazo ziligharimu takribani shilingi bilioni 4.6 kila shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule zile zimejengewa miundombinu yote kwa maana ya maabara za Fizikia, Kemia na Biolojia, na zimepelekewa vifaa vya maabara na wataalamu wa maabara ili kuwezesha masomo ya sayansi yaweze kufanyika kwa ufanisi mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea kutenga fedha. Hivi sasa tuko kwenye taratibu za manunuzi ya vifaa vya maabara vya zaidi ya shilingi bilioni 13.97 ili kuhakikisha shule zetu zote za wasichana, shule za wavulana na shule mchanganyiko zinapata vifaa vya kutosha vya maabara ili wanafunzi wetu waweze kusoma vizuri na kwa ufanisi zaidi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Jimbo la Bunda Mjini linahitaji maabara 48 na maboma ya maabara 13. Ni lini mtatusaidia kukamilisha hili ili na sisi tutoe wataalamu wa sayansi katika jimbo la Bunda Mjini?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka mpango mzuri na madhubuti wa kuhakikisha maeneo yote ya shule zetu za sekondari yenye upungufu wa majengo ya maabara au yenye maabara ambazo hazijakamilishwa, tunakamilisha maabara hizo na tunajenga maabara na kupeleka vifaa na wataalamu ili kuhakikisha watoto wetu wanasoma masomo ya sayansi katika mazingira bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mtaala wa Elimu wa Mwaka 2014, Toleo la 2023, ambapo tumeanzisha utaratibu wa shule za amali pamoja na kuboresha sana eneo la shule za masomo ya sayansi, tumeweka mkakati ambao nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hivi karibuni baada ya taratibu kukamilika tutakuwa na mpango kabambe wa kuboresha miundombinu ya elimu ya sayansi kwa maana ya kujenga maabara hizo na kukamilisha pia elimu ya mafunzo ya amali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali iko makini na tutahakikisha tunatekeleza suala hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Alan Mvano, swali la nyongeza.

**MHE. ALAN T. MVANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Shule tatu za sekondari katika Jimbo la Kakonko hazina kabisa vyumba vya maabara, nazo ni *Kambi Secondary*, *Dr. Mpango Secondary* na *Kakonko Boys Secondary School*. Je, nini mpango wa Serikali kuhakikisha shule hizi tatu nazo zinapata maabara? Ahsante sana

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Alan Mvano, Mbunge wa Kakonko, alishaleta taarifa hiyo Ofisi ya Rais, TAMISEMI, na tayari Idara ya Elimu imeshaandaa mpango kwa ajili ya kuanza ujenzi wa maabara hizo katika shule za sekondari tatu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itafanya shughuli hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia kumsisitiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko kwamba pamoja na fedha za Serikali Kuu, ni muhimu waanze hatua za awali za ujenzi kwa awamu kwa kutumia fedha za mapato ya ndani ili fedha za mapato ya Serikali Kuu zikienda zifanye umaliziaji wa majengo ya maabara hizo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sara Ally Msafiri, swali la nyongeza.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ni ahadi ya Serikali kupitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi kujenga maktaba na maabara ya kisasa kwenye kila wilaya. Je, ni lini Serikali itajenga maabara na maktaba ndani ya Jimbo la Mvomero?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ni Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, na ni dhamira ya Serikali kuendelea kuboresha miundombinu ya maktaba na maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Sara Msafiri, Mbunge wa Jimbo la Mvomero, Serikali inaendelea hivi sasa na ujenzi katika maeneo mbalimbali kote nchini, lakini kwa sababu uhitaji ni mkubwa, Serikali inaendelea kuratibu upatikanaji wa fedha na tutaendelea kujenga miundombinu hiyo kwa awamu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba pia Jimbo la Mvomero litapewa kipaumbele.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fadhili Chilombe, swali la nyongeza.

**MHE. FADHILI S. CHILOMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Katika Jimbo la Tunduru Kusini kuna Sekondari ya Tuwemacho na Masakata, Mtina na Mchoteka, zote hizi tayari zimeshakamilika, zina maabara, lakini hazina vifaa. Nini kauli ya Serikali kupeleka vifaa kwenye shule hizo?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kusini kwamba kama alivyosema Serikali tayari imekamilisha ujenzi wa maabara katika shule hizo tatu na hiyo ilikuwa ni hatua ya kwanza, hatua ya pili ambayo tutakwenda kuhakikisha inatekelezwa ni kupeleka vifaa vya maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, na katika kipindi hiki ninachoongea hapa tayari tuna taratibu za manunuzi ya vifaa vya maabara vya zaidi ya shilingi bilioni 13.97 na mara baada ya kukamilika taratibu hizo tutahakikisha shule hizo pia zinapewa kipaumbele kupelekewa vifaa vya maabara ili watoto wetu waweze kupata mazingira bora zaidi ya kujifunza.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Saidi Salim Hamad, Mbunge wa Ole, sasa aulize swali lake.

Na. 172

**Kukuza na Kuhifadhi Miti ya Mikoko**

**MHE. SAIDI SALIM HAMAD** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kukuza na kuhifadhi Miti ya Mikoko ili kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi kwa niaba ya Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, ninaomba kujibu swali namba 172 la Mheshimiwa Saidi Salim Hamad kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kukuza na kuimarisha uhifadhi wa mifumo-ikolojia ya mikoko nchini ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Hatua hizo ni pamoja na: -

(1) Kuweka misitu ya mikoko katika mojawapo ya maeneo ya vipaumbele vya uzalishaji wa viwango vya Kaboni ili kuwezesha jamii za pwani kunufaika na biashara ya kaboni;

(2) Kuwezesha jamii za pwani kutekeleza miradi na shughuli mbadala za kiuchumi ikiwemo ufugaji nyuki, kilimo cha mwani, uvuvi endelevu, ufugaji/uboreshaji wa kaa ili kupunguza utegemezi wa jamii kwenye misitu ya mikoko;

(3) Kuhamasisha upandaji na urejeshaji wa mikoko ili kuhifadhi mifumo ikolojia ya misitu ya mikoko; na

(4) Kujenga uwezo wa Kamati za Uhifadhi za Mazingira na vikundi vya usimamizi wa maeneo ya fukwe ili kuongeza usimamizi na utekelezaji wa Sheria zinazosimamia rasilimali za pwani na bahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Saidi Salim, swali la nyongeza.

**MHE. SAIDI SALIM HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza madogo kama ifuatavyo: _

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali kupitia Waziri iko tayari kuja Jimbo la Ole kuona jitihada ambazo tunazifanya kwenye suala hili la mikoko?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa Jimbo la Ole tumeanzisha vikundi kwa ajili ya kuvikuza na kuitunza mikoko, je, Serikali iko tayari kuviwezesha vikundi hivyo vya akina mama? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Saidi kwa jitihada zake za kusimamia mazingira, na kama ulivyofahamu, mazingira ni kipaumbele na ni moja kati ya nguzo katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi na *Vision 2025.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana, na ninakuahidi kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, nitaambatana naye baada ya kukubaliana ni lini ambapo yeye atakuwa na nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nimhakikishie, pwani ambayo ina kilomita zaidi ya 1,424 hivi, inaendelezwa kwa kutumia mpango huu wa kupanda mikoko, na tunatumia sana vikundi kwa ajili ya kupanda mikoko. Hili nimhakikishie, tunaendelea na tutaendelea pamoja na vikundi ambavyo ataviainisha katika Jimbo lako la Ole.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu ya swali la Mheshimiwa Mbunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maji. Mheshimiwa Khalid Mussa Nsekela, Mbunge wa Kyerwa, sasa aulize swali lake.

Na. 173

**Uhitaji wa Maji Safi Mashuleni, Stendi, Vituo vya Afya na Masokoni - Kyerwa**

**MHE. KHALID M. NSEKELA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itachukua hatua za haraka za upatikanaji wa maji safi na salama katika Zahanati, Vituo vya Afya, Masoko na Mashuleni – Kyerwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso, majibu.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Khalid Mussa Nsekela, Mbunge wa Jimbo la Kyerwa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali ni kuhakikisha inafikisha huduma ya majisafi na salama kwenye maeneo yote yanayotoa huduma za kijamii ikiwemo shule, vituo vya kutolea huduma za afya, vituo vya mabasi na masoko. Huduma hiyo imeshapatikana kwenye baadhi ya maeneo mbalimbali nchini kupitia miradi ya maji iliyopo, sambamba na ile inayoendelea kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2026, Serikali imefikisha huduma ya majisafi na salama kwenye shule 9,957 na vituo 4,348 vya kutolea huduma za afya kote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Wilaya ya Kyerwa, Serikali imefikisha huduma ya majisafi na salama kwenye Shule za Msingi na Sekondari 55 na Vituo 18 vya kutolea huduma za Afya pamoja na Hospitali ya Wilaya. Serikali itaendelea kutoa kipaumbele cha kipekee kwenye maeneo yote yanayotoa

huduma za kijamii ili kuhakikisha yanafikiwa na huduma ya majisafi na salama kadiri miradi ya maji inavyotekelezwa kwenye maeneo yote nchini ikiwemo Wilaya ya Kyerwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khalid Mussa Nsekela, swali la nyongeza.

**MHE. KHALID M. NSEKELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, je, kwa kuwa Wilaya ya Kyerwa imekuwa na changamoto ya muda mrefu ya huduma ya maji, Serikali haioni haja ya kuifanya Wilaya ya Kyerwa kuwa kanda maalum ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuambatana na mimi na kufika Kyerwa kujionea changamoto ya maji iliyokuwa? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge. Kwa kweli moja ya ajenda yake katika Bunge hili ni kuhusu suala zima la Wanakyerwa kuweza kupata huduma ya majisafi na salama. Sisi kama Wizara ya Maji ni wilaya ambayo tumeiangalia kwa kina sana. Ni moja ya wilaya tulizoifanyia tathmini, hasa katika kipindi hiki kwamba ni wilaya ambayo ina vijiji takribani 99, tumeshafikisha zaidi ya vijiji 55. Ipo miradi ya kimkakati ambayo tunaitekeleza katika kuhakikisha wananchi wa Kyerwa wanapata huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao mradi wa Runyinya-Chanya zaidi ya shilingi bilioni 3.7, Kimuli-Nyanga zaidi ya shilingi bilioni mbili, Kaisho-Isingiro zaidi ya shilingi bilioni 1.9. Ninataka niwahakikishie, tutaisimamia Wanakyerwa waweze kupata huduma ya majisafi na salama, na mimi baada ya Bunge nipo tayari kuongozana na wewe kufika katika jimbo lako la Kyerwa. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninawaona wengi, kwa hiyo, maswali mafupi. Mheshimiwa Deo Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Halmashauri ya Mji Njombe tuna mradi wa Igombwi umekaa zaidi ya miaka sita bila kukamilika, uko 85%. Ninaomba uhakika ni lini mradi huu utakamilika? Je, umetengwa kwenye bajeti ya sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa swali hili. Huo ni mradi wa kimkakati, na ni moja ya agenda katika jimbo lake. Tumepokea zaidi ya shilingi bilioni 30 kwa ajili ya malipo ya wakandarasi. Tutatoa fedha kuhakikisha mradi unakamilika na wananchi hawa waweze kupata huduma ya majisafi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bashungwa, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Wanavijiji wa vijiji vya Nyakakika, Kanogo, Omukakajinja, Janyanatika na Kanyamaganda, kwanza wanampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya, lakini wanamlilia na kuomba mtambo wa kuchimba visima katika hivi vijiji. Je, anawaambiaje wananchi hawa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ninampongeza Mheshimiwa Mbunge. Nimwambie tu, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameapa kumtua mwanamke ndoo kichwani. Katika jitihada zake za dhati amenunua mitambo kwa ajili ya uchimbaji visima katika kila mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, mitambo yetu ipo karibu, lakini hayo maeneo ambayo ameyaeleza tutayapangia nguvu na kuhakikisha kwamba mtambo unafika na wanachimbiwa visima na watu waweze kupata huduma ya majisafi na salama.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu la Same Mashariki lina kata kubwa mbili. Kata ya Maore ina takribani watu 20,000 na Kata ya Ndungu ina takribani watu 19,000. Kata hizi miradi yake yote ni ya mwaka 1967 na kwa sasa hivi wana shida kubwa sana. Mheshimiwa Waziri alifika jimboni kwangu, ananiambia nini sasa kuhusu kata hizi mbili asubuhi hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira ya Serikali ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie Mheshimiwa Mbunge, kwa kuwa tunakwenda kwenye bajeti, na bajeti yetu ni tarehe tano na tarehe sita, niombe saa saba tukutane, tuone namna tunavyojipanga ili kuweza kuwasaidia wananchi wake, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Moses Kaegele, swali la nyongeza.

**MHE. MOSES L. KAEGELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Wazir, Kata ya Myula yenye vijiji vitano, ndani ya vijiji vinne vyote hamna maji safi na salama lakini Shule ya Sekondari ya Myula nayo haina maji safi na salama. Ni upi mpango wa Serikali wa dharura wa kupeleka maji safi na salama katika Shule ya Sekondari ya Myula?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka niwahakikishie Wabunge na nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa ajenda yake hii ya maji. Ninataka nimhakikishie tumejipanga vizuri kwenye bajeti yetu maeneo ambayo nchi nzima ambapo hatujafikisha maji ni vijiji 1,575. Kwa hiyo, mkakati wetu wa Wizara ya Maji ni kuhakikisha bajeti hii katika kipindi cha miaka mitano vijiji vyote ambavyo vimebaki vinakwenda kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Sekondari ya Kata ya Nanyala imekuwa haina maji kwa muda mrefu na ni sekondari ya kidato cha kwanza mpaka cha sita. Ni lini mkandarasi aliyepewa kupeleka maji katika shule hiyo atarudi kazini ili aweze kupeleka maji kwenye shule hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mkandarasi yupo na anatekeleza mradi ninadhani kuna haja ya kumwongezea nguvu na kumpatia fedha. Nipo tayari kuwapatia fedha kuhakikisha mradi unakamilika na shule hii iweze kupata huduma ya maji safi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Bakari Bakari Shingo Mbunge wa Ukonga sasa aulize swali lake.

Na. 174

**Marekebisho ya Dharura Barabara ya Mombasa – Gongo la Mboto – Makaburi ya Kiltex**

**MHE. BAKARI B. SHINGO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani kukarabati kwa dharura barabara ya Nyerere katika maeneo ya Mombasa – Gongo la Mboto na maeneo ya makaburi ya Kiltex?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa *Engineer* Kasekenya majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Bakari Shingo, Mbunge wa Ukonga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha ujenzi wa barabara kwa sehemu ya Mombasa hadi Gongo la Mboto kupitia mradi wa mabasi yaendeayo haraka awamu ya tatu *(DRT 3)*. Aidha, kwa barabara ya inayopita maeneo ya makaburi ya Kiltex, tayari kuna mkandarasi anaendelea kuifanyia matengenezo kwa kuchonga tuta na kuweka tabaka la changarawe ili kuwezesha barabara kupitika majira yote ya mwaka. Kazi za matengenezo zinatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2026.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bakari Bakari, swali la nyongeza.

**MHE. BAKARI B. SHINGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Swali langu msingi wake ulitokana na ujenzi huo wa barabara ambapo ujenzi huo umepelekea kuwa na mafuriko na Mheshimiwa Waziri analijua hili jambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya Mombasa kulikuwa na kalavati la asili pale lenye ukubwa wa sentimita 60, sasa hivi ujenzi huu wameenda kuweka kalavati lenye ukubwa kama sentimita 90 ama 120 ambayo imepelekea mafuriko, ndiyo ambayo swali langu la msingi lilivyokuwa linaelekea hivyo. Kumekuwa na mafuriko sasa Wizara iniambie inafanyaje kudhibiti yale mafuriko yasiende kuingia kwenye makazi ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa na tukio hilo pia lipo katika msikiti wa mashine ya maji kwamba pale tulikuwa na kalavati kubwa lenye ukubwa wa zaidi ya sentimita 120 sasa hivi ile njia imefungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa hiyo kitendo cha kufunga na barabara imepanda juu kumesababisha pia mafuriko yanaingia kwenye misikiti na majengo ya wakazi eneo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, hapo mwisho wa stendi ya mwendokasi palikuwa na kalavati, kalavati lile limeondelewa pakajengwa stendi kwa hiyo maji yamekuwa mafuriko na yanaelekea kwenye makaburi ya Kiltex ambavyo hivi ninavyozungumza inawezekana hata mabaki ya wanadamu yakawa yako juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ndiyo hoja yangu ipo hapo kwamba mpango gani wa dharura sasa wa hiyo shida ambayo imesababishwa na ujenzi wetu itakwenda kwisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tuna suala la stendi ya pale ubena, mmejenga barabara imepanda juu vizuri na stendi lakini hatukuweka *service road*, (sehemu ya kupita waenda kwa miguu) kwa hiyo imekuwa kama kisiwa, ndiyo msingi wa swali langu kwako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa naibu spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kwa pamoja ya Mheshimiwa Bakari Bakari Shingo, Mbunge wa Ukonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hili analolisema tunakubali lipo, na bahati nzuri mimi hilo eneo kwa kweli nalifahamu vizuri. Nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba *TANROADS* makao makuu, *TANROADS* mkoa waliokuwa wanasimamia ujenzi wa hiyo barabara ya *DRT* na wenzetu wa *TARURA* ambao sisi tuna ushoroba wetu ambao ni mdogo huko tunapokwenda kwenye makazi sisi hatutakiwi kwenda, lakini tunashirikiana na wenzetu wa *TARURA* kutengeneza hiyo mifereji na hasa baada ya kukamilisha huo mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nataka nitumie nafasi hii kumwelekeza Meneja wa Mkoa wa Dar es Salaam, *TANROADS* Makao Makuu waweze kumshirikisha Mheshimiwa Mbunge mipango ambayo ipo na wanachokifanya ili aweze kusaidia na kuwaelimisha na kuwaeleza wananchi Serikali inafanya nini ili kuondoa hiyo adha baada ya kukamilisha ujenzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge watakushirikisha, watakupa mipango ya kufanya ili kuhakikisha kwamba baada ya ujenzi huu hatufanyi adha kwa wananchi ambao walikuwa na maisha ambayo hawakuwa na hayo mafuriko.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza. Mheshimiwa Shangazi subiri, Mheshimiwa Zodo, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Barabara ya Handeni-Kang'ata-Negero-Mziha mpaka Turiani ni mbovu sana. Je, ni lini Serikali inakwenda kujenga barabara hii inayohudumia majimbo manne; Jimbo la Handeni Mjini, Handeni, Kilindi pamoja na Mvomero?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge tumeshaanza kuijenga kwa awamu na sasa hivi tumeshajenga mpaka pale Turiani na tunategemea katika bajeti hii tutaendelea kujenga kilometa 30, na malengo ni kukamilisha barabara hiyo kadiri fedha itakavyopatikana lakini tuna uhakika tumepanga kuendelea kilometa 30.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mashimba Ndaki, swali la nyongeza.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Barabara ya Njia Panda - Ikungu kwenda Malampaka kilometa 15, mkandarasi wake ametelekeza kazi na inasemekana ni kwa sababu ya malipo. Je, ni lini mkandarasi huyo atalipwa ili arudi kazini kuendelea na kazi yake? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, iko miradi kadhaa ambayo tulikuwa tunatekeleza na wakandarasi wameshaleta *certificate* (hati za madai ya malipo) ambapo tuko tunaendelea kutafuta fedha na kuwalipa ikiwa ni pamoja na huyu mkandarasi ambaye Mheshimiwa Mashimba Ndaki amemsema. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa hivi kazi zote ni kuhakikisha kwamba kazi zote zilizokuwa zimesimama tunawalipa wakandarasi na wanarudi *site* ili kuendelea na kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Lukozi kwenda Malindi mpaka Mlalo, takribani wiki moja sasa haipitiki baada ya mkandarasi kuweka kifusi ambacho hakina ubora. Je, ni mkakati gani wa dharura ambao utafanyika ili wananchi hawa wa Lukozi, Malindi mpaka Mlalo waweze kuwasiliana kwa haraka? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, barabara aliyoitaja ni kati ya barabara ambazo kwenye ziara ya Mheshimiwa Waziri mkuu tulipita na akatolea maelekezo moja ilikuwa ni kwanza kuifanyia usanifu, na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tayari hiyo kazi imeshaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matengenezo ya dharura, hiyo barabara ni barabara ambayo kuna mvua nyingi sana. Tuna wakandarasi ama tuna mkandarasi ambaye yupo *standby*. Nitumie nafasi hii kumwelekeza Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Tanga, mkandarasi huyo aende *site* akarekebishe yale maeneo ambayo hayapitiki. Lakini baada ya hapo tutasubiri mvua mpaka itakapokuwa imepungua ndio tutaitengeneza barabara yote, lakini kwa sasa ahakikishe anakwenda kurekebisha maeneo yote ambayo hayapitiki ili wananchi waweze kuwa na mawasiliano.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Mpwapwa, sasa aulize swali lake.

Na. 175

**Ujenzi wa Barabara ya Kongwa – Mpwapwa**

**MHE. GEORGE N. MALIMA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara kutoka Njiapanda ya Kongwa hadi Mpwapwa Mjini kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kongwa – Mpwapwa yenye urefu wa kilometa 38.45 unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Hadi sasa jumla ya kilometa 6.45 zimejengwa kwa kiwango cha lami kuanzia Mpwapwa Mjini hadi Mwanakianga. Aidha, mkataba wa ujenzi kwa sehemu iliyobaki ya kuanzia Mwanakianga – Kongwa (urefu wa kilometa 32) umesainiwa ambapo taratibu za malipo ya awali kwa Mkandarasi kwa ajili ya kuanza ujenzi zinaendelea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malima, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya serikali, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mkandarasi huyu amekuwepo *site* kwa zaidi ya miaka miwili sasa na kumezuka uvumi kwamba huyu siyo yule anayetarajiwa kujenga hii barabara isipokuwa yeye ni mfanyabiashara wa kokoto tu. Hii inatokana na ukweli kwamba wananchi wamekuwa wakiona malori yakibeba kokoto inayotengenezwa katika site hiyo na kupelekwa maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ili kuondoa sintofahamu hii, Serikali inawaambia nini wananchi wa Mpwapwa kuhusu uvumi huu ambao umezagaa katika Jimbo la Mpwapwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Mpwapwa lakini pamoja na wananchi wa jimbo lake kwamba mkandarasi huyu ambaye ni *SG* ni kati ya wakandarasi naweza nikasema kati ya wakandarasi bora wazawa katika nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunapoongea sasa hivi huyu mkandarasi ndiye anayejenga barabara ya kule Kigamboni - Kibada kwenda Mwasonga kilometa 41. Lakini mkandarasi huyu ndiye aliyejenga njia nne za Kimara kwenda Kibaha. Mkandarasi huyu pia ndiye amejenga ile pale tulipokuwa tunakwama sana eneo la Mtanana, nadhani wote tunapita Mtanana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niwahakikishie waheshimiwa wananchi wa Mpwapwa na Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi tunaamini kati ya wakandarasi bora ni huyu na nadhani nimetaja barabara chache ambazo amezijenga nadhani zinaweza zikapimwa na ubora wake. Kwa hiyo, niwahakikishie wana Mpwapwa na Mheshimiwa Mbunge kwamba kinachosubiriwa alipwe *advance* na hakika mtaelewa kwamba huyu ni mkandarasi ambaye ni bora kabisa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anton Mwantona, swali la nyongeza.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkuu alifanya ziara katika jimbo langu la Rungwe akaahidi kwamba barabara kutoka KK kuelekea Kafwafwa kule Ileje na barabara kutoka Kiwira kuelekea Isangati maandalizi yaanze kufanyika kwa kuijenga kiwango cha lami. Je, ni lini barabara hizi zitaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. KK kwenda Kafwafwa inakamilishwa usanifu na kutoka Kiwira kwenda Isangati barabara hiyo ipo kwenye mpango sasa wa kuanza kusanifiwa kwa sababu ilikuwa bado haijasanifiwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu, swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa Serikali ina mpango wa kuanza ujenzi wa barabara ya Makofia-Mlandizi; je, lini sasa wananchi wa kata ya Yombo watalipwa fidia zao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Barabara ya Makofia-Mlandizi ilikuwa imeshafanyiwa uthamini siku za nyuma lakini muda wake ulikuwa umeshapita, na tumeshafanya uthamini upya kwa ajili ya kufanya maandalizi ya kuwalipa na tunapoongea sasa hivi majedwali ya fidia ya wananchi hao yako hazina kwa ajili ya kupata fedha ili waweze kulipwa hiyo fidia na barabara ijengwe ya kuunganisha Bagamoyo na Mlandizi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ilitujengea barabara kutoka Tosamaganga kwenda kijiji cha Ugwachanya, bahati mbaya kuna mita kama 900 zimebaki sasa ni miaka mitatu. Je, Serikali itatumalizia lini hicho kipande cha mita 900 kati ya Tosamaganga na kijiji cha Ugwachanya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba aweze kurudia ninaomba Mheshimiwa Mbunge niweze kuelewa vizuri kipande hicho cha barabara alichokitaja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiswaga, taja barabara hiyo hajasikia vizuri Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi mara ya pili. Nasema hivi, Serikali ilitujengea barabara kutoka kijiji cha Tosamaganga kwenda kijiji cha Ugwachanya lakini barabara hiyo haijakamilika kwa kipande cha mita kama 900 huu ni mwaka wa tatu. Je, ni lini sasa Serikali itamalizia kipande hicho kilichobaki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue suala hili la Mheshimiwa Mbunge na niweze kujiridhisha baada ya kuwasiliana na wenzetu wa Mkoa wa Iringa changamoto ya hicho kipande kilichobaki ni nini halafu nitampa majibu sahihi Mheshimiwa Mbunge na nini mpango wa Serikali katika hicho kipande ambacho kimebaki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kafiti William Kafiti, Mbunge wa Ilemela, sasa aulize swali lake.

Na. 176

**Ujenzi wa Barabara ya *Airport* - Kayenze Ilemela**

**MHE. KAFITI W. KAFITI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa barabara ya Airport – Kayenze kilometa 34?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Kafiti William Kafiti Mbunge wa Ilemela kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara ya Airport – Kayenze – Nyanguge yenye urefu wa kilometa 46 unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Awamu ya kwanza inahusisha ujenzi kwa kiwango cha lami kuanzia maeneo ya *Airport* hadi Kibangaja (kilometa 10) ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia sita. Kwa sehemu iliyobaki, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kafiti William Kafiti, swali la nyongeza.

**MHE. KAFITI W. KAFITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Ilemela, Mkoa wa Mwanza ni moja ya mikoa ya

kimkakati na ni mkoa wa pili unaochangia mapato katika pato la Serikali. Mkoa wa Mwanza moja ya wilaya za kimkakati ni wilaya ya Ilemela. Wilaya hii ndio wilaya ya pili inayochangia mapato katika mkoa wa Mwanza. Barabara tuliyouliza hapa iko kwenye ilani zaidi ya nne, mpaka leo bado haijatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ndiyo barabara ya kimtakakti katika Jimbo la Ilemela. Tunasema tumechoka na haya majibu, kila siku ni maneno maneno, tunataka majibu ya kweli. Barabara hii mkandarasi atalipwa lini *advance payment* ili aweze kutekeleza mradi huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Ni miaka miwili toka mkandarasi huyu amesaini mkataba na ana *reminder* zaidi ya 12 kulipwa hii *advance payment* yake *shillings* 2.7 *billion,* mpaka leo hakuna majibu yoyote ya Serikali. Leo tunaomba majibu hapa tujue mkandarasi huyu atalipwa lini? Hii ndiyo barabara ya kiuchumi tunayoitegemea Ilemela. Tunaomba majibu ya Serikali. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mbunge. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikiliza Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii imekuwepo kwenye ilani zaidi ya nne, na maana yake ni kwamba katika hii awamu ya sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ndiyo sasa tumeanza kuitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa hatuongelei namna ya kuijenga, ni kwamba tayari tumeshapata mkandarasi, na mkandarasi ameshaanza kazi, tumeshafikia asilimia sita. Anachohitaji mkandarasi ni kulipwa hiyo fedha anayodai.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tulikuwa na miradi mingi ambayo tumekamilisha na awamu tunazoendelea sasa ni kuhakikisha kwamba miradi yote iliyokwama inakwenda kukwamuliwa na Mwanza ikiwepo na hiyo barabara ya kwake ya *Airport,* Igombe, Kayenze hadi Nyanguge na sisi tunajua ndiyo *bypass* kubwa ya watu wanaotoka *Airport* kwenda Musoma, kwenda Magu, watapita hiyo barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali inaitambua na ni barabara ambayo inapita kwenye ukanda wa Ziwa Nyanza kwa maana ya Ziwa Victoria. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Ilemela, Serikali inaitambua sana hii barabara ni muhimu na tutakwenda kuijenga hiyo barabara, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Katani Katani, swali la nyongeza.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Barabara ya Mnivata – Nanyamba - Tandahimba mpaka Masasi unaoendelea, ipo miradi midogo midogo ya ziada ikiwemo na ujenzi wa ghala la kuhifadhia korosho pale Lidumbe. Je, ni lini miradi hii midogo ya ziada itaanza kujengwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tuna miradi ya *complimentary* kwenye Mradi wa Mnivata, Newala hadi Masasi kilomita 160. Tuna masoko, tuna maghala, tuna hata nyumba za waganga lakini pia na miradi ya stendi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunavyoongea sasa hivi tayari tumeshaanza kutangaza hizo kazi ili hao watu waanze kufanya kazi. Kwa urahisi zaidi, Mheshimiwa Mbunge akiwasiliana na Meneja wa Mkoa wa Mtwara, atamhakikishia kwamba tuko kwenye hatua za manunuzi na hizo kazi zote zilizokuwa zinatakiwa zifanyike kama miradi ya ziada, ama kama *CSR* imeshaanza kutangazwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Agnesta Kaiza, swali la nyongeza.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Jana asubuhi na leo asubuhi nimekutumia picha na *video* za wananchi wanaotumia barabara ya kutoka Kifuru kwenda Pugu Stesheni, yaani mnada mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri, alijionea kwa macho jinsi ambavyo maisha ya wananchi yamesimama.

Hivi sasa tunavyoongea, na mpaka jana saa 8.00 za usiku, wananchi hawawezi kuvuka kutoka upande wa A kwenda upande B, na wa upande B kwenda upande A. Maisha yamesimama, na barabara hii tangu kipindi cha Hayati Dtk. Magufuli, Serikali iliahidi kuijenga kwa kiwango cha lami, na ipo ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri atueleze ni lini barabara hii inakwenda kujengwa? Je, nini mpango mkakati sasa wa kuwasaidia wananchi ambao mpaka hivi sasa wanashindwa kuendelea na maisha yao, hawavuki kabisa? Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mheshimiwa Mbunge aliwasilisha hilo, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na pia nilimwambia kwamba, timu ya *TANROADS* Mkoa wa Dar es Salaam, itatembelea hiyo barabara ya Kifuru kwenda Pugu kwa ajili ya kukwamua yale maeneo yanayowezekana. Hata hivyo, barabara hizi za vumbi inapokuwa ni suala la mvua, wakati fulani kuna kazi ambazo haziwezi kufanyika kama maji yapo, mpaka maji yaondoke.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuijenga kwa kiwango cha lami, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Kifuru – Pugu, Kajiungeni – Chanika ni moja ya barabara kama unavyosema ni ya kimkakati, lakini iko kwenye mpango wa kujenga kama *ring road* ama (barabara ya mzunguko) kwa mkoa wa Dar es Salaam. Kwa hiyo, bado usanifu unaendelea ili iendane na barabara ambayo itajengwa kama *outer ring road* ya Mkoa ama Jiji la Dar es Salaam. Kwa hiyo, sehemu inayopita ni pamoja na hiyo Kifuru, Pugu - Mnadani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Eng. Johnston swali la nyongeza.

**MHE. ENG. JOHNSTON J. MUTASINGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anatujengea barabara

katika Jimbo letu Bukoba Mjini ya njia nne, maeneo ya Nyangori, na huu mradi ulianza mwaka 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninapenda kujua, Serikali itamlipa lini mkandarasi anayejenga barabara hiyo ya *Abemulo Contractors* ili aweze kumalizia ujenzi wa barabara hiyo kwa wakati? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, labda tu niwajulishe Waheshimiwa Wabunge kwamba, tunatambua kuna miradi mingi ambayo tulikuwa tumeianza na ikawa inasuasua ama kwa sababu ya kutokulipa malipo ya awali, ama wakandarasi hawajalipwa zile hati zao za malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesema na tutaendelea kusema kwamba, baada ya kukamilisha shughuli zote, na ni maelekezo kwamba ni lazima sasa barabara zote hizo zianze kulipwa na tumeshaanza, barabara nyingi kukwamua, ili zianze kukamilishwa ikiwa ni pamoja na iyo barabara muhimu ya Bukoba Mjini ya Njia Nne.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nianze kushukuru, Waziri wa Ujenzi alifika Tarime juzi akajionea dhahiri jinsi uharibifu wa barabara ya *Keep Left* mpaka Mogabili ilivyokaa, faida yake katika uchumi, kijamii na akaahidi kwamba wanaenda kupeleka fedha kwa uharaka. Wananchi wa Tarime wanatamani kujua kama Serikali itapeleka fedha ndani ya mwaka huu wa fedha ili ile barabara ianze kutengenezwa mara moja?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama Waziri wangu alienda na akaahidi, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali itapeleka ndani ya mwaka huu. Huu ni mwezi wa Nne, *by June* nitahakikisha kwamba tutakuwa

tumepeleka fedha ili mkandarasi aweze kuendelea kufanya iyo kazi ambayo tayari ameshaianza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Janeth Peter Pinda, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 177

**Ujenzi wa Barabara ya Lami Kibaoni – Majimoto Inyonga**

**MHE. JANETH P. PINDA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya kiwango cha lami kutoka Kibaoni kupitia Majimoto hadi Inyonga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Peter Pinda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kibaoni – Majimoto hadi Inyonga yenye urefu wa kilometa 152 ni barabara ya mkoa na inahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)*. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami umekamilika. Kwa sasa, Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Janeth, swali la nyongeza.

**MHE. JANETH P. PINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake aliyonipatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Katavi, wananchi wake ni wakulima wazuri sana wa mazao ya chakula. Kwa kuwa

barabara hii ni kiungo kikubwa sana ambacho kinaweza kikasaidia usafirishaji wa mazao hayo, lakini mpaka sasa hivi ujenzi huo bado haujaanza, je, Serikali haioni kucheleweshwa kwa ujenzi wa barabara hii, kunawacheleweshea maendeleo hasa ya kiuchumi hawa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu walipiga makofi nikashindwa kupata maneno yake vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba tusipige makofi wakati wanauliza maswali ili Mheshimiwa Waziri aweze kusikia vizuri. Mheshimiwa Janeth, naomba urudie maswali ya nyongeza.

**MHE. JANETH P. PINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Swali langu, nauliza, je, ucheleweshwaji wa ujenzi wa barabara hiyo ya kutoka Kibaoni - Inyonga kupitia Majimoto, Serikali haioni kwamba inawacheleweshea wananchi wa Mkoa wa Katavi kiuchumi na kimaendeleo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakati, tunakuwa hatujajenga barabara kwa kiwango cha lami, tunachofanya ni kuhakikisha hizo barabara zinapitika muda wote. Hatua ya kwanza tuliyoifanya ni kuisanifu hiyo barabara ili tuweze sasa kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge atakuwa shahidi, tukiwa kwenye ziara na Waziri Mkuu, alitoa maelekezo kwamba hiyo barabara sasa katika kipindi kinachokuja tuweze kuitandaza hata kama ni kwa awamu, ili tuweze kuanza kuijenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatambua kwamba ndiyo barabara ambayo inayopita mikoa yote ya kaskazini kwa maana ya Tabora, Geita, Mwanza wanapokwenda kusini. Tunafahamu yalikuwa pia ni maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba

tuitangaze kwa ajili ya kuanza ujenzi. Kwa hiyo, tutahakikisha kabla hatujaanza, hiyo barabara inapitika muda wote kwa sababu ni barabara ya muhimu sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, ninawaona, ninaomba maswali mafupi ili angalau wachache mpate nafasi. Mheshimiwa Eng. Ramadhani, swali la nyongeza.

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Bumbuli barabara ya Soni – Bumbuli kilomita 22 kiwango cha lami, ni miongoni mwa hali ya muda mrefu. Ni lini Serikali itatimiza ndoto hii ya Wanabumbuli ya kuwapa matumaini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Soni – Bumbuli kilomita 22 ipo kwenye hatua za manunuzi ili iweze kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Makete tuna maeneo mawili ambapo barabara hazijajengwa; Kipande cha Matamba Mjini lakini pia barabara ya Makete – Mbeya. Ni kweli wakandarasi wamewalipwa, lakini walisema tatizo ni mvua. Sasa kama Mbunge wa Jimbo, mvua ndiyo inakata sasa hivi. Ipi kauli ya Serikali kwa mkandarasi huyu kuanza kazi mara moja kabla ya msimu mwingine wa mvua haujaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ninaomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwamba anatambua eneo lake ni eneo ambalo kwa sasa kazi kubwa haziwezi kufanyika hasa kwa mwezi huu wa Aprili, na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, iko mikoa na hasa ya Nyanda za Juu Kusini, tuna miezi kama minne ambayo mkandarasi asipofanya kazi, kipindi chote hawezi kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kupitia Bunge hili na niwaelekeze hata Mameneja kwamba, pale tu ambapo msimu wa mvua unaisha, wahakikishe kwamba wakandarasi sasa hivi wanafanya maandalizi, mvua inapokatika basi waanze kufanya hizo kazi ambazo zilitakiwa zifanyike kipindi ambacho hakuna mvua na hasa hiyo barabara ya Mheshimiwa Mbunge ya Makete kwenda Isyonje – Mbeya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fadhili Ngajilo swali la nyongeza.

**MHE. FADHILI F. NGAJILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi niulize swali la nyongeza. Iringa tuna barabara ya kutoka Pawaga kuja Iringa Mjini. Barabara hii ina umuhimu sana hasa kwa sababu Serikali imeshaweka zaidi ya shilingi 56,000,000,000 pale Pawaga kwa ajili ya kujenga ile miradi ya umwagiliaji kwa ajili ya kuzalisha mchele mzuri sana kutoka Pawaga.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, tangu mwaka 2020 mmetoa kibali cha kujenga barabara kilomita 20 tu. Sasa swali langu, kilomita 51 zilizobakia ambazo zinapita Jimbo langu la Iringa Mjini, pale Mkwawa, zitaanza kujengwa lini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema kwamba hiyo barabara bado kilomita 51, na sisi tulisema kwamba tutaanza kujenga kwa kiwango cha lami. Hizo barabara kukamilika kwake kutategemea na upatikanaji tu wa fedha, kwamba tutakapopata fedha, tutaendeleza ili tuweze kukamilisha kipande chote, lakini kwanza tukamilishe hizo kilomita 20 halafu tunafuata hizo kilomita nyingine. Kama tutapata fedha, basi tunaweza tukaanza na kuikamilisha hiyo barabara yote kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Devotha, swali la nyongeza.

**MHE. DEVOTHA D. MBURARUGABA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Ninapenda kujua, nini mkakati wa

Serikali kuhusiana na barabara ya Umurushaka kwenda mpaka Benako?

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ni muhimu kwa wananchi wa Karagwe na Ngara. Ninaona mkandarasi anasuasua, nini mkakati wa Serikali, tatizo ni mkandarasi au kuna tatizo lingine? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nimemwelewa Mbunge, nadhani ni barabara ambayo inaanzia Bugene – Buligichato kwenda Benako kama sikosei ndiyo anayoiongelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ina mkandarasi. Mkandarasi huyu ameshaleta maombi ya malipo yake na tukishamlipa. Nina hakika ataendeea na kazi hiyo kwa kasi. Kwa hiyo, tunachofanya sasa hivi ni kuandaa malipo yake, aweze kulipwa na kuendelea na hiyo kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Kwa kuwa barabara ya Babati – Kirumburu ni barabara ya *TANROADS,* na kwa kuwa barabara hiyo kila inapofika kipindi cha masika inajifunga. Je, ni lini Serikali itaanza usanifu wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo barabara nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutafikiria namna ya kufanya. Kwanza, kuifanya iwe inapitika kipindi chote na kuifanyia usanifu kwa ajili ya kuiandaa kwa kuijenga kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na

Wizara ya Afya, Mheshimiwa Adonis Alfred Bitegeko, Mbunge wa Muleba Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 178

**Changamoto za Maduka ya Dawa za Binadamu za Rejareja**

**MHE. ADONIS A. BITEGEKO** aliuliza:-

Je, lini changamoto ya uwepo wa Maduka ya Dawa yasiyo na vibali, wataalamu wenye sifa, utoaji dawa kiholela na uuzaji wa bidhaa zisizoruhusiwa itatatuliwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Samizi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Adonis Alfred Bitegeko, Mbunge wa Muleba Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia mamlaka za udhibiti, yaani Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba, pamoja na Baraza la Famasi inaendelea kusimamia na kufuatilia mwenendo wa utoaji wa huduma za dawa katika maeneo mbalimbali kwa kushirikiana na Mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ambapo huchukua hatua kwa watoa huduma wasiofuata taratibu za uendeshaji wa maduka ya dawa na bidhaa nyingine za afya, ikiwa ni pamoja na kusitisha huduma mara moja na kuwaelekeza wahusika kufuata taratibu zilizowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni pamoja na wale wanaotoa huduma bila vibali vya usajili, kutoa dawa zisizoruhusiwa na kutokuwa na watoa huduma wenye taaluma ya famasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe rai kwa Waganga Wakuu wa Mikoa na halmashauri kupitia timu zao za usimamizi wa afya za mikoa na halmashauri, kuendelea kusimamia huduma za dawa

katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na maduka ya dawa na kuchukua hatua kwa wale wanaoendesha huduma hizo kiholela bila kufuata taratibu zilizowekwa kisheria.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Adonis Maswali ya nyongeza.

**MHE. ADONIS A. BITEGEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Itakuja kuwa tatizo; je, Serikali katika mwaka huu wa fedha imekagua maduka mangapi ya rejareja na mangapi yamesitishiwa huduma au kufutiwa vibali?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kutambua changamoto iliyopo katika uzingatiaji wa sheria wa maduka haya, hasa maduka ya dawa muhimu, lakini pia kutambua dhamira ya Serikali kuona kama maduka haya yanatoa huduma bora za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kufanya mapitio ya mfumo wa udhibiti wa maduka hayo unaofanywa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba *(TMDA)* na Baraza la Famasi kwa kushirikiana na halmashauri ili kuona kwamba inatoa huduma bora zaidi za dawa, vifaa tiba na vitendanishi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge Bitegeko kwa kazi nzuri anayoifanya na hasa ya kusimamia afya ya Watanzania. Suala la ukaguzi wa maduka ya dawa ni suala linalofanywa mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa makadirio ya mwaka huu wa fedha, maduka zaidi ya 8,600 yamekaguliwa. Kati ya hayo, maduka 1,200 yalikutwa na matatizo mbalimbali ambayo ni 14% ya maduka yaliyokaguliwa. Matatizo yaliyopatikana ni pamoja na kutoa dawa bila kuwa na vibali, kutoa dawa bila wataalamu, kutoa dawa zilizoisha wakati na kutoa dawa bila kufuata utaratibu na maduka haya yalisitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba nitoe rai kwa watoa huduma wote kwamba wanapotoa dawa wafuate utaratibu na kanuni ili kuepuka usumbufu ambao wataupata pale tutakapokwenda kukagua dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili la kufanya tathmini, Serikali inajali afya ya Watanzania na imekuwa ikifanya tathmini kila wakati kuhakikisha kwamba afya za Watanzania zinakuwa imara. Kwa kufanya hivyo, zimekuja na kanuni mbalimbali kila mwaka. Tuna kanuni mbalimbali zaidi ya tano zinazosimamia utoaji wa dawa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumekwenda kufanya tathmini mpya ambayo tutakwenda kuanza na *e-Prescription* kwa maana hakuna ruhusa ya kutoa dawa bila kuwa na cheti. Cheti hicho kitakuwa cheti cha mfumo ili kudhibiti dawa zote zitakazotolewa nchini ziweze kusimamiwa na Serikali ili kuepuka utoaji wa dawa kiholela. Hivyo nitoe rai kwa Watanzania kwamba ni muda mwafaka sasa kutumia dawa kwa kufuata ushauri wa daktari. Kwa sababu dawa yoyote ikitumika bila kufuata utaratibu, basi inageuka sumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tunajua kabisa kwamba wauguzi wengi ndio wanaokuwa na wagonjwa muda mrefu na kutoa dawa, lakini kwa mujibu wa *TMDA* sasa hivi wale wauguzi hawaruhusiwi kutoa dawa katika maduka ya dawa muhimu. Je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kuwarudisha wauguzi wawe wamoja wanaotoa dawa katika maduka muhimu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava

kwa kuendelea kuwapigania Watanzania na hasa akina mama wa Mkoa wa Shinyanga waliomleta humu Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa dawa kwa Watanzania ni jambo la muhimu na hatuwezi kuliacha kiholela kwamba kila mtaalamu wa afya aweze kutoa dawa. Hivyo, ninaomba nitoe rai, kama mtaalamu wa afya anataka kutoa huduma, ziko *course* tunazozitoa kwa ajili ya yeye kuweza kutoa dawa. Hawa wataalamu ambao ni ma-*nurse* wanaweza kupata hiyo *course* ili waweze kutoa dawa kama itawapendeza kusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Janeth Mahawanga, swali la nyongeza.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha inafanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye maduka ya dawa yaliyomo pembezoni mwa miji ili kuhakikisha hii biashara ya uuzaji wa dawa kiholela inakomeshwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninampongeza Mheshimiwa Janeth Mahawanga kwa kusimamia afya ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa ukaguzi wa dawa, hili suala tumelirasimisha. Ukaguzi wa dawa unafanyika Kitaifa, kikanda na kwenye halmashauri zetu. Tuna wakaguzi zaidi ya 760 katika halmashauri zetu wanaoshirikiana na mamlaka hizi katika ukaguzi ili kuhakikisha kwamba huu ukaguzi unafanyika katika ngazi ya chini kabisa kuanzia ngazi ya kijiji. Hivyo, tumefanya urasimishaji na ushirikishaji kwenye ngazi ya chini ili tuweze kudhibiti matumizi ya dawa holela, na uuzaji wa dawa holela kwenye maduka ya dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kamonga, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kumetokea matukio machache ya wananchi wanaoenda kufuata dawa vituo vya afya, wanaambiwa aina fulani fulani ya dawa zinapaswa kupatikana kwenye hospitali ya wilaya. Je, Serikali haioni ni wakati wa kupitia upya sera, kanuni na sheria ambazo haziendani na hali ya sasa na kuzifanyia marekebisho ukizingatia kwamba kwenye vituo vya afya sasa hivi Serikali imeajiri wataalamu wenye sifa zile zile za wale walioko wilayani? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye kwa moyo wa dhati kabisa ameendelea kuongeza bajeti ya dawa kwenye hospitali zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba, upatikanaji wa dawa muhimu katika hospitali zetu upo zaidi ya 80% kulingana na jinsi ambavyo bajeti ya dawa imeongezeka. Hata hivyo, Mheshimiwa Rais ameenda mbali zaidi, amefanya maamuzi ya dhati kwamba sasa ni muda mwafaka wa kuwa na uzalishaji wa dawa katika nchi hii ili kuepuka uhaba wa dawa katika hospitali zetu. Hii ni hali inayodhihirisha dhahiri kwamba sasa tutakwenda kuwa na upatikanaji wa dawa katika hospitali zetu kwa kiwango cha juu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, kulingana na mikakati tuliyonayo ya kuongeza upatikanaji wa dawa katika nchi yetu na kuendelea kusomesha wataalamu na hasa kupitia *Samia Scholarship Program* tumthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutakuwa na upatikanaji wa dawa za kutosha katika hospitali zetu. Pia, tutakuwa na wataalamu makini katika hospitali zetu watakaotoa dawa kwa umakini ili kuendelea kulinda afya za Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Kwa kuwa Serikali ina mpango wa kuanzisha e-*Prescription* ambayo nimeisikia sasa hivi, na kwa kuwa tunafahamu kwamba...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa hujawasha kisemeo chako.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Kwa kuwa Serikali ina mpango wa kuanzisha e-*Prescription* ambayo nimeisikia sasa hivi, na kwa kuwa, tunafahamu kwamba tuna Watanzania wengi ambao wako vijijini na wengi hawajui kutumia simujanja, je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia hawa wananchi wanaopewa *e-Prescription* kwenda katika maduka ya dawa na kuweza kupata msaada wa matibabu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuwajali Watanzania ambao hawana simu, lakini ninaomba niwathibitishie Watanzania kwamba kutokuwa na simujanja hakutomfanya Mtanzania asipate huduma ya *e-Prescription*. *E-Prescription* itapatikana kwa mifumo itakayofungwa hospitalini ambayo itakwenda kusomana na *Pharmacy*. Kwa hiyo, haijalishi una simu janja au hauna, wewe ukishaenda hospitalini utaandikiwa kwenye mifumo ya hospitalini na hiyo *e-Prescription* yako itaenda utaikuta kwenye *Pharmacy* tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni mifumo itakayofungwa kati ya hospitali na *Pharmacy*. Mteja haitaji kuwa simujanja ili kuweza kupata huduma ya *E-Prescription*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge tunakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwetu na majibu kwa upande wa Serikali. Ninaomba niwaletee matangazo kama ifuatavyo: -

Tunao wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Kwanza ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge: Tuna wageni 73 wa Mheshimiwa David Ernest Silinde, Naibu Waziri wa Kilimo ambao ni wanafunzi na walimu wa Shule ya Awali na Msingi Elisabene kutoka Tunduma Mkoani Songwe. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Mwantatu Mbaraka Khamis ambaye ni Ndugu Rukia Mbaraka Khamis, huyu ni ndugu yake kutoka Zanzibar. Karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 31 wa Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, wapigakura wake kutoka Gairo Mkoani Morogoro. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga ambao ni Wasimamizi wa Hospitali na Chuo cha Afya kutoka Ludewa Mkoani Njombe. Ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Jahannes Lembulung' Lukumay, Ndugu Mariam Ally, ni mpigakura wake kutoka Arumeru Magharibi Mkoani Arusha. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni tisa wa Mheshimiwa Onesmo Merdson Mnkondya, ambao ni Wadau wa Shirika la Maendeleo ya Watu kutoka Mbozi Mkoani Songwe. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge pia tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wapo wanachama 60 wa Shirika la *International Peace Information* kutoka Mkoani Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wanafunzi 29 na walimu watano wa Shule ya Awali na Msingi *Rampo Nation* kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana Dodoma, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Nina wachangiaji hapa. Tunaanza na Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanahamisi Athumani Munkunda, Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, ajiandae.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi siku ya leo kuwa mchangiaji wa kwanza kwenye hotuba iliyopo mbele yetu ya Wizara yetu hii ya Nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa usomaji wao wa bajeti, bajeti ni nzuri. Pia, niwapongeze kwa namna wanavyochapa kazi wote wawili pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Zipo changamoto kadhaa, lakini wameendelea kuimarisha, kuonesha uimara wao, hawajayumba na ndiyo hili ambalo sisi tunalitaka sana hasa tunapoona Mawaziri vijana wamepewa ridhaa ya kuiongoza nchi kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo kadhaa ambayo ningetamani leo nichangie. La kwanza, ninaomba nichangie juu ya nishati ya mafuta. Kama tunakumbuka mwaka 2022 mimi nikiwa Mbunge kwenye hili Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilitokea vita ya Ukraine na wenzetu wa Urusi. Kwa namna yoyote ile iliathiri sehemu kubwa ya nishati ya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unakumbuka, Bunge hili kati ya mambo kadhaa ambayo tulishauri na Serikali ikayachukua, yalikuwa ni mengi, lakini mimi nitataja matano pekee yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, kwa kumbukumbu ya Bunge hili; moja, tulishauri na kuielekeza Serikali kuhakikisha mafuta yanapatikana kwa wingi. La pili, kupitia Bunge hili tuliishauri Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutazama na kupunguza ruzuku kwenye nishati hii ya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, tulishauri hapa ndani ya Bunge hili na Serikali ikalichukua, ilikuwa ni kuondoa na kufanya mapitio ya tozo. Serikali ifanye mapitio ya tozo na ikaondoa baadhi ya tozo na shilingi mia mia, zilikuwa zinakatwa kwa ajili ya kwenda *TARURA*, Serikali iliridhia na kuondoa tozo ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne, tuliitaka Serikali kwenda kutoa elimu kwa wananchi kuwaeleza ni nini kilichopelekea nishati ya mafuta ikapungua nchini na ikapelekea kupanda kwa bei. Tukaitaka Serikali kupitia Wizara husika, iende kwa wananchi itoe elimu; kitengo husika cha Wizara kiende kiwaelimishe wananchi na wananchi waelewe. La tano, ilikuwa ni kusimamia bei kwenye vituo vya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili limejirudia tena. Kipekee nichukue nafasi hii kabisa kutoka moyoni, kwanza kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia, na pili, kuipongeza Wizara. Pamoja na changamoto zinazojitokeza duniani, bado Serikali imeweza kuhimili upatikanaji wa mafuta ukilinganisha na nchi jirani zinazotuzunguka. Leo hili pekee yake lingekuwa ni changamoto na hapa ndani pasingekalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru sana na kuipongeza Serikali kwa sababu zipo nchi nyingine ambazo zinatuzunguka, hili tu peke yake limekuwa ni tatizo, achana na tatizo la bei peke yake, hata upatikanaji wa nishati ya mafuta imekuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia pamoja na Mheshimiwa Waziri, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana angalau katika kutimiza majukumu yao na ndilo jukumu la msingi kuwahakikishia Watanzania kwamba nishati ya mafuta inapatikana. Hili ndilo jambo kubwa na ndilo jambo Mheshimiwa

Waziri analolisimamia kwenye Wizara yake. Ninampongeza sana na kwa kweli ninampatia maua yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwa muktadha wa ushauri ule ule wa Bunge, nichukue nafasi hii kuishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha iende ikatazame namna ya kupunguza bei ya mafuta kama tulivyofanya awamu ile iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitashauri mambo kadhaa. La kwanza, kwa kuwa wakati ule tulishauri kwa usikivu wa Mheshimiwa Dkt. Samia na hii Serikali ikaenda ikatazama ruzuku, ninaiomba Serikali, wakatazame hii ruzuku ili kuipunguza na kulainisha angalau upatikanaji wa bei, yaani bei iweze kushuka wananchi waweze kumudu gharama za mafuta nchini. Ninaamini hii Serikali yetu sikivu ina uwezo wa kulifanya hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni lazima Mheshimiwa Waziri arudi kwenye lile jambo la kutoa elimu. Elimu haijakaa sawasawa kwa wananchi. Yawezekana tukachukulia kwamba wananchi wanajua kwa nini bei imepanda, lakini kule vijijini inawezekana hawajui hilo au wanalijua katika mtazamo tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya sana siku hizi kila mtu analizungumza kwa *angle* anayojisikia yeye kulizungumza. Wizara itoke nje ikawaambie wananchi nini athari ya kupanda kwa bei kwa mafuta? Nini kimesababisha? *Measures* gani zinazochukuliwaa, hatua tunayokwenda nayo ni nini kama Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, isiwe elimu ya siku moja. Tunataka kuona elimu inayotoka Serikalini kwenye *instrument* ambayo inaeleweka moja kwa moja. Tusiache mitandao ya kijamii ndiyo ikawa msemaji mkubwa, Serikali ikawa imekaa kimya. Kule vijijini hawawezi kuelewa nini ambacho kinafanyika? Mheshimiwa Waziri, hili analiweza na anaweza kulifanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, nichukue nafasi hii kuishauri Serikali. Ni lazima twende tukatazame pia tozo. Kwenye tozo, mimi nilikuwa nina ushauri. Twende tukatazame tozo inayohusiana na

mafuta lakini tusiende kuipunguza wala kuigusa tozo inayotokana na matengenezo ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakubalina hapa tumeshapitisha bajeti ya TAMISEMI. Maelekezo ya hili Bunge kwa Wizara na ushauri tulioutoa hapa ni kwamba tozo inayokatwa kwenye mafuta ambayo wanakata shilingi 100 inakwenda *TARURA*, wanakata shilingi 100 inakwenda kwenye Mfuko wa Barabara, ambapo shilingi 30 inakwenda *TARURA*, shilingi 70 inakwenda kufanya matengenezo ya barabara zinazotokana na *TANROADS*. Mkienda kuigusa ile mkaiondoa, maana yake mnakwenda ku-*paralyze* matengenezo ya barabara nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tuwe wa kweli, na tuseme ukweli, Wizara iende ikatazame tozo zinazohusiana na mafuta, ipunguze. Mimi siwezi kuwashauri wakapunguze tozo zinazowasaidia barabara wananchi wangu wanyonge kule kijijini. Ambacho kinatakiwa kifanyike kwa Serikali katika hili tozo wanazokata kwenye mafuta, tulishauri hapa na tunaendelea kushauri, wakate ile tozo wapele kule, zisiende tena zikafika Hazina, zikabaki Hazina. Fedha zipelekwe *TARURA* na *TANROADS*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo unaona barabara zilivyoharibika maeneo mengi ni kwa sababu ile fedha haijaenda. Tukienda kuitoa tozo ile tukasema tuiondoe ile fedha, itakuwa tume-*paralyze* matengenezo ya barabara nchini. Sisi kama Wabunge kiukweli tutakwenda kwenye jambo lingine la pili kwa sababu litakuwa lina-*sabotage* uchumi wa nchi hii na sisi hatutaki iende hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo kadhaa ambayo tunapaswa kuyapitia ikiwemo suala la kodi na ruzuku. Kama Serikali, iende ikatazame, maeneo mengine yanaweza kushusha bei ya mafuta na wananchi wakapata unafuu, lakini siyo kushusha tozo. Kwa maana ya kwamba, leo *TARURA* wabaki tena wamekaa kama yatima; *TANROADS* wabaki wamekaa kama yatima wakati tunahitaji ile fedha kwa ajili ya masilahi mapana ya barabara. Yote haya yanawagusa wananchi hawa hawa wanyonge ambao tunakwenda kuwahudumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine baada ya kusema suala la mafuta, nilitaka nirudi ndani ya jimbo langu. Mheshimiwa Waziri tuitazame hii sheria ambayo ilikuwa ikitaja gharama za umeme kwenye maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sheria inasema, pamoja na maeneo yanaweza yakawa ni kijijini, kwa mfano mimi eneo langu ni Mkoma pale Shirati. Pale Mkoma, Shirati ni mji unaoanza kukua, umepewa jina la Mamlaka ya Mji Mdogo, lakini siyo mamlaka ya mji kamili, kwa sababu bado hawana *GN* ya kujiendesha wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu na sheria zinazotumika na watu wa *TANESCO* kuchaji umeme kwamba pamoja na kwamba iko kwenye eneo la kijiji hawalipi shilingi 21,000, lakini wanawachaji shilingi 320,000 wakati wapo miongoni mwa maeneo na maeneo mengi nchini wamekuwa mkifanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama maeneo ni miji inayokua bado hayajafika kupewa *GN* ya kujiendesha kama mamlaka ya mji mdogo na bado haihudumii kama mamlaka ya mji mdogo, ningeshauri Mheshimiwa Waziri, waende wakaitazame hii, walipe shilingi 21,000 kama wanavyolipa wengine ili waweze kunufaika kama wananchi wengine wanavyoenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, tumeona hapa wanazungumza namna ya kuendelea kuongeza vituo vya gesi kwenye maeneo ya Kanda ya Ziwa. Ninaomba Mheshimiwa Waziri atusikilize sana sisi Kanda ya Ziwa, anavyotuona kule na sisi tunatamani tupate ile *incentive* ya gesi. Tunataka wananchi wetu wa Kanda ya Ziwa nao waanze kuwa na *alternative, in case* ikitokea bei ya mafuta imepanda, wawe na *alternative* ya kutumia gesi. Tumeona kwenye mpango namna wanavyokwenda ku-*supply* gesi kule, lakini tungetamani hivi vituo vijengwe Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *population* ya watu wa Kanda ya Ziwa zaidi ya milioni 16 au 17 haiwezekani sisi tukawa tunategemea nishati moja tu ya mafuta wakati tumeona wenzetu wa kanda nyingine wananufaika. Ninaomba sana, kasi hii

iongezeke ili angalau na sisi wananchi wa maeneo yale tuweze kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni pamoja na kukamilisha umeme kwenye vitongoji. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri, wamefanya kazi kubwa sana kuhakikisha umeme unakwenda kwenye vitongoji vyetu nchini na tumeona kazi kubwa kwa kweli kwa muda mfupi. Leo ninajivunia kwamba angalau kwenye vitongoji zaidi ya 74 ndani ya wilaya yangu wamekwenda na Mkandarasi yupo *site*, anachapa kazi ili kukamilisha hii kazi. Ninawapongeza sana katika hili na wamefanya kazi maeneo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia angalau amekwenda kuwasaidia wananchi wetu wanyonge wa kule na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba, kwa kuwa nimebakiza vitongoji 119 na wamesema ndani ya miaka mitano mpaka 2030 vitakuwa vimekamilika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri aweke nguvu kazi, aende akamwinue mama, angalau vitongoji vyote tukifika 2036 kwa mujibu wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi na tulivyowaahidi wale wananchi, umeme uwe unawaka maeneo yote nchini. Ndiyo sehemu kubwa ya sisi kuendele kubaki humu ndani ya Bunge, kwa sababu kama umeme haupo vijijini, kama umeme haujatimia kwenye maeneo yote, tunapata wakati mgumu sisi kuendelea kubaki kwenye haya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa, ni kukatikakatika kwa umeme. Katika maeneo yangu, haiwezi kupita mwezi au wiki mbili wakati wa mvua, lazima tutapata changamoto ya kukatika kwa umeme; na changamoto kubwa ni uchakavu wa miundombinu ya umeme, nguzo pamoja na vitu vingine. Ninaomba Serikali iende ikaainishe hayo maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatamani kwangu Rorya Mheshimiwa Waziri aniletee zile nguzo ambazo ni imara, zile ambazo wananchi wangu wakiwekewa na watu wa *TANESCO*

zitaweza kuimarisha upatikanaji na usambazaji wa umeme kwenye maeneo yetu kwa sababu, nguzo nyingi zimechoka. Mvua ikinyesha zile nguzo zinadondoka, zinasababisha umeme kukatika kwenye maeneo yetu na tunapata athari kubwa sana kwa sababu, umeme ndiyo sehemu ya kuinua uchumi wa maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ninawatakia kila la heri, waende wakachape kazi. Kama nilivyoisema, jitokezeni, nendeeni mkatoe elimu wananchi waelewe, na msiogope kwa sababu, jambo hili lipo kidunia, sio sisi tuliosababisha vita, ila wananchi wanataka elimu, waone namna Serikali ilivyoweka nguvu yake kuhakikisha bei ya mafuta inashuka. Tokeni mbele, semeni haya, mimi naamini wananchi watawaelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jafari Wambura Chege.

Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma tafadhali. Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Kwanza, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri, ameonesha ukomavu na hii inajenga heshima kwa viongozi wetu wakuu kwamba, vijana wanapopewa nafasi wanao uwezo wa kukabiliana na majanga yoyote bila kutikisika. Nina imani angekuwa mzee kwenye hii nafasi, kwa sasa angekuwa anaishi na vidonge kwenye mfuko kwa sababu ya maneno yanayozungumzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninafanya biashara ya mafuta. Nimesikiliza ajenda na hoja nyingi za Wabunge toka tumeanza Bunge letu toka jana. Ni kweli, inaonekana kama tunaisukumia Serikali kwamba, punguza, toa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mbunge wa awamu ya tatu humu ndani. Kazi ya kupitisha bajeti siyo ya Rais, wala siyo ya Serikali, ni kazi yetu sisi wenyewe humu ndani. Huwa tunabishana, tunavurugana, tunafikia muafaka, tunapitisha bajeti. Sasa katikati ya bajeti kama limetokea janga la kidunia, sidhani kama ni sahihi kumsukumia mtu mwingine arekebishe suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni la kwetu, Mbunge yeyote anayeona kuna upenyo wa kupunguza fedha kwenye mafuta, kodi kwenye mafuta, asimame tu atuambie ni wapi? Halafu tuulizane, mimi kwangu siwaogopi wananchi walionichagua, kwa sababu, wananijua na waliniamini niwe msemaji wao, na hii kazi hatutakiwi kusema iwe ya Waziri au iwe ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wabunge ndio wawakilishi wa wananchi, tunajua kwa nini mafuta yamepanda bei. Tutoke sisi wenyewe kwenye majimbo yetu tukaelimishe watu wetu. Mimi binafsi, Musukuma, sikubaliani kabisa kupunguza bei ya mafuta. Hili ni janga la kidunia, na huu ndiyo ukomavu wa nchi yetu. Lazima tukabiliane nalo kwa njia yoyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwangu, barabara ndiyo imeanza kuwekwa lami toka imeumbwa dunia. Tupunguze bei, tukatoe hela ya mafuta, tuache kutengenezewa lami! Hapana. Nitafanya mikutano, hata leo nina mkutano kule jimboni, nitawaambia wananchi wangu jinsi gani mafuta yamepanda na tukubaliane, tujifunge mkanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imeonesha mifano mingi. Tulipata *Corona* humu ndani, sisi Wabunge kuna wenzetu walitangulia mbele za haki. Tulikuwa tunakaa na maplastiki puani, lakini tuka-*save*, hatukuyumba. Nchi nyingine ziliyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunakimbilia kusema tupunguze bei ya mafuta; kuna nchi pamoja na kupunguza na kuweka *incentives,* bado hawana mafuta. Bado bei ni kubwa kuliko! Kwa hiyo, ninawaomba ndugu zangu Watanzania, suala hili siyo la kumsukumia mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaambia, hata tunaotafuta Urais huko mbele, hii ndiyo kazi ya Urais. Huko mbele kuna majanga mengi yatatokea kwa sababu dunia inaenda kasi, ni vizuri mjipange. Sisi Wabunge tutoke tuseme, siyo suala la Waziri, siyo suala la Rais, ni suala letu sisi Wabunge. Twendeni tukaelimishe watu wetu tusije tukaingia kwenye mtego wa akina Heche wa kusema tupunguze kodi. Tulipitisha hizo kodi tukiwa nao humu ndani, mimi nikiwa Mbunge, tunapunguza sehemu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wenyewe ndio tunaomba tuongeze shilingi. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge tukubaliane kwamba, hili ni janga la kidunia, tumwombe tu na kumshawishi ndugu yetu Trump alegeze ili mafuta yaweze kushuka bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri, wala usiwe na wasiwasi, Watanzania walio wengi wanakuelewa. Sasa hivi kila Mbunge anayesema tupunguze mafuta, mwisho wa siku anaeleza anataka *transfoma*, anataka barabara, kwangu hakuna maji. Ukisikiliza maswali, hizo ndizo fedha tunataka tuingie mtegoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania na sisi Wabunge wa CCM tumeandika ilani yetu, tutaitekeleza kwa bajeti ambazo tumezipitisha. Tusiingie huo mtego. Ingekuwa ni janga ambalo liko Tanzania peke yake, mtu yeyote angejua sasa kwamba, kweli tunatakiwa turekebishe wapi, ili tuweze kwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninafanya biashara ya mafuta. Ninarudia kusema, kama Mtanzania mfanyabiashara wa mafuta, mafuta yapo, wala tusiwe na wasiwasi. Mafuta yapo, wala sisi hatuna wasiwasi. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri aendelee na msimamo wake, asimame imara na watumishi wake wa Wizara, tuendelee kupata mafuta. Haijalishi bei, tungekuwa tuna bei kubwa na mafuta hayapo, hilo ndiyo tatizo, lakini kwa sasa nadhani nchi iko salama, tunaendelea kumwombea Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nitazungumza kuhusu umeme. Ndugu zetu wa *TANESCO* na *REA* wamefanya kazi kubwa sana, na kila Mbunge atakayesimama hapa atasema

hivyo. Zamani nakumbuka tukianza hii Bajeti ya Nishati, ilikuwa ni shughuli. Ninamkumbuka ndugu yangu Mheshimiwa Januari, nilimpiga swali hapa, akaniambia mimi simpendi Mheshimiwa Dkt. Samia. Acha kukimbilia kwa Mheshimiwa Dkt. Samia, tuambie umeme; lakini leo ukisikiliza toka tumeanza, kila mtu anasifu *TANESCO* na *REA* wamefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoka kwenye umeme unaokatika wiki, leo ukikatika tunajua ni sababu ya miundombinu, labda nguzo imeanguka na tunataarifiwa na mameneja wetu. Kwa kweli, tunakoenda ni kuzuri. Watanzania tuendelee kuiunga mkono Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kutoa ushauri kwenye *angle* hii kwamba, kweli tumepeleka umeme vijijini, tunasambaza. Umeme ni fursa, kila utakapofika umeme kuna vitu vinaanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa mfano, sisi kwetu vijijini tunaishi kwa kutegemea kilimo. Kila utakapofunguliwa umeme kwenye kijiji zinajengwa mashine. Mashine zile, sisi *TANESCO* na *REA,* tumeweka transfoma za mia mia; zote, zinazidiwa. Kwa hiyo, inakuwa mpaka mtaa fulani msage, mwashe mashine kwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninakuomba, pamoja na kazi zuri iliyofanyika na *TANESCO* na *REA,* tutoke kwenye hizi transfoma ndogo, kwa sasa tufikirie kwenda kwenye transfoma kubwa kwa sababu, watu wanataka kufanya vitu vya maendeleo. Ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri, tulizingatie.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakuwa tuna umeme, lakini ni umeme wa kuwasha balbu peke yake ambao hauwasaidii wananchi. Tunahitaji kuwa na viwanda vidogo vidogo huko tunakotoka, lakini tatizo linakuja, wakiwasha umeme tu, labda mashine tano, transfoma imezidiwa, inazima. Kwa hiyo, ninamwomba sana Mheshimiwa, kwenye bajeti yako lizingatie hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwa sisi tunaotoka vijijini, kila Mbunge atakayesimama hapa atasema tu, kama alivyosema mwenzangu, kuna *centr*, zimepewa mamlaka ya mji

mdogo. Yaani kunakuwa na tofauti ya hizo bei, unaambiwa hapa ni mjini, hapa ni hivi. Tunaomba, kama tumeamua kusema vijijini ni shilingi 27,000, tuache kuwa na ndimi mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili. Watanzania hawataki kusikia kitu kinaitwa *REA* na *TANESCO*, kuna huo msuguano kule vijijini; wanakwambia huu ni mradi wa *TANESCO*, au huu ni mradi wa *REA*. Watanzania wanajua mwenye umeme ni *TANESCO* peke yake. Sasa nadhani muweke mkakati wa pamoja, ambao tusiwachanganye wananchi, kujua huyu ni nani na huyu ni nani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, tuko kwenye kipindi kigumu sana, tunaendelea kumwombea Mheshimiwa Waziri. Yeye ni kijana, ni moja ya Mawaziri vijana humu ndani. Naomba nimwambie, simama, utapigwa mishale, utasemwa, lakini huo ndiyo ukomavu. Yajayo yanafurahisha. Tunatamani kuliona baraza la vijana watupu kama mtaweza kupambana na majanga kama haya na mkaweza kujisimamia. Niaomba sana endelea na moyo huo, simamia Wizara yako, usiogope kupigwa mishale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, na Mungu akubariki. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Musukuma.

Nilimtaja Mheshimiwa Esther Matiko, lakini ataanza Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Matiko, halafu Mheshimiwa *Eng*. Ezra John Chiwelesa.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara yetu hii ya Nishati. Ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, aliyetujalia afya njema na hatimaye kutupa hekima na busara ya kuendelea kulipigania Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri wetu, Mheshimiwa Naibu Waziri na timu yao yote kwa namna

ambavyo wanafanya vyema, wanapambana kwa ajili ya kuhakikisha hali ya usalama wa nchi yetu inakaa sawasawa kwa sababu, umeme ndiyo kila kitu sasa hivi, lakini tukizungumzia suala la mafuta, yote haya tunayaingiza kwenye suala la usalama. Wamekuwa watulivu, tunawashukuru sana kwa utulivu wao na hekima.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumshukuru pia, Mheshimiwa Rais kwa busara zake ambazo ameweza kuzionesha ndani ya Taifa letu na ulimwenguni kote. Wapo waliokuwa wanajaribu kumchokonoa, lakini amesimama, ameonesha hekima, busara na uongozi. Kaweza kuliweka Taifa letu na utulivu, mpaka sasa nchi imetulia. Tunampongeza na tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumjalia hekima na busara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze na suala zima la utumiaji wa gesi kwenye magari, pamoja na umeme. Tumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, ametuletea magari yanayotumia umeme, tumeyaona, na pili, tumeona magari yanayotumia gesi. Mheshimiwa Rais ametangaza suala zima la kupunguza matumzizi ya mafuta ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nikawa najaribu kuwaza, Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla wake watanisaidia, ni kwa nini Serikali hawataki kutumia umeme na gesi, ili tuweze kupunguza matumizi makubwa ya mafuta yanayotumika Serikalini? Wakitumia wao itatia chachu kwa watu wengine binafsi kwenda kutumia nishati hizo na kuanza kupunguza matumizi ya mafuta kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali yenyewe haijaamua kwenda kutumia nishati ya umeme kwenye magari, na kutumia nishati ya gesi kwenye magari, bado na sisi Watanzania tutabaki na mashaka na kuvuta miguu kwenda kutumia hiyo nishati mbadala kwenye vyombo vyetu vya usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri akija, atuambie, ni kwa nini Serikali haitufikirii? Ama hatuoni umuhimu wa kutumia hizi nishati mbili mbadala ambazo zinaweza

kutusaidia kupunguza gharama kubwa ya mafuta kwenye Taasisi zetu za Serikali kwa ujumla wake?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ambalo natamani kusema siku ya leo, kwanza tumshukuru sana Mheshimiwa Rais, kuanzia mwaka 2024 baada tu ya kuingia madarakani aliamua kujipambanua, akaamua kuwa mwanamazingira na kuhakikisha tunatoka kwenye suala zima la utumiaji wa kuni, kwa maana ya kukata miti yetu, na kuharibu uoto wa asili ndani ya Taifa letu. Akatoa mitungi mingi sana kwenye halmashauri na maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wengi walifurahia kwa sababu, imewarahisishia namna ya matumizi. Ile mitungi iko kule vijijini mpaka leo. Changamoto iliyoko leo ni bei kubwa ya gesi iliyopo. Kwa hiyo, wananchi wetu baada ya kuwagawia ile mitungi, awamu ya kwanza, bei ni kubwa wanashindwa kumudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni upatikanaji wa gesi maeneo ya vijijini. Mfano kwangu Chemba, baada ya ule mtungi kwisha, hana mahali pa kwenda kuikuta hiyo gesi na kujaza. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ione ni namna gani ya kuliangalia suala la upunguzaji wa bei ya gesi na upatikanaji kwa urahisi. Hilo tunaomba mtusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninaomba tuwekeeni basi mita ya kwenye ile mitungi, ili mama wa Chemba anapopika ajue gesi yake imebaki kiasi gani? Hii biashara anapika, kagesi kanakatika, ugali ndiyo kwanza *ya kuvuga baali yakago, bwana ndugu yangu gwegwe*, unakuta sasa tena mzee huko anakula ugali mbichi. Kwa hiyo, tusaidie kaka Deo, twende kwenye teknolojia, tuwekee mita ambayo inaweza kuonesha mtungi wake gesi imebaki kiasi fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba sasa niseme mambo yanayowahusu Wanachemba. Mheshimiwa Waziri Wilaya yangu ya Chemba anaifahamu, ni Mwanadodoma mwenzangu tunakutana kwenye vikao vingi. Wilaya yangu changamoto ya kwanza kwa Watumishi wa *TANESCO,* hawana gari dogo wala kubwa, kwa maana ya lile la kubeba nguzo, la *crane* kwa hiyo, naomba sana tusaidiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wilaya ile ni kubwa, magari wanayoyatumia leo, tunamshukuru Meneja wetu wa Mkoa, kaka Shamba, anapambana, ni ya kukodi na gharama ya kukodi ni kubwa. Kwenye suala la magari hapo, wilaya yetu sisi imegawanyika kwenye kanda mbili. Tuna Kanda ya Magharibi na Kanda ya Mashariki. Kwa hiyo, tuna magari ambayo yamekodiwa pale wilayani, lakini kwenye hizi kanda mbili kwa Mrijo pale tunakodi gari, na ukija huku Kwa Mtoro pia, kwa ajili ya kuharakisha huduma, nako tumekodi gari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Wizara ione namna ambavyo wanaweza kutusaidia, tupatiwe magari ili wananchi wetu waweze kuhudumiwa kwa urahisi na hatimaye waweze kuendelea kufanya shughuli zao za kulijenga Taifa lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu la pili ni suala zima la nguzo. Wilaya ya Chemba tunahitaji nguzo, na nguzo tunazozihitaji, ni za zege. Kwa nini tunahitaji nguzo za zege?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji nguzo za zege kwa sababu, Wilaya ya Chemba tuna changamoto kubwa sana ya mchwa. Kwa hiyo, kila tunapoweka nguzo hizi za kawaida zinaliwa na mchwa. Pili, maeneo mengi sisi ni mkondo wa maji, kwa hiyo, nguzo zile mara nyingi zinaoza kwa sababu ya kukutwa na maji mengi. Tukisaidiwa nguzo za zege zitasaidia sisi kuwa na umeme wa uhakika usiokatika wala uangukaji wa nguzo, na gharama kubwa ya kurudia yale maeneo kwa uharibifu wa nguzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji nguzo kubwa 822. Tukitupatiwa hizo, sisi tumemaliza, hatudai tena, yaani tutakuwa tumefunga kazi kwenye suala la umeme mkubwa, kwa maana ya hizo nguzo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme wa mjazilizo kwenye vitongoji vyetu ambavyo *REA* wamefanya halafu tunawaachia *TANESCO*, hebu tusaidieni, tunawaomba nguzo 300, hata hizo nazo kaka yangu haiwezekani! Kwa hiyo, naomba *this time* nisaidiwe nguzo 500 ili niweze kufikishia umeme shule zetu, zahanati zetu, pamoja na visima vya maji na taasisi za dini

tulizonazo. Tukipatiwa nguzo 500 awamu hii kwenye bajeti hii, tutakuwa tumesukumwa kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ninatamani kulisema ni kama wenzangu pia walivyosema. Jimbo la Chemba, Kijiji cha Chemba, siyo mji, wala siyo mamlaka, wala siyo kitu chochote. Maeneo yote, vijiji 113 wanaunganishiwa umeme kwa shilingi 27,000 lakini tukija Chemba Mjini pale ni shilingi 320,000. Watu wanakosa majibu, na wanauliza, hivi Chemba imekuwa Dodoma Jiji? Ama Chemba imekuwa kitu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, wanatamani kusikia majibu ya Mheshimiwa Waziri. Hili siyo ninaomba, ninamsemea na yeye, Chamwino hali kadhalika ni vivyo hivyo, wanalalamika na suala zima la vijiji vyetu hivi kuwepo kwenye mifumo ya miji, kitu ambacho hatuwatendei haki. Wanatamani kusikia Kauli ya Serikali kwamba, ni lini Serikali itawapa fursa ya kutumia huduma ya shilingi 27,000 kwa ajili ya kuunganisha umeme kwenye kaya zao badala ya shilingi 320,000 kwa sababu, wako vijijini, hawako mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu la mwisho ninaomba niwashukuru sana, lakini Mheshimiwa Deo, Kata yetu ya Farkwa, wataalamu wao walikuja, kuna eneo ambalo sijui lina maji moto, sijui lina uji moto, sijui lina vitu gani? Walikuja wakapima pale, wakapata majibu, wakaondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ile hali namna inavyozidi kuendelea, wananchi hawana majibu na wamejawa hofu. Ninaomba tusaidiwe, ije timu yake itupe majibu. Lile eneo pale kuna kitu gani? Siyo ajabu kunaweza kukawa na mafuta pale ndugu yangu, tukawa matajiri Chemba ghafla bin vuu! Kwa hiyo, tunaomba waje wapime.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, waweze kutusaidia kutupa elimu kwamba, kile kitu ni nini? Wanaposikia na kuona, waone ni kitu cha kawaida ama muwape tahadhari ya nini cha kufanya, badala ya kuendelea kuwa na taharuki inayoendelea pale kwenye ile kata. Wananchi wengi wamekuwa hawaelewi na wengine wameamua kuhama kabisa, wamesogea kwa sababu

ya ule mngurumo na vile vitu vinavyotokea pale vinakuwa vinawapa mashaka sana kwa maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa muda wako. Ninawashukuru na ninawapongeza kwa kazi kubwa mnayoifanya na Mungu awabariki sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, atafuatiwa na Mheshimiwa *Eng.* Ezra John Chiwelesa. Mheshimiwa Chiku Athman Issa ajiandae.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuweza kunipatia na mimi fursa ya kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana kwa mustakabali wa uchumi wa Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, ninaanza kwa kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada ambazo ameonesha kwenye sekta hii muhimu sana ya nishati kwa kuhakikisha kwamba kunakuwepo na ongezeko la uzalishaji wa umeme, usambazaji, na zaidi kuhakikisha tunavutia wawekezaji wengi kuja kuwekeza nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita zaidi kwenye kuhakikisha ninashauri Serikali kwenye *mix energy,* maana yake sasa hivi kuna vyanzo vingine hatuvitumii kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tukubali kwamba sasa hivi kasi ya uchumi Tanzania imekua. Kuna uzalishaji mkubwa sana na miradi mikubwa mingi ya kimkakati. Mathalani, tunao mradi wa kimkakati wa Liganga na Mchuchuma, lakini kuna mradi mkubwa unakuja wa reli ya umeme ambao unaenda kuunganisha na Maziwa Makuu. Reli hii itakuwa inahitaji umeme, na pia itaenda kuweka uchumi shindani katika Taifa letu kikanda na hata Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunatambua tuna wawekezaji wengi tumewavutia kuja Tanzania kwenye viwanda, sekta ya

kilimo, ufugaji na uzalishaji mbalimbali ambao utahitaji umeme toshelezi wa uhakika na wa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo nitapenda sasa kujielekeza kwenye kuangalia uhalisia rasilimali ambazo tumejaliwa na Mwenyezi Mungu. Kwa sasa hivi tunazalisha *megawatt* 4,075, 4,300 *something like that,* lakini uhalisia, tungechukua na rasimali nyingine ambazo tumejaliwa ambazo pia zingeweza kuzalisha umeme mwingi na toshelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, nikirejea umeme wa jua, nilikuwa najaribu kufanya tafiti, kwa Tanzania napongeza Machi, 2026 tumefungua ile *plant* ya pale Kishapu ambayo ina-*generate 50 megawatts* na mna-*plan* kuongeza zifike *100 megawatts,* ziwe 150 kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jinsi tulivyojaliwa na Mwenyezi Mungu, umeme wa jua, sisi majira ya huku Tanzania tunapata jua kwa muda mwingi sana, na tungeweza kutumia umeme wa jua, pamoja na kwamba inawezekana ikawa na *initial investment cost* ikawa kubwa, lakini tukishawekeza tunapata umeme mwingi na wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilijaribu kufanya tafiti tu ndogo kwa ukanda wetu wa *SADC Africa,* lakini na nchi nyingine, ukizingatia Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ni kinara wa nishati safi, umeme wa jua ni nishati safi. Nikajaribu kuangalia Afrika Kusini wenyewe wana-*generate 12,000 megawatts* za umeme wa jua na wamefanya hivyo kwa sababu wameshirikisha pia na *private sector* kupitia *PPP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi Tanzania ifike wakati pia tusiache zigo lote kwa *TANESCO,* yaani wazalishe, wasambaze kila kitu! Tukaribishe *PPP*. Kwenye dira ya 2050 tumesema kwamba tunawakaribisha *private sector*. It's like *they are engine* ya hii kitu *70%* ya *private sector*. Kwa hiyo, tu-*introduce* hii *PPP* kuhakikisha tuna-*generate* umeme wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikajaribu kuangalia pia Misri *so far* wana *300 megawatts* lakini *they plan* ku-*add* mpaka wafike 6,500

na kitu *megawatt*. Ukiangalia hali ya hewa ya Misri na *South Africa* siyo kama kwetu huko kuna kipindi wanakuwa na *winter,* sisi kwetu Tanzania maeneo mengi ni jua, lakini tuna-*generate only 50* mpaka leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikajaribu kwenda Spain, wenyewe *as we speak* wana-*generate 50,000 megawatts,* yaani 50 *Gigawatts.* Mwaka 2025 tu wali-*generate* 8,700 *megawatts.* Sasa Spain napo ukiangalia majira yake na kwetu kwa kweli *it's a high time,* Serikali ifanye tafiti ya kina kama ni kuweza kuchukua hata mikopo, na bahati nzuri *the President* ana *political will* ya kuhakikisha anawekeza huku.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutumie nyakati za Awamu ya Sita kuhakikisha watendaji ambao wamedhaminiwa; Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wa sekta hii kwanza tunawapongeza, *they have been doing* vizuri kabisa, lakini tutumie hizi *alternative source* kuhakikisha tunajaziliza tuweze kufika mbali zaidi, ili hizi shughuli zote na miradi ya kimkakati ambayo tunaiweka, iweze ku-*pick* bila kupata kikwazo chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hilo lilikuwa ni la kwanza, tufanye tafiti za kina, tupeleke wataalamu wetu wajifunze kwenye hii miradi, kwa sababu inawezekana kuchukua *expert* kutoka nje ni *expensive,* lakini pia tutafute *source,* hiyo *private sector* na kama kuna *grants* zinapatikana, tuwekeze hapa. Hiyo kusema kwamba *152* tuna-*relax,* hapo siyo vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nikaangalia kwenye jotoardhi *(the geothermal)* na yenyewe tumebarikiwa sana. Kwa Tanzania nimejaribu kuangalia maeneo 50 yana hii *geothermal* takribani mikoa 16, lakini mpaka sasa hivi, pamoja na kwamba mwaka huu wa fedha 2026/2027 mmeanza kule Mbeya sijui na wapi ambapo ninatarajia ku-*generate 30 megawatts* na mpaka kufikia *130 megawatt by 2030, I think* hizi ni ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kuangalia tu nchi jirani ya Kenya *by now* wana-*generate almost one gigawatt* ya *geothermal.* Ukiangalia maeneo yetu tuliyonayo ni mengi sana, na *their target by 2030* sisi tunasema *130 megawatts* wenzetu

Kenya *they are targeting* ku-*generate 10,000 megawatts* kwa maana ya *10 gigawatts, 10,000 megawatts;* ni mara mbili ya umeme ambao tuko nao sisi Tanzania, na ukizingatia tulivyobarikiwa, sisi tunatakiwa tutumie hii rasilimali ambayo Mwenyezi Mungu ametubariki. Tulitakiwa sasa hivi tuwe tunazungumzia zaidi hata ya *megawatts 20,000* ukiangalia hizi *source*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba sana Waziri na wataalamu wakoetuende na hii kasi ya Mama, kwa kuwa ana hiyo *political will,* tuhakikishe tuna-*exhaust* hapa, hiyo *130 by* 2030 *is a peanut*. Naomba Serikali iende i-*revisit* tuone ni njia gani nyingine ambazo tunaweza tukatumia hata kuwavutia hao *private sectors* tu-*push*. Wenzetu Kenya sijui ni *source* ngapi tu hizo mbili walizonazo, lakini *they are targeting by 2030, 10,000 megawatt*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumeona hii *crisis* ya mafuta na usalama wa nchi yetu na nini, *a lot of prial* lakini tunaweza tukajiondoa kabisa kutegemea mafuta na *petrol, diesel and the likes,* tumebarikiwa madini ya *graphite, nickel, phosphate lithium.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo madini, pamoja na kwamba Serikali inatambua wameweka jitihada kubwa sana kuvutia wawekezaji kuja hapa, lakini *as we speak* tumefanya tukiyasafirisha kama malighafi tu, kama makinikia kwenda nje, nchi za Ulaya na Asia wana-*benefit* madini yetu *from Africa*. Wao wanatengeneza betri kule ambazo zinakuja kutumika kuhifadhi hata umeme kama unatumia jua au hiyo *geothermal,* mengine yanatumika kwenye magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, *it is high time,* kwetu tuna madini ya kutosha, tutumie *graphite,* tutengeneze viwanda hapa Tanzania, tutakuza uchumi wetu, tutakuza ajira, lakini zaidi tukiwa na betri, tutaondokana hata na *false fuel emission*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mama ni Balozi wa Mazingira hapa Afrika, lakini tutahakikisha tunakuwa na magari yanayotumia umeme, tutahakikisha tunakuwa na uhakika wa umeme kama ni wa jua, tunatumia betri ambazo tunazizalisha hapa hapa

Tanzania; tutahakikisha tunasonga na kuwa shindani hata kuweza kuuza kwenye mataifa mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tu-*exhaust* kwenye *graphite* na haya madini tusiache yakae tu *merely* kama madini. Twende mbali zaidi yaweze kuleta tija kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye *LNG* na *gas,* ina *CNG,* tumebarikiwa nazo pia. *Last year* nilichangia hapa kwenye bajeti nikasema *by then,* sasa hivi tukichukua hata mfano wa Ethiopia wenzetu wamewekeza pale, *electric vehicle* na hizo *gas,* Sisi Tanzania tuna zote tumebarikiwa, zikiwa na hizo *battery* tutatumia kwenye *electric vehicle.* Tukitengeneza *LNG* na *CNG* zikaenda kote zitoke Dar es Salaam tuweke kwenye miji yote mikuu na njia zote ambazo zinapitika kuunganisha Tanzania yote, tuhakikishe kuna hizo gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunaweza tukafanya kwa *petrol,* kwa nini hata hizo gesi zisiwepo, ziweze kuwa *transported* kote, tuhakikishe kwamba tunatoa hata vivutio vya kodi Watanzania binafsi, mabasi, malori na magari yote yaweze kutumia *gas,* na umeme. Ikiwa hivyo, hatuna hata tishio. Hata mafuta yasipatikane, *we are good to go.* Haya mambo ya kuwa tunapata *pressure* kwa vitu ambavyo Mwenyezi Mungu ameshatubariki ndani ya nchi yetu kuweza kuachana na kuwa tegemezi wa *petrol* na *diesel,* siyo *fair* kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kule Dubai baada ya hii *crisis* licha ya kwamba wana mafuta, lakini hawakupata kabisa ku-*loose their sleep* kwa sababu wanakosa mafuta. Wamepata *disaster* kwenye *tourism* kwa sababu gani? Wenyewe wanatumia magari ya umeme na magari ya gesi, *they are less dependent* kwenye mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania *we should go and do that* kwa sababu tumebarikiwa kila rasilimali. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Esther Matiko. Nilimtaja Mheshimiwa Injinia Ezra John Chiwelesa, atafuatiwa na

Mheshimiwa Chiku Athman Issa na Mheshimiwa Arif Suleiman Premji ajiandae.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye bajeti hii ya Wizara ya Nishati ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nichukue nafasi hii kumpongeza sana Rais kwa kazi kubwa ambayo inafanyika, kazi ya kuwaletea wananchi nishati bora ya gesi, hali kadhalika nishati ya umeme ambayo inaendelea kusambazwa, na zaidi tukizingatia siku 100 zilizokuwa zimeahidiwa. Ilisainiwa mikataba ya kupeleka umeme kwenye vitongoji 9,009, kwa hiyo, tuna hakika neema inaonekana kwenye eneo hili. Tunampongeza sana Waziri na watu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ni kubwa na inafanyika. Tunachoomba tu ni usimamizi ili hawa wananchi waweze kupata umeme kwenye vitongoji tukisubiria vitongoji vingine vitakavyofuata kwenye awamu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wenzangu walivyosema, Waziri kipindi linatolewa tangazo la kubadilika kwa bei, na baadhi ya maeneo yakawekwa kwenye shilingi 320,000 na mengine yakabaki 27,000, mimi ninakumbuka niliandika barua tarehe 23 Januari, 2023 na barua yangu ipo na nimefuatilia nyakati zote mpaka tunavunja Bunge lililopita, tukaambiwa *list* ilikuwa huku kwa sababu haikuwa sehemu moja tu, ilikuwa ni nchi nzima. Kwa hiyo, tukawa tunatarajia tupate majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tungeomba hili jambo lifanyike haraka kwa sababu hata ilipokuwa shilingi 27,000 tu, baadhi walikuwa hawawezi kuunganisha. Sasa inapopandishwa ikaenda juu zaidi inakuwa *disaster* kubwa kabisa, kwa sababu ukipita kwenye maeneo mengi ya miji, wale ambao wanaonekana ni wa mjini kabisa walishapata umeme siku nyingi. Kwa hiyo, walio pembeni ndiyo wanaojenga na maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wale bado wanapambana tuone jinsi ya kuwasaidia ili irudishwe shilingi 27,000 na wao waweze kupata hii nishati, hatimaye waweze kuendana na wenzao. Hilo ni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Serikali inafanya *distribution* ya hii miradi mipya, kuna jambo ambalo tume-*observe* huko tunapokuwa vijijini. Unakuta baadhi ya maeneo tunagawa nguzo 60 *flat rate* kwa vitongoji, lakini vitongoji nchi hii havilingani. *As long as* kinaitwa kitongoji, kila kitongoji tunakipa sawa. Unakuta wengine wana nguzo tu zimebaki hazina kazi, zimesimama tu hamna hata uunganishaji, halafu baadhi ya maeneo watu ni wengi, walihitaji umeme, waweze kupata huduma ile, lakini hawawezi kupata kwa sababu tumewa-*limit* kwa zile nguzo za *REA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tulione hilo, kama inawezekana tuhusishwe. Kama ni vitongoji labda 60, Wilaya fulani tunajua idadi nguzo ni hizi, wakafanye *feasibility study* kabla ya kufanya *distribution,* ujue kabisa eneo hii inaweza ikabeba nguzo 30, hapa *transformer* tuweke aina gani? *Sometimes* wanapeleka *transformer* kubwa ambayo haiwa-*sustain,* wakati wengine ni wengi halafu *transformer* huenda ni ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tulione hili ili tuweze kusaidia wananchi umeme usiwepo wa kuwashia hata lakini uwepo wa kufanyia kazi za kuwaletea maendeleo hatimaye na wao waweze kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi niliongea kwa habari ya umeme wa kwenda kwenye baadhi ya maeneo ya kimkakati. Kwa mfano, vituo vya afya, kuna miradi ya maji, lakini vilevile, shule nyingi hazina umeme, kwa sababu shule unakuta ziko pembeni, vituo vya afya vimekaa pembeni, miradi ya maji iko pembeni. Sasa unapopeleka hizi nguzo, *sometimes* zinaishia tu kwenye *center* zile ambazo zina watu, maana huwezi kupeleka umeme kule, na wananchi wakakosa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tulione hili, tuliandikie *package* maalum. Bahati nzuri Mheshimiwa Rais ni msikivu, Wizara

iandike andiko zuri wapeleke, na tuna hakika atafanya. Kama amefanya mengi haya, ile hatashindwa kufanya, kuliko kupeleka mradi ukakaa, halafu hauna umeme, baadaye watu hawafurahii ule mradi na wanaona kama vile umeenda kuwa mzigo tu ambao hauwasaidii, wanaona miradi mingine ni kama *white elephant* kwa sababu haiwezi kuwasaidia. Walione hilo waweze kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho nataka niongelee ni suala zima la mafuta. Kipekee nisimame ndani ya Bunge hili kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa. Wenzangu waliotangulia wanaweka kwenye lile Bunge lililopitam ninadhani tunakumbuka *issue* ya Russia na Ukraine ilitufundisha jambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipokaa humu ndani kuishauri Serikali, ilichukua hatua, ndiyo maana tarehe 17 Oktoba, 2024 ulisainiwa mkataba mkubwa wa kujenga *farm tank* kubwa ya lita takribani milioni 378 au *cubic meter* 378,000 yenye gharama ya shilingi bilioni 678. Kwa hiyo, Serikali ilichukua hatua na ikasikiliza maoni ambayo tuliyatoa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo lazima tupongeze, ni kazi kubwa imefanyika. Hii fedha ingeweza kwenda kwingine, lakini tunaweka *reserve* ya mafuta kwa ajili ya kuilinda nchi, na huu utata unaokuwa unatokea, kwa sababu ilikuwa Ukraine leo, kesho hatujui tunaenda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba nimejaribu kupiga hesabu zangu tu za kawaida, nikawa najaribu kuona mafuta yanavyozidi kuwa na gharama kubwa, kwa sababu mafuta yakipanda bei, yaani hata kuyasafirisha tena unaongeza gharama nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mafuta yanavyoongezeka na anayesafirisha mafuta yale yale kuyapeleka Biharamuro, naye ana gharama anayoiongeza kwa sababu yamepanda, kwa sababu na yeye anatumia mafuta kuyaleta Biharamuro, bado anatumia gharama nyingine kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunachotakiwa kufanya ni nini? Nimejaribu kwenda haraka haraka nikawa nimewaza, kama Taifa, tuna haja ya ku-*shift* sasa kutoka kwenye kusafirisha mafuta kwa kutumia matenki au magari, tukaanza kutumia *pipeline*. Kwa nini nasema *pipeline?* Nilipiga hesabu, tunatakiwa tujenge *storage farms* nyingine hapa, hizi *farm tanks.* Hatuwezi kubeba tu Dar es Salaam, mtu anatoka Bukoba, anatka Burundi, au wapi, lazima afuate mafuta Dar es Salaam, haitawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa hili linakua na sisi ndio *saving hub* ya majirani zetu. Kama ni *saving hub* ya majirani zetu, ni lazima tuone jinsi ya kufanya mradi huu badala ya kujenga *storage farm* zote Dar es Salaam tuweke nyingine hapa Dodoma, tuweke nyingine Mwanza kwa ajili ya Kanda ya Ziwa. Wanaotoka Burundi na maeneo mengine, hata Uganda, wanaweza wakachukulia Mwanza pale, ikawa kuna *storage farm* kubwa, wakachukulia pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikawa napiga hesabu, leo mmejenga *storage farm* ya lita milioni 378, ukifanya *distance* ya kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma ambayo ni kilomita 450 ni sawa na mita 450,000. Ukichukua bomba lenye kipenyo cha milimita 600 ndani ile bomba pekee yake, kwa sababu mafuta yakija hayataisha kwenye ile bomba, kwa hiyo, bomba pekee yake ile itakuwa *storage farm* ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ile *storage farm* ya bomba pekee yake kwa Dodoma nilikuwa napiga hesabu inaweza ikabeba *cubic meter* 127,000 sawa na lita milioni 127 yatakayokuwa kwenye bomba muda wote. Kwa hiyo, uliyojenga hapa yanavyo-*pump* yakajaa, magari yanavyochukua kwa sababu yapo kwenye *system,* yanazidi kuja, maana yake ile bomba iliyolala pale ni *storage farm* nyingine itakayosaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikapiga hesabu kutoka hapa kwenda Mwanza kuna kilomita kama 686. Kilomita 686 ukipiga hesabu bomba litakalolala hapa kwa kipenyo cha milimita 600 ile ile litakuwa limebeba mafuta takribani *meter cubic* 193,000; au lita milioni 193 ya kubaki kwenye bomba tu. Dar es Salaam mpaka Mwanza ni takribani lita milioni 321, *almost* sawa na ile *storage*

*farm* mnaojenga Dar es Salaam na bado mtakuwa mmejenga tenki kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukishafanya hivyo itatupunguzia nini? Kwanza, barabara hizi ambazo tunaweka tozo nyingi sana kwa ajili ya kuzilinda zitapungua. Magari mengi hayo unakuta yana matenki labda ya lita 45,000; haya magari ni mazito, kwa hiyo, yanavyotembea kwenye barabara yanaharibu barabara zetu na bado tunaendelea kuchaji na *life time* ya barabara za lami zilizo nyingi ni miaka 15 mpaka miaka 20, inabidi ibadilishwe au ifanyiwe *repair.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tukiweza kupunguza haya mambo yanayofanyika, kwanza gharama ya usafirishaji wa mafuta itashuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninaangalia huku wanavyoelezea, ambao wametumia hizi, kwamba usafirishaji wa lita moja katika magari inaenda kati ya dola 0.03 mpaka dola 0.06, lakini ukiangalia kwenye *pipeline* inaenda kati ya dola 0.01 mpaka dola 0.02.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unaweza ukaona gharama itapungua hata ya kusafirisha, na itatuwezesha tuwe na mafuta ya uhakika. Hapo huongelei ajali, hakuna mtu sijui anasema mafuta yameibiwa, huongelei foleni, vitu vitakuwa vimerahisishwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zile zile ambazo tunataka tukajenge *storage farm* nyingine ili tuziongeze, basi tuzilete Dodoma tujenge *pipeline,* twende mpaka Mwanza ili iweze kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaosafirisha mafuta kwenda Nyanda za Juu Kusini watakuwa wanachukulia Dodoma kwa sababu kutoka Iringa kuja hapa wanapounganisha ni rahisi zaidi; wanaotoka Burundi wanaotoka kwetu tutachukulia mafuta Mwanza itatusaidia kwanza nchi, tunaweka kwenye usalama zaidi wa mafuta kwa sababu mafuta yako kwenye bomba, na mengine yako kwenye matenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, hata kama kutatokea *disaster,* bado tunakuwa na uhakika wa mafuta yaliyopo kwenye bomba, yanatosha kwa siku 20 mpaka 30, mengine tulionayo kwenye matenki yanatosha. Kwa hiyo, Taifa tunaweza kusimama hata kwa siku nyingi zaidi kipindi *stabilization* inafanyika kule nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niliona niliseme hili liweze kusaidia tuone sasa tu-*shift* kutoka huko tuje huku ili hatimaye tuweze kusaidia kuipeleka hii nchi mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, kipekee kabisa ninapomalizia, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri, amekuwa msikivu, simu anapokea, kila wakati anapotafutwa anajibu. Dada yangu Mheshimiwa Salome hapo, Naibu Waziri, Wizara imepata wenyewe. Kikubwa, tuko tayari kuwasaidia na kuwapa ushirikiano kama hivi, ili tuendelee kulipeleka hili Taifa mbele. *Big up,* mnafanya kazi kubwa zaidi ya kumsaidia Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsanteni sana, na Mungu awabariki. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ezra John Chiwelesa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Chiku Athman Issa atafuatiwa na Mheshimiwa Arif Suleiman Premji, Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima ajiandae.

**MHE. CHIKU A. ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana na mimi kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Nishati. Kwa vile ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge hili Tukufu, ninaomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema aliyetuwezesha kufikia siku ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kumshukuru Rais wetu Jemedari wetu, Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa heshima kubwa aliyonipa yeye na vikao vyake, jina langu kupendekezwa na hatimaye kuteuliwa na kuwa Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Arusha. Ninasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani zangu za tatu ziende kwa wapiga kura wangu wa Mkoa wa Arusha, Wanawake wote wa Mkoa wa Arusha. Ninawashukuru kwa kunipa dhamana kubwa ya kuja kuwawakilisha kama mwakilishi wao, na mwanamke ambaye nimekuja kuwasemea kero, maoni na kutoa ushauri kwa Serikali. Ninawaahidi kwamba nitafanya kazi kwa weledi, unyenyekevu, utii na sitawaangusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa shukurani, ninaomba nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Rais. Sisi wote ni mashahidi, kazi zinazofanyika katika nchi hii, ni kazi kubwa sana. Mheshimiwa Rais ameibeba nchi kama alivyobeba familia yake na watoto wake nyumbani. Anafanya kazi usiku na mchana, anafanya kazi bila kuchoka, Mheshimiwa Rais anafanya kazi kwa ajili ya kuitoa Tanzania kutoka *level* moja kwenda *level* nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba tumhakikishie Mheshimiwa Rais wetu, sisi wanawake wa Tanzania tupo nyuma yake tunamuunga mkono. Akanyage mwendo, sisi tupo, tutaendelea kumsemea mahali popote na kuhakikisha kwamba yale maono yake yanatimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais, ninaomba nichukue nafasi hii niipongeze Wizara ya Nishati. Nianze kwa kumpongeza mdogo wangu Mheshimiwa Deogratius Ndejembi kwa kazi kubwa anayoifanya. Pembeni yake ana jembe lingine, mdogo wangu Mheshimiwa Salome Makamba. Kwa kweli wanafanya kazi ambayo inaakisi ujana wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati sisi tukiwa na umri wao, tulifanya kazi wanazozifanya, na ninapowaona wanapokimbia, mimi ninaona fahari kubwa ya kwamba Mheshimiwa Rais hakufanya makosa kuwapa nafasi alizowapatia. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninawashukuru watumishi wote katika Wizara. Ninajua kazi hizi zinafanywa na watu wengi. Niwape pongezi nyingi Makatibu Wakuu na viongozi wote walioko katika Wizara ya Nishati. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwape pongezi nyingine Waziri pamoja na Naibu Waziri na wafanyakazi wote wa Wizara hii. Niwatie moyo, wamepewa kazi katika kipindi kigumu, kipindi ambacho tunapita kwenye tatizo kubwa la mafuta duniani. Nami ninasisitiza, dunia siyo Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama msemaji aliyetangulia kusema, tatizo hili halijasababishwa na nchi yetu, limesababishwa na vita inayoendelea kati ya Marekani, Iran na Israel. Kwa hiyo, kazi yetu kubwa kama Wabunge, tutoke tuwaelimishe wananchi, tukawaeleze kwa nini sasa hivi bei zetu zinapanda?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza kwa juhudi ambazo kama viongozi waliodhaminiwa katika hii Wizara juhudi wanazozifanya kuhakikisha kuwa hata kama bei ya mafuta imepanda tumehakikishiwa na Mheshimiwa Waziri kuwa tuna mafuta ya kutosha ya kuendesha nchi yetu kwa miezi mitatu. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niwatie moyo. Mara nyingi wanasema mtoto aliyelelewa kwenye mazingira magumu ndiye anayekuja kuwa imara. Kwa hiyo, wameingia Wizarani katika wakati mgumu. Hili ni somo, haya ni mafunzo, na ni *skills* ambazo wanaenda kuzitumia katika siku zijazo, na watakuwa imara zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa pongezi zangu, mimi nitajikita kwenye masuala ya *REA* kutoka Mkoa wetu wa Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru pia Mheshimiwa Rais wetu kwa kuhakikisha kwamba mpango wetu wa *REA* unafanya kazi. Sisi wote ni mashahidi, kazi inaendelea, watu wako *site* na kazi inafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wetu wa Arusha tuna wilaya saba, tuna vitongoji ambavyo vilikuwa vinahitaji umeme 1,505. Hadi sasa *REA* imeweza kutuwekea umeme kwa asilimia 63 kwenye vitongoji 945. Kazi ambayo inaendelea ni vitongoji 128 ambayo ni asilimia nane, tumebakiza vitongoji 433.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilipata nafasi ya kutembelea maonyesho yanayoendelea, nikakutana na kiongozi mkuu wa *REA* ndugu yangu *Eng.* Hassan Saidy kama nitakumbuka jina lake vizuri. Alinihakikishia kwamba Serikali imejipanga kuhakikisha vitongoji vyote vilivyobaki vinaenda kukamilika ndani ya awamu nne. Kilichonifurahisha zaidi ni aliponiambia kwamba, kila kitongoji kitapewa nafasi ya kuamua chenyewe wapi kipeleke umeme? Hii itatusaidia kupeleka umeme mahali ambako kuna uhitaji zaidi. Akaja akanihakikishia kwamba *speed* ya safari hii itakuwa ya tofauti kwa sababu wamekuja na kitu kinaitwa *Framework Contract*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Framework Contract, REA* imekuja nayo ikiwa na madhumuni ya kuonyesha kwamba wakandarasi ambao watafanya kazi kwa haraka zaidi ndio hao watakaopewa kazi nyingine zaidi. Mkandarasi akimaliza, akipewa miradi kumi akimaliza, anapewa miradi mingine kumi. Hii itatusaidia kuwaengua wale ambao hawafanyi kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hili nilikuwa ninaomba nitoe ushauri. *Speed* hii iende na *quality, value for money* tuione. Isije ikawa tu mtu anakimbiza kazi ili baadaye apate kazi nyingine, lakini mwisho tunajikuta zile kazi hazina mashiko au tunarudia kuzifanya tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nilitaka kuliongelea, nina taarifa ambayo ni ya Machi, 2025, katika mkoa wetu tulikuwa na miradi ipatayo 1,082, lakini miradi iliyowekewa umeme ni 824, hivyo tumebakiza miradi 258. Nilijiuliza kidogo. Ninaamini kabisa *BOQ* tunazofanyia miradi yetu yote ina *contents* za kila kitu. Inakuwaje tunamaliza mradi ambao unakuwa baadhi ya vitu havijakamilika, kwa mfano umeme, ilhali ukiangalia maeneo hayo ni maeneo nyeti; kuna shule za msingi, sekondari, hospitali na zahanati?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali yangu Tukufu kwamba inapokabidhiwa hii miradi, wale wahusika wahakikishe *contents* zote ambazo ziko kwenye mradi, basi zinafanyiwa kazi. Ninaishauri Serikali kuhakikisha kwamba Wizara yetu ya Nishati

inapatiwa fedha za kutosha na fedha zitoke kwa wakati. Hizi fedha zitatuwezesha kwenda kufikia dira yetu ya 2050.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chiku Athman Issa, ahsante sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Arif Suleiman Premji atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima, na Mheshimiwa Jamila Mahmoud Juma ajiandae.

**MHE. ARIF S. PREMJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa. Nishati ya umeme inaenda na thamani na kuna kipimo chake cha thamani hiyo wanaita *kilowatt per hour,* yaani kilowati moja kwa saa. Hiki ndicho kipimo, na ndivyo unavyoweza kuijua *value* yake; na inaweza ikaku-*guide* ukajua kwamba uko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Rais pamoja na Wizara husika na Mawaziri wetu. Ninasema hizo pongezi kwa ajili ya *facts*. Leo hii Afrika Mashariki, Tanzania ndiyo nchi pekee ina gharama nafuu kwenye *kilowatt per hour*. Kipimo hicho ni sawa sawa uchukue pasi ya *kilowatts* 1,000 na uiendeshe kwa saa moja, ndipo utajua thamani. Sisi kwa wastani inatugharimu Dola za Kimarekani 0.09 hadi 0.1. Ukiangalia Kenya ni 0.26 *dollars kilowatt per hour* na ukiangalia Uganda ni 0.17 *dollars* kwa *kilowatt per hour*. Hicho ndicho kipimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ndiyo sababu kuu utaona wawekezaji wengi sana wanakimbilia Tanzania kwa gharama nafuu kwetu; na hiyo ndiyo inayosababisha hadi *TISEZA* kuweka rekodi ya *10 billion dollars* kwenye miradi ya uwekezaji. Kwa hiyo, hilo ni jambo la kujivunia sisi kama Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije hasa kwenye suala la Jimbo la Mtwara Vijijini na Mtwara yenyewe. Hii ndiyo sehemu ambako gesi inatoka. Kuna ujumbe wa watu wa Mtwara Vijijini wamenipa ambao ni lazima niufikishe kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, 2016 kuna mradi wa *power station* Kata ya Naumbu, Kijiji cha Namgogoli na Kisiwa; walifanyiwa tathmini, wakaja kulipwa tarehe 21 Disemba, 2023; na fedha waliyolipwa ilikuwa ni 13.8%. Mradi huo ni wa *power station*. Kwa hiyo, nimkumbushe hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, uchimbaji wa gesi unaoendelea Msimbati wakati *Rig* na mitambo inapita pale, imeacha madhara makubwa sana kwa kuharibu barabara. Kwa hiyo, huo ni ujumbe wa pili, wanasema kwamba wanaomba waboreshewe barabara ile ili irudi kwenye hali yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni Songo Songo, kijiji ambacho kinapewa umeme bila malipo, nacho kinapewa gesi. Kwa hiyo, ndugu zangu wa Msimbati wamenituma na hata wa Nanguruwe na Makata, kwamba gesi inachimbwa pale nao pia wanaomba wapewe umeme bila malipo kwa kuwa ndio sehemu mradi unapozunguka, na wao ndio walinzi wa kwanza wa eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vya *CNG* vinavyojengwa; kinajengwa Dar es Salaam, kinatarajia kujengwa Dodoma, sisi Mtwara Kusini tumeshahaulika kwenye kituo cha *CNG* ilhali sisi ndio wazalishaji. Ni sawasawa na kusema kwamba mpunga unalimwa Kyela, biriani linaliwa Dar es Salaam. Kwa hiyo, hili ninaomba nisisitize sana, tunahitaji kituo cha *CNG* Kusini Mkoa wa Mtwara, Jimbo la Mtwara Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia gesi, Serikali yetu imeweka *incentives,* imetoa misamaha. Leo hii ukiagiza gari ambalo linatumia *CNG*, linatumia gesi asilia hakuna *VAT*. Bunge la Kumi na Mbili, kama sikosei, kulikuwa na mpango wa kuweka shilingi 384 kwenye kila kilo ya *CNG*. Baadhi ya Wabunge wakakataa, na Serikali ikaondoa tozo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vivyo hivyo gesi inabidi ilete tija kwa wananchi. Mwekezaji yeyote anapopewa gesi, basi tuangalie je, inaleta tija gani kwenye maisha ya mwanachi wa kawaida? Ninasema hivyo kwa uhalisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatoa *incentives* nyingi sana. Kwa mfano, leo hii tuna kiwanda cha saruji, kuna *incentive* wanapewa pia Kusini. Mfuko mmoja wa saruji Dar es Salaam ambako ndiko kituo cha biashara, ni shilingi 17,531; na njia ya usafirishaji kutoka Mtwara tani 30 mpaka Dar es Salaam, sasa hivi vyombo vinavyotumika ni vya *CNG*. Gharama za kusafirisha ukitumia dizeli tani 30, gari hilo ni takribani shilingi 80,000, lakini ukitumia gari ambalo lina *CNG* kwa kila tani inakuwa ni shilingi 41,000. Maana yake nini? Ana-*save* shilingi 2,050 kwa kila mfuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei iliyokuwa Dar es Salaam shilingi 17,531, na ukizingatia unasafirisha kwa kutumia chombo cha usafiri kinachotumia gesi ambayo gharama yake ni nafuu, ni hali iliyo wazi kabisa kwamba, bei ya saruji ambayo inabidi itozwe Mtwara inabidi iwe pungufu ya bei ya Dar es Salaam kwa shilingi 2,050. Hiyo ndiyo tija tunayoitaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri kwamba, tunapowapa wawekezaji gesi, basi tuangalie, wapo wengine wanachukua ndiyo njia ya kuongeza *margins* zao. Huo ndiyo ulikuwa ujumbe wa Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye jambo lingine. Tunachanganyikiwa na vitu hivi vitatu; Wizara ya Viwanda, Wizara ya Nishati, na Wizara ya Uwekezaji. Kwa kuwa leo hii tunapozungumzia gesi, hatutajua hasa kipaumbele chetu kwenye gesi. Je, tunataka kwa ajili ya kuzalisha umeme? Au je, tunataka kutumia kama malighafi? Ni lazima tuchague. Kama ni malighafi kwa ajili ya viwanda vya mbolea au *petrol chemical,* basi iende huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni *CNG* na kuzalisha umeme, basi tujue. Hatimaye patakuwa na mivutano kati ya Wizara hizo. Wawekezaji watataka gesi, Wizara ya Nishati ili kutimiza lengo la *megawatt 30,* 2050 atakuwa anavutia kwake; na hatimaye wote tutachanganyikiwa. Kwa hiyo, lazima tuweke vipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tumejaliwa pia kuwa na *uranium* kwenye *Mkuju River Project;* na kuna kampuni inaitwa

*Rosatom* ya Urusi. Tani moja ya *uranium* unaweza ukazalisha *kilowatt hour* milioni 45 kwa kuweka kinu cha nyuklia. Katika Bara la Afrika, *South Africa* ndiyo pekee ina kinu cha nyuklia. Tunashindwa nini sisi kufanya tukawa wa pili kwenye Bara la Afrika kama nchi? Kwa kuwa leo hii tunasafirisha malighafi kupeleka huko, kwa hiyo, ni vyema sasa tufikirie, *it is high time* sisi kama nchi, tuangalie kuwekeza kwenye *atomic energy;* na hapo tunasema wanaita *small modular reactors*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajili ya muda, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima atafuatiwa na Mheshimiwa Jamila Mahmoud Juma, Mheshimiwa Mohamed Mussa Utaly, ajiandae.

**MHE. DKT. REGINA C. MALIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Nishati. Nitaenda moja kwa moja kwenye hoja zangu, lakini kipekee kabisa nichukue fursa hii kuipongeza Wizara hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika kuandaa bajeti hii yenye mwelekeo mzuri na kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilipata amani sana wakati Mheshimiwa Waziri akifanya wasilisho lake kwa kuona namna ambavyo Wizara hii imejipanga kimkikati kuhakikisha kabisa kuwa inasaidia wananchi. Takwimu walizozitoa inaonyesha kabisa upande wa uwiano wa matumizi, miradi ya maendeleo ni zaidi 97%, lakini upande wa matumizi ya kawaida ni asilimia mbili nukta tano. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri, na ninafikiri Wizara nyingine inabidi tuje tujifunze kwenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nimepata amani na nimelala usingizi mzuri nikasema kumbe kuna Wizara ambazo zinaweza zikajikita katika kuhakikisha zinatetea maslahi ya wananchi wa Tanzania! Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipaumbele cha Wizara hii kimejidhihirisha wazi, kipaumbele chao ni kuwatumikia

Watanzania, na Taifa haliwezi kukua bila kuwekeza katika miradi ya kimkakati. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri na timu yake hongera sana kwa kazi kubwa ambayo wameifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, mimi nimeenda mbali, nimefanya *analysis* kwenye upande wa fedha ambazo mnatumia katika kuhudumia hii Wizara. Fedha za ndani ni 65.1% lakini fedha ambazo Wizara hii itategemea kutoka nje ni 34.9%. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa sababu gani nawapa hongera? Kwa sababu nchi haiwezi kutegemea fedha za nje katika kuendeleza miradi ya kimkakati. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri amefanya jambo kubwa sana la heshima kwa nchi kuhakikisha kabisa bajeti yao ambayo inahudumia wananchi pia inatumia kwa kiwango kikubwa fedha zinazotoka ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hasara kubwa kutegemea fedha kutoka nje. Hasara hizo zinaweza zikawa ni kutokuwa na uhuru *(decision making)* ya kufanya mambo yetu wenyewe. Pia, tukitegemea fedha kutoka nje tunaweza pia tusitimize vipaumbele vyetu kwa sababu fedha kutoka nje mara nyingi zinakuja na masharti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme tu kwamba kazi ya Mheshimiwa Waziri ni nzuri kwa sababu fedha za ndani zinasaidia pia kupunguza madeni ya Taifa na kuhakikisha nchi inaenda vizuri. Kwa hiyo, hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongee kitu kingine. Mimi ni Mbunge mwakilishi wa kundi la vyuo vikuu. Nchi yetu ina changamoto ya ajira, na ajira imekuwa ni tatizo kubwa kwa sababu kila Mbunge anayesimama, hoja kubwa ni ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoongea *issue* ya ajira, vijana wetu wengi wako mtaani. Kwa hiyo, kuna kitu ambacho nimekiona katika wasilisho la Mheshimiwa Waziri. Taarifa ni nzuri, lakini inaelezea habari ya ongezeko la ajira kwamba ajira katika Wizara yake zimeongezeka kutoka watu 225 hadi 35.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi hii ni ndogo sana na ninaomba leo nitoe ushauri ambao kama atapenda basi atauchukua. Serikali imewekeza kwa kiwango kikubwa katika Wizara hii. Taarifa ya Mheshimiwa Waziri imesheheni miradi mikubwa ya kimkakati, lakini sasa tukiangalia idadi ya ajira katika Wizara hii au katika miradi iliyoko kwenye Wizara hii ni chache sana. Hatuwezi kuongeza watu 335 tu ndio wamepata ajira katika miradi ya kimkakati ambayo iko katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe, kwa sababu nia ya Serikali ni njema, na kwa sababu imejikita kabisa kutetea wananchi, lazima Wizara ije na mikakati ambayo itakuwa *sustainable* kwa ajili ya kuhakikisha Wizara pia inakuwa na sehemu ya kutoa ajira kwa vijana wetu. Ongezeko kubwa la ajira nchini tunategemea litoke kwenye kila Wizara. Kila Wizara itenge sehemu ya ajira kwa ajili ya vijana wetu ili vijana wetu waweze kupata ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina wazo zuri kwa ajili ya hii Wizara, na kama watahitaji pia nitawapa *input* zangu kuhakikisha hiki kinaenda kutendeka. Kitu cha kwanza, ninaomba Wizara ya Nishati iwe na mfumo rasmi wa ushirikiano kati yao na vyuo na vyuo vikuu. Ushirikiano huu utasaidia kuibua ajira katika sekta ya mafuta na gesi na miradi mingine ya kimkakati iliyoko katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itasaidia vijana wetu waweze kupata ajira. Hii haiondoi ile *Ajira Portal* iliyoko katika mifumo yetu ya ajira, hapana. Mfumo huu rasmi wa ushirikiano wa vyuo vikuu utasaidia kuhakikisha vijana wanaohitimu vyuo na vyuo vikuu wanapata ajira na inaweza ikawa tunaweza tukaita ni *industry academia linkage*. Mashirikiano yawepo kati ya Wizara na vyuo na vyuo vikuu pamoja na vyuo vile vya *VETA*, basi vijana wetu waweze kupata ajira katika miradi hii ya kimkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninapendekeza, Wizara ianzishe mfuko maalum wa ujuzi wa sekta ya Nishati utakaowezesha vijana kupata mafunzo ya utaalamu unaohitajika sokoni. Hii imekuwa ni changamoto kubwa sana. Vijana wetu wengi hawana ujuzi, na hili ni jambo la Kitaifa ambalo linatakiwa

liangaliwe kwa sababu tunapoona vijana wetu hawana ajira, ni lazima tujiulize, kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna sehemu mambo hayaendi vizuri. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, aache *legacy* kwenye nchi. Amepewa Wizara hii, atengeneze kitu ambacho hata ukiondoka leo, tutasema ya kwamba Mheshimiwa Deogratius Ndejembi kuna kitu alikifanya pamoja na msaidizi wake Mheshimiwa Salome, na timu ya watumishi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine cha tatu ninapendekeza, Wizara iweke masharti kwa kila miradi mikubwa ya kimkakati iliyoko chini ya Wizara, iwe na kipengele cha mafunzo na ajira kama sehemu ya kuwasaidia hawa vijana na hata mikataba ile wanayosaini, wahakikishe kuna hicho kipengele kidogo ya kwamba miradi hii ya kimkakati basi itakuwa inahakikisha Watanzania wanapata ajira katika miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo yalikuwa ni upande wa changamoto ya ajira, lakini pia kuwakilisha nafasi ya vyuo na vyuo vikuu katika ajira kwenye hii miradi ya kimkakati ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho niongee tu kwa niaba ya wananchi wa Tanzania, Wizara imekuwa ikifanya kazi njema sana na nzuri, lakini bado kuna mambo madogo madogo tu ambayo yamekuwa hayaendi. Wizara iongeze magari katika vitengo vya *emergency* ili kuwahudumia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kumekuwa na changamoto ya hapa na pale ya kukatika kwa umeme, lakini pindi kunapokuwa na vitendea kazi kama hivi kukosekana, basi huduma zinakuwa hafifu kwa wateja wao au kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Regina Malima. Mheshimiwa Jamila Mahmoud Juma, atafuatiwa na Mheshimiwa

Mohamed Mussa Utaly, Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, ajiandae.

**MHE. JAMILA MAHMOUD JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia hii fursa na mimi ya kuwa mmojawapo kati ya wachangiaji katika Wizara hii ya Nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha siku ya leo kuweza kusimama hapa na kuchangia Wizara hii. Nami niungane na wenzangu katika kutoa pongezi zangu kwa Mheshimiwa Rais wetu kipenzi, Mama Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake mbalimbali ambazo anazifanya kuhakikisha kwamba Watanzania wanakuwa na maisha mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake iliyojaa maono, hotuba ambayo imebeba matumaini kwa Watanzania. Kusema kweli sekta ya nishati ni sekta muhimu sana katika kuleta maendeleo ya nchi yetu. Ni sekta ambayo inabeba nafasi kubwa sana katika jamii yetu kwa sababu bila ya umeme, bila ya mafuta, bila ya gesi, basi maisha hayaendi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hii kusema kweli imeleta mafanikio makubwa kwa kuhakikisha kwamba gridi ya Taifa inasababisha au inaleta upatikanaji wa Nishati ya uhakika katika jamii yetu au katika Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo ambayo yapo au yamepatikana katika masuala ya nishati, mchango wangu zaidi nitauangazia kwa upande wa Zanzibar ambapo kwa muda mrefu sasa Zanzibar imekuwa tunategemea nishati hii kutoka Tanzania Bara na Nishati ambayo imekuwa ikitumia mifumo ya baharini ambayo tunaita *Submarine cable* kitu ambacho kwa muda mrefu sasa imekuwa kinasababisha au kinaleta usumbufu kwa namna moja au nyingine kutokana na tatizo la kuharibika kwa miundombinu ya mara kwa mara, na pia kusababisha kukosekana kwa umeme kwa baadhi ya sehemu kwa upande wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na utegemezi huo ambao Zanzibar tumekuwa tukitegemea umeme huu kutoka Tanzania Bara, kumekuwa na changamoto nyingi za kukosekana kwa umeme, kunakosababisha ukosekanaji wa huduma muhimu katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, tukiangazia katika sekta ya afya ambayo tunategemea umeme kwa kiasi kikubwa; kuna sekta ya elimu nayo pia kwa maeneo ambayo yanahitajika umeme huwa yanakosekana; na kwa wafanyabiashara huwa wanapata hasara kwa sababu ya kukatika umeme mara kwa mara. Pia kuna watu ambao wanatumia viwanda. Tuna viwanda vidogo vidogo na vikubwa kiasi, lakini pia navyo hupata hasara katika ukosefu wa mahitaji hayo ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii imefanya kwamba tujiulize je, kama Zanzibar iko salama katika suala zima la nishati? Hiki kitendo cha kukosekana nishati mara kwa mara kunaipelekea Zanzibar kutokuwa salama kwa sababu Zanzibar ni nchi ambayo tunaelewa kwamba uchumi wake mkubwa unategemea utalii. Kama inategemea utalii, ina maana wageni wanapokuja wanategemea wapate huduma ya umeme ya uhakika, lakini wale watoa huduma katika mahoteli na *service* nyingine za kitalii wanahitaji kuwa na umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaweza kutoa pendekezo kama wenzangu walivyotangulia kwamba kuna njia nyingi ambazo zinaweza kusababisha tukawa na umeme wa uhakika au upatikanaji wa nishati ya uhakika. Kuna masuala mazima ya utumiaji wa *solar*. Tumeona kuna masuala mazima ya kutumia gesi na pia kuna nishati ya umeme wa upepo. Ni kitu ambacho pia kinaweza kusaidia kuleta mabadiliko au kuhakikisha kwamba tuko katika nishati salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninaweza kutoa pendekezo katika suala zima la utumiaji wa nishati, kwa sababu hili linapunguza nguvu ya kiuchumi, lakini siyo uchumi tu, lakini hata usalama wa nchi nao unakuwa unatetereka kwa sababu ile miundombinu ya kudhibiti usalama wa nchi inakuwa inatetereka kutokana na ukosekanaji wa hiyo nishati ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Wizara ni kwamba wakati umefika, kwa sababu Zanzibar imekuwa inategemea umeme kutoka Tanzania Bara, ni wakati sasa wa Wizara ya Nishati kukaa na Wizara ya Nishati ya Zanzibar kuona namna gani sasa wanaweza kwa pamoja kuja na miundombinu ya uhakika ya kuhakikisha umeme wa Zanzibar haukatiki hovyo, lakini pia wananchi wa Zanzibar wanafaidika na hii nishati ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Wizara ije na mawazo au miundombinu mbadala katika kuhakikisha kwamba umeme unapatikana kwa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kusema kwamba ninaunga hoja mkono, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jamila Mohmoud Juma kwa mchango wako. Mheshimiwa Mohamed Mussa Utaly atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila, ajiandae.

**MHE. MOHAMED M. UTALY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ninaomba nishukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia katika Wizara ya Nishati, lakini ninaomba nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuipaisha Tanzania katika sekta ya umeme. Sasa hivi umeme umeshapita, umeshafika katika vijiji vyote, na sasa tunaelekea katika kukamilisha vitongoji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anastahili pongezi kubwa sana katika jambo hili. Pia, ninapenda niwapongeze kwanza Waziri wa Nishati, ndugu yangu Mheshimiwa Deogratius Ndejembi pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Salome Makamba kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaiangalia sifa pekee waliyokuwanayo, sifa ya kuwa wasikivu na unapowapa jambo, wanafuatilia na kukupa mrejesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo ni kubwa sana, na sisi Wabunge tunafurahishwa sana na jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, niseme tu kwamba nimesoma Randama pamoja na Hotuba ya Bajeti. Katika ukurasa wa 84 wa Randama na katika ukurasa wa 88 wa hotuba, linazungumziwa suala la majadiliano ya *LNG,* (mradi wa kusindika gesi asilia kuwa katika hali ya kimiminika) kwamba mjadala unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu mjadala wake umechukua muda mrefu sana na hata tunavyohisi sasa hivi katika mjadala, ni kana kwamba mjadala huu hautaisha kwa sababu hatujiandai kwamba mjadala ukiisha tumejiandaa vipi na mradi wa *LNG?*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nikitoa mfano, wakati ule tulikuwa na suala la gesi kutoka Mtwara, yapo mambo tulikuwa tunaona yanaanza kufanyika. Kwa mfano, sasa hivi hatujajiandaa na suala la uwekezaji kwa sababu ipo miundombinu muhimu ambayo inahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu hii ikiimarishwa itatusaidia kwenda vizuri na mradi wa *LNG*. Tuna suala la barabara. Hili suala ninajua halihusiki na Wizara hii, lakini tunalo suala la nishati ya umeme. Lindi umeme wetu siyo wa uhakika. Umeme unazimika mara kwa mara na ndiyo maana tunaomba, na tumeshakuwa tukiomba tangu siku za nyuma, Mkoa wa Lindi na Mtwara uunganishwe katika gridi ya Taifa ili tuwe na umeme wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kukosa umeme wa uhakika katika Mikoa ya Mtwara na Lindi kunasababisha matatizo mengi ya kiuchumi katika mikoa yetu. Tunafikia mahali tunakosa wawekezaji wakubwa. Hata huo umeme tunaoupata, una *fluctuation,* mara unakuwa umeme mkubwa mara unakuwa umeme mdogo unasababisha uharibifu wa miundombinu katika huduma nyingine za jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshapata uharibifu katika mitambo ya kusambaza maji pale Ng'apa mara kadhaa kutokana na *fluctuation* ya umeme. Kwa hiyo, ninamwomba sana

Mheshimiwa Waziri atuangalie Mikoa ya Lindi na Mtwara ili na sisi tupate umeme wa uhakika tuweze kupata wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ninasema, kuna tatizo la maandalizi ya rasilimali watu. Nami nilijaribu kuomba katika vyuo vyetu vya *VETA*, mitaala *(syllabus)* ambayo inafanyika pale, hakuna hata chuo kimoja cha *VETA* kinachozungumzia masuala ya ufundi wa gesi na mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana ninasema tunajadiliana kana kwamba hatujiandai. Sasa hivi ingetakiwa vyuo vyetu vya *VETA* viwe vinatoa taaluma hiyo, angalau tuwe na vijana ambao wana ufundi watakaoweza kuingia katika mradi huu, lakini kwa hali ilivyo sasa hivi, tutashtukizwa tu tukishakubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, tuliahidiwa kujengewa Chuo cha Ufundi wa Mafuta na Gesi pale Lindi, Chuo cha Arusha *Technical* kwamba kitajengwa pale ili kutoa mafunzo hayo. Pamewekwa bango pale, "*Arusha Technical Coming Soon,*" lakini inafikia mahali mpaka wanafunzi wetu hawalielewi neno "*coming soon*" kwa kuwa ni *coming soon,* lakini bango hilo limewekwa sasa yapata miaka mitano na bado chuo hicho hakijajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningemwomba Mheshimiwa Waziri, kwa sababu chuo hiki kinahusiana na Wizara yake uweze kushauriana na Wizara ya Elimu ili tuweze kupata hiki chuo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni ushirikishwaji wa wananchi. Wakati gesi ya Mtwara ipo katika shamrashamra zake, wote tunazijua humu ndani, wananchi walishirikishwa. Yalichukuliwa makundi ya wananchi kupelekwa katika maeneo mbalimbali kwenda kujifunza juu ya masuala ya gesi, kwenda kujifunza faida watakazozipata kuhusiana na gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nimwulize Mheshimiwa Waziri, kuna dhambi gani ukiamua kuwachukua Madiwani, ukawachukua viongozi wa dini, ukawachukua na watu wengine wakaenda kujifunza jambo hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana inafika mahali wakati mwingine watu wanajitengenezea tu taratibu za kutoa mafunzo ambayo hata Wizara haikuwatuma. Kwa hiyo, ni vizuri tusitoe *vacuum*, Wizara iingie kati iweze kutoa mafunzo kwa wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa nilizungumzie ni suala la fidia. Ipo laini ya umeme ambayo imepita kutoka Mtwara kwenda mpaka Somanga. Laini hii imepita katika kata ya Mnazi Mmoja iliyopo katika jimbo langu, Mtaa wa Ruaha, uthamini umefanyika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri watu hawa walipwe fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, imefika mahali ukienda kuwatembelea hawana ajenda nyingine zaidi ya fidia, na hata ukisikiliza mambo mengine hawayasikii. Ninaomba, jambo hili, nimezungumza na dada yangu Mheshimiwa Salome, ameahidi kwamba litafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuahidi ni mbali na kutekeleza ni mbali, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri kwa kushirikiana na Naibu Waziri jambo hili litekelezwe, wananchi hawa wapewe fidia kwa sababu maeneo yao yamechukuliwa, hawafanyi shughuli za uzalishaji katika maeneo yale. Basi walipwe fidia ili fedha hizi waweze kuzizungusha katika biashara zao wapate tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningeomba nichangie kwa wakati huu ni suala la usambazaji wa gesi majumbani. Kasi yetu ya usambazaji wa gesi majumbani kwa maana ya upelekaji wa moja kwa moja katika nyumba ya mtumiaji, imekuwa ndogo sana. Katika jimbo la Lindi, ni Kata ya Mnazi Mmoja pekee ndiyo ambayo ina gesi majumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, usambazaji huu wa gesi majumbani una faida kubwa. Mwananchi anapoamua kupika chakula, maana yake anaenda kujinunulia kiasi cha gesi kwa kiasi cha matumizi yake tu. Kwa hiyo, ninaomba sana usambazaji wa gesi uende kwa kasi kubwa na ufike katika maeneo mengi. Wananchi wengi sasa hivi wanahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafahamu katika siku za kwanza kulikuwa na wasiwasi kwa wananchi kuwapelekea gesi majumbani moja kwa moja, lakini sasa wameelimishwa na wameelimika, wanahitaji hilo jambo lifanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo ningependa nichangie kwa siku ya leo ni kuhusiana na maeneo ambayo yapo Manispaa, lakini kwa silka na mienendo yake yana hadhi ya vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunaunda Manispaa ya Lindi, tulichukua vijiji vilivyoko Lindi Vijijini tukaleta Manispaa ya Lindi. Watu hawa kuwaambia kwamba walipe shilingi 320,000 kuunganishiwa umeme hawatuelewi hata kidogo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. MOHAMED M. UTALY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba dakika moja nimalize.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Mheshimiwa Waziri hili alichukue na walifanyie kazi ili watu hawa nao waweze kulipa shilingi 27,000 wapate umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni walioko Bungeni asubuhi hii. Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Kwanza ni wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Johannes Lembulung' Lukumay, Mbunge, ambao ni wapiga kura wake kutoka Arumeru Magharibi, Mkoani Arusha. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao wanafunzi 51 wa Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao "Jukwaa Huru la Wazalendo" kutoka mikoa mbalimbali Tanzania, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, atafuatiwa na Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila, Mheshimiwa Dkt. Wilson Charles Mahera ajiandae.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi nami niungane na wenzangu kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya hususan kwenye sekta hii ya nishati. Maelekezo yake, miongozo yake na matokeo yake tunayaona. Mradi mkubwa wa *REA* ambao kwa Afrika sasa tunaongoza umetekelezwa na unaendelea kutekelezwa kwa ufanisi mkubwa sana. Kwa hiyo, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua nafasi hii kumpongeza kijana machachari ambaye bado ana nguvu, ndugu yangu Mheshimiwa Ndejembi, kwa kazi nzuri ambayo anaifanya. Pia ana msaidizi wake makini sana, Mheshimiwa Salome Makamba. Ni mtu mahiri ambaye anaifahamu vizuri Sekta hii ya Nishati, atamsaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua nafasi hii kuwapongeza Makatibu Wakuu wote wawili, ndugu yangu Mramba na ndugu yangu Matarajio kwa kazi nzuri ambazo wanaendelea kuzifanya, na watendaji waliopo chini yao bila kuwasahau Ma-*CEO*, watendaji wakuu wa makampuni yaliyopo chini ya Wizara hii, kwa maana ya *TANESCO*, *TPDC*, *REA* na *PURA* kwa kazi nzuri ambazo wanaendelea kuzifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utajikita kwenye maeneo matatu; upatikanaji wa umeme, shirika letu la *TPDC* na mradi wa *LNG*. Kama nilivyosema kwamba mzungumzaji aliyepita ametoa sifa kubwa sana ya Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwamba ni wasikivu, lakini mimi ninasema wana sifa ya pili, kwamba hawajatumika sana, kwa hiyo, wana nguvu ya kukimbia

kimbia kwa unyeti wa sekta hii. Kwa hiyo, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni ishara ya usikivu kwa changamoto ya umeme ambayo tulikuwa nayo Mtwara na Lindi. Tulifanya kikao maalum na Mheshimiwa Waziri na tukampa malalamiko yetu na yeye kwa uzito ule, alipeleka kwa Mheshimiwa Rais kwa sababu tuna mkandarasi ambaye anajenga laini ya umeme kuunganisha mikoa ya kusini na gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya wiki mbili tumeambiwa mkandarasi yule amelipwa shilingi bilioni 33 na yupo *site*. Tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa usikivu wake na tumefuatilia mkandarasi yupo *site* ili kuhakikisha Mtwara na Lindi inaungwa kwenye gridi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hata maneno ambayo tulitaka kuchangia Wabunge wa Mtwara na Lindi tumeyashusha kidogo kwa sababu ya hicho alichokifanya. Ninamwomba aendelee kufuatilia, kumsimamia mkandarasi na tunataka matokeo. Sisi Mtwara na Lindi tuna changamoto ya umeme na tulimwambia siku ile kwamba suluhisho kubwa ni hii ya kuiunga Mtwara na Lindi kwenye gridi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suluhisho lingine ni mradi wetu wa megawati 300 ule wa Naumbu ambao ameelezea vizuri kwenye kitabu chake kwamba majadiliano yanaendelea, kwa sababu mradi ule wanashirikiana na *JICA*, na kwamba fidia imetolewa na sasa hivi wanaendelea na hatua zinazofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana huo mradi utekelezwe kwa sababu utakuwa mwarobaini wa Mikoa ya Mtwara na Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimkumbushe Mheshimiwa Waziri, vile vile suluhisho lingine, laini yetu ya kutoka Mtwara – Nanyamba – Tandahimba – Newala ina changamoto kubwa na Wizara iliamua kuanza mradi wa kutoa nguzo za zamani na kuweka nguzo za zege, ule mradi umesimama.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, ule mradi uendelee ili kuhakikisha kwamba Nanyamba, Tandahimba na Newala tunakuwa na laini imara na ambayo miundombinu yake haileti usumbufu mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Waziri, akikamilisha hili la kuunga Mtwara na Lindi kwenye gridi ya Taifa utakuwa umeandika historia kubwa na tutakuandika kwenye historia ya Mikoa ya Mtwara na Lindi kwamba mradi mkubwa ambao ulikuwa unasuasua, Mheshimiwa Ndejembi na Mheshimiwa Salome Makamba wakati wameshikilia ile Wizara wameukamilisha mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwomba Waziri atumie nguvu zake zote, uwezo wake wote na umahiri wake wote akamilishe mradi huu; na uwezo huo tunawaamini wanao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya pili kama nilivyosema ni shirika letu la *TPDC* chini ya Mkurugenzi Mussa Makame na wasaidizi wake, ni miongoni mwa mashirika yanayofanya vizuri sana kwenye nchi yetu na ni miongoni mwa mashirika ambayo yametuthibitishia kwamba wapo Watanzania wazalendo ambao tunaweza tukawapa miradi mikubwa wakaisimamia kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mawaziri hawa wanasimamia vizuri Sekta ya Nishati na miradi yote iliyopo kwenye shirika hili. Tuwape nguvu kwa kuwaongezea fedha ili wakamilishe maono yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya kazi zao nzuri ambazo wanazifanya hapa, ninawashauri mambo mawili tu. Kama alivyosema msemaji aliyepita kuhusu mradi wa usambazaji wa gesi majumbani, hebu waongeze kasi. Wale wateja ambao wamepewa sasa hivi ni wachache sana, na hata bajeti iliyopita nilisema, siyo vibaya wakajenga laini kutoka Mtwara – Nanyamba – Tandahimba – Newala – Masasi ili na wale waliopo ndani ya Mkoa wa Mtwara wanufaike na mradi huu wa usambazaji wa umeme majumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni kwamba wawekezaji wanapotaka kupewa huduma ya gesi asilia, basi wahudumiwe haraka sana. Kuna kampuni sasa hivi zimekuja Mtwara, kuna mwekezaji wa kiwanda cha mbolea, apewe mapema ili aweze kutumia nishati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Mtwara tuna kongani ya viwanda vya korosho pale Maranje na kutoka Maranje hadi ulipo mkuza wa bomba la gesi asilia ni kama kilomita 30 tu. Hebu tupeleke pale hiyo gesi asilia ili wawekezaji ambao wanakuja pale Maranje wakutane na huduma kama hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa tatu unahusu mradi wa *LNG*. Ninaipongeza Serikali kwa taarifa ambayo wametuletea sasa hivi kwamba wapo katika hatua za mwisho za ukamilishaji mazungumzo na wawekezaji, na imebaki maeneo ya kisheria tu, hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Waziri na nimesema kwamba Waziri ana mtu ambaye anaifahamu nishati. Mradi huu Naibu Waziri anaufahamu vizuri sana na ninaomba amtumie sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokaribia kwenda mwishoni mwa kuhitimisha mradi huu waanze kutumika, hebu twende kwenye kazi ya kuiandaa jamii. Kule nyuma tulikuwa na Kamati mbili ambazo zilianzishwa wakati mradi unaanza, ule wa utwaaji wa ardhi na ule wa uhamasishaji wa jamii. Twendeni tukaielimishe jamii *LNG* ni nini? Manufaa yake ni nini? Ni wakati gani wananchi watanufaika na mradi huu? Tuka-c*ontrol expectation* za watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtwara iliharibika kwa yale yaliyotokea kwa sababu tulipeleka matumaini ambayo Serikali tusingeweza kuyafikia. Unaambiwa Mtwara itakuwa ni Singapore, itakuwa ni wapi, hebu twendeni tukawaambie vizuri wananchi wa kusini *LNG* ni hatua gani wao watanufaika?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uelewa wangu mdogo, jamii ya Mtwara na Lindi itanufaika sana na mradi huu wakati wa ujenzi

wa mradi. Baada ya kukamilika kwa ujenzi wa mradi utabaki na watendaji wachache sana. Sasa kipindi hiki hiki cha ujenzi wa mradi tuwaandae watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mzungumzaji aliyepita amesema, huko nyuma, tuliandaa programu za mafunzo kwa vijana wetu wa Mtwara na Lindi. *VETA* Mtwara na *VETA* Lindi kulikuwa na kozi mbalimbali. Muda huu sasa tukarejeshe yale mafunzo ili vijana wetu wa Mtwara na Lindi wakati mradi utakapoanza wapate ajira ndogo ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatutarajii tushtukize tena kama tulivyofanya wakati ule. Kwa hiyo, ninaishauri Wizara kwamba muda wa ku-*engage community* ni kipindi hiki hapa. Tuwaeleze vizuri, watanufaika na nini, na Wizara ziongee.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Lindi na Mtwara kuna miradi mingi ya umwagiliaji. Ni muda wa kuanza sasa hivi, wakati watu wengi watakapokuwepo pale Lindi wakati wa ujenzi wa mradi, basi miradi ya umwagiliaji ya kule Namupa, Ndanda, Newala na Tandahimba wapeleke huduma kwa watu watakaokusanyika pale wakati wa ujenzi wa mradi huo wa *LNG*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake, wasife moyo, waendelee kuchapa kazi na sisi tupo nyuma yao na tunatarajia mambo mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Wilson Charles Mahera. Mheshimiwa *Eng*. Kija Limbu Ntemi ajiandae.

**MHE. MABULA J. MAGANGILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwanza kabisa ninaomba niipongeze Wizara kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya ya kupeleka nishati katika nchi yetu. Kipekee kabisa, katika Jimbo la Msalala kwa mradi wa vitongoji waliotuletea katika vitongoji 392, tunakwenda kufikia vitongoji 254. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, isitoshe tu kwamba, kwa sababu ya kusogeza huduma na kuwahudumia wananchi kwa haraka zaidi, tunashukuru tumepokea magari mawili mapya, lori moja na gari ndogo. Ahsanteni sana, na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Msalala tunawashukuru sana na tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru zaidi Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwani alivyotembelea katika Wilaya ya Kahama tulimwomba atupelekee umeme wa uhakika kwa wachimbaji wadogo wadogo ambapo kwa kweli tunatumia gharama kubwa sana kuzalisha dhahabu kwa kutumia mafuta. Kwa maana sehemu ambayo tulitakiwa tufunge *winch* ya umeme tunafunga injini ya pikipiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaiomba Wizara kwa mradi huu unaoendelea, tuendelee kuharakisha kufikisha huduma kwa wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada nzuri sana ambazo zimefanywa na Wizara ya Nishati kutuhakikishia upatikanaji wa mafuta nchini. Nami ninaongeza ushauri wangu kwamba sasa zoezi hilo la upatikanaji, tumeshaliweza kwa kiwango kikubwa na kwa jitihada za Wizara. Tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, yapo mambo ambayo yapo ndani ya uwezo wetu kama Taifa. Suala la usafirishaji, ninaomba Wizara ya Nishati pamoja na Wizara ya Uchukuzi, tunalo shirika letu la reli ambalo kwa kiasi kikubwa miundombinu ya reli ipo na pia matenki ya kutunza mafuta yaliyounganishwa na miundombinu ya reli tayari yapo, sehemu ya kupakia baharini tayari matanki yapo na miundombinu ipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifika pale kwetu Isaka Bandari Kavu tayari matanki ya kutunza mafuta yapo na yana *siding rail* tayari. Ambapo kwa kiasi kikubwa tukitumia miundombinu ya reli kusafirisha mafuta, yataenda kupunguza bei ya mafuta kwa kiasi

kikubwa hasa katika Kanda ya Ziwa. Kwa maana gani? Pia tutasaidia mafuta yanayoweza kwenda nchi za jirani, badala la malori kwenda Dar es Salaam yakaishia Isaka, malori ya kutoka Rwanda, ya kutoka Burundi, pia, tukalipatia mzigo wa kutosha Shirika letu la Reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, kaka yangu Deo, Mheshimiwa Waziri, ametoka sekta binafsi. Tunazo kampuni ndogondogo za ujenzi katika Shirika letu la *TANESCO*. Ninaomba, badala ya kampuni hizi kufanya kazi za ujenzi wa miundombinu yetu hapa nchini, tuziwezeshe kutoka nje zikachukue tenda kwenye nchi za nje. Kama ambavyo mashirika mengine ya mataifa makubwa yanakuja kuchukua tenda nchini kwetu na baada ya hapo yana *subcontract* kampuni zao za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika letu la *TANESCO* liende likachukue kazi nje ili tuweze kufanya *labor export* kubwa kwa Watanzania na kampuni zetu ndogondogo za Kitanzania na kuweza kuingiza mapato na fedha za kigeni katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya wananchi wa Msalala, ninaridhika na Wizara hii ya Nishati kwa kiwango hiki ambacho wameweza kuji-*commit* kwa 97% kupeleka pesa kwenye miradi ya maendeleo. Ninaamini mapendekezo haya ya mageuzi makubwa ambayo tumeyatoa Waheshimiwa Wabunge, watakwenda kuyafanyia kazi kwa kiwango cha 97% pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Wilson Charles Mahera, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Kija Limbu Ntemi, Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga ajiandae.

**MHE. DKT. WILSON C. MAHERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Sasa ninaomba kuchukua nafasi hii kuchangia katika Wizara hii ya Nishati. Kwanza kabisa kabla sijasahau, ninasema ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaanza na pongezi, kwanza kabisa ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwekeza kwa kiasi kikubwa katika nishati hii ya umeme na kufanya mageuzi makubwa sana kwa kuhakikisha kwamba vijiji vyetu vyote 12,300 na kitu vina umeme, hiyo inastahili pongezi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mnavyojua kwa sasa tunakwenda kutekeleza Dira hii ya Mwaka 2050 na tuko kwenye Mpango wa Nne ambao ndiyo wa kwanza kabisa wa kwenda kutekeleza hiyo Dira ambayo dhima yake inasema: "*Mageuzi kwa ajili ya ukuaji wa uchumi jumuishi na kuzalisha ajira.*" Hasa nishati hii ya umeme ni nguzo muhimu sana katika uchumi wa viwanda. Kwa hiyo, ninadhani katika miaka hii minne ambayo tumebakiwa nayo katika utekelezaji wa huu Mpango wa Maendeleo, kuna baadhi ya wizara muhimu ambazo zinabidi zipewe kipaumbele, mojawapo ni hii ya Nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninampongeza pia Mheshimiwa Waziri Deogratius Ndejembi kwa umakini wa hali ya juu pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri wake, tuna imani kubwa naye. Katika vitongoji ambavyo ni 64,359, tayari Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imepeleka umeme katika vitongoji 39,003. Ni 61% na ndani ya hizi siku 100 tayari wametenga fedha *1.2 trilion shillings* kwa ajili ya vitongoji 9,009. Sasa hapa wanasema kwamba watakwenda kutekeleza kwa muda wa miaka mitatu, ina maana bado tuna vitongoji vingine 30,000. Ninataka kujua Wizara inakuja na mkakati gani wa kuhakikisha kwamba hivi vitongoji vingine 30,000 navyo vinapata umeme kabla ya mwaka 2030.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokwenda 2030 maana yake mahitaji ya umeme yatakuwa ni makubwa zaidi ya *megawatts* ninadhani 10,000. Kwa sasa tuna *megawatts* 4,500, kwa hiyo ninashauri, nilikuwa napitia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, miradi inayoendelea kama 21 itatupatia *almost megawatts* 3,000 na kitu. Kwa hiyo, tuhakikishe inakamilika kwa haraka, lakini tuongeze vyanzo vya kuzalisha umeme hasa kwa kutumia njia hii ya *solar* na gesi asilia. Hii itatusaidia sana kuhakikisha kwamba tunapata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapo nitakwenda kwenye Jimbo langu la Butiama, tunavyo vitongoji 370, lakini tayari vitongoji 210 vimepata umeme. Ninaishukuru pia wizara na Serikali hii kwamba ndani ya siku 100 tunatekeleza vitongoji vingine 51. Nimeangalia katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, masuala haya ya *Universal electrification* kwenye hivi vitongoji na kulikuwa na mradi ule wanaouita *National Energy Compact*. Pale Butiama kuna vitongoji 37 ambavyo vingeweza kunufaika na huu mradi, lakini hadi sasa mkandarasi hajafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ajitahidi kwa sababu watu wengi wanadhani Butiama hali ni nzuri sana lakini Butiama bado tuna mahitaji ya msingi kama ilivyo kwenye wilaya nyingine. Kingine Mheshimiwa Waziri, kuhusu bei, Butiama bado ni wilaya mpya lakini kuna maeneo kama vile ya Kiabakari, maeneo ya Sirorisimba na Buhemba napo unakuta wamepangiwa kulipia umeme kwa shilingi 321,000 na wengi wameshindwa. Kama ambavyo wenzangu wamesema, ninadhani hili waliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakirudisha shilingi 27,000, watu watalipia, wameshafanya *wiring*, *then* watapata wateja na mambo yatakwenda. Kwa hiyo, ninaendelea kuwashukuru pia kwa hizi juhudi za kukamilisha hili bomba la mafuta ghafi kutoka Uganda – Hoima – Chongoleani, ninaona limefikia 82% pongezi kubwa sana kwa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija kwenye suala la mafuta, bei ya mafuta imeleta changamoto kidogo kutokana na hii vita ya Marekani na Iran, lakini ninaishukuru Wizara na Serikali kwa kuhakikisha kwamba bei ya mafuta haipandi kwa kiasi kikubwa sana hasa kwa kuendelea kulitumia Shirika letu la *TPDC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Mheshimiwa Waziri aendelee kuwa na msimamo, aliwezeshe liweze kufanya kazi zake vizuri ili kuhakikisha kwamba bei ya mafuta haipandi kama ilivyo kwenye nchi nyingine, lakini pia uhakika wa kupata mafuta nchini uendelee kuwepo. Kama wanavyoshauri hadi mwezi Julai huko wakati tunasubiri kuona hali inakwendaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masuala ya ujenzi, nilisoma kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, wanakwenda kuongeza namna ya kupokea mafuta na kuyahifadhi kwenye Bandari yetu ya Dar es Salaam na Mtwara. Ninaomba sana Wizara ijitahidi kuhakikisha kwamba hilo linafanyika na hizo asilimia za utekelezaji ziongezeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tuchukue mawazo ya Mheshimiwa Mbunge, *Engineer* Ezra alivyosema hapa tuweze kutumia *pipeline,* inaweza kuwa pia ni njia nzuri badala ya magari kwenda Dar es Salaam, basi kuwepo na vituo vingine katika maeneo mengine. Kwa hiyo, ninapenda pia kushauri kwenye hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija kwenye suala la hotuba pia, ninadhani ukiangalia umeme huu mnaopeleka kwenye vitongoji lakini kuna taasisi kama vile zahanati, vituo vya afya na hospitali ninadhani Mheshimiwa Waziri Mkuu alielekeza Wizara ijitahidi. Ninadhani wangekuja na mpango maalum wa kuhakikisha kwamba shule zetu, zahanati na vituo vya afya vinapata umeme. Waje na mpango tofauti kabisa ili *REA* waendelee kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua pia nafasi hii kuipongeza *REA* kwa kazi nzuri wanayoifanya, wanaendelea kufanya kazi hiyo vizuri sana. Kwenye Jimbo letu la Butiama tuna madini yanapatikana sehemu mbalimbali hasa madini ya dhahabu. Kwa hiyo, kuna maeneo kama vile Kwigutu, Buhemba, Tarani na Kyawazaru wanahitaji nguzo za umeme ili waweze kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo ambayo tuliomba nguzo 300 wakati Mheshimiwa Rais alipokuja kwenye ziara, Meneja wa pale Daniel amefanya *BOQ*, tukaletewa zile nguzo 300, lakini *Engineer* Babu ambaye amehamia Temeke akazipeleka anapojua Tarime.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wananchi wa Butiama mpaka sasa hivi wana malalamiko makubwa sana. Ninaomba Wizara ijitajidi tupate hizo nguzo angalau tuweze kupata umeme kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri; wanapowatafuta wakandarasi ambao wanasimamia hii miradi, hii ya *REA*, kuna baadhi ya wakandarasi ninadhani hawana uwezo mzuri. Kwa sababu tuna wakandarasi wengine wanaweza kuitumia hiyo kama fursa ya kupata fedha, lakini kuna mkandarasi mmoja kwenye jimbo letu anaitwa Alpha, *transfomer* iliharibika ya Kongoto, miezi sita na hajakabidhi mradi, hawezi ku-*replace* transfomer.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkandarasi huyo huyo kuna eneo moja Majengo pale Kiabakari ameleta *transfomer* ambayo inatoa njia mbili tu. Watu wanaohitaji kutumia umeme kwenye mashine hawawezi kutumia na tangu Januari anaambiwa arekebishe, hajarekebisha. Kwa hiyo, ninadhani wakandarasi inawezekana wapo kwenye maeneo mengine pia, wasitumie fursa hii kupata fedha za *TANESCO* halafu matokeo yake wakapeleka vitu ambavyo siyo vitu imara. Kwa hiyo, ninaomba sana hilo lifuatiliwe kwa umakini wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninadhani kingine tujifunze, tulikuwa na kampuni yetu ya *TIPER* ya *refinery*, kama inawezekana pia waiangalie. Kwa sababu tukiwa na vitu vya Serikali, inapotokea changamoto kama hizi ninadhani ni wakati muafaka. Tumeona *TPDC* imetusaidia bei kutokupanda. Kwa hiyo, kama inawezekana *refinery* hiyo iweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninarudi kusema, ninatumia nafasi hii pia kuipongeza Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuhakikisha tunakuwa na umeme wa hakika na tujitahidi sana, lakini masuala ya nishati safi, akina mama wa Butiama pia wanaomba kupata ile mitungi ya ruzuku kama itawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Wilson Charles Mahera. Mheshimiwa *Engineer* Kija Limbu Ntemi, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga na Mheshimiwa Bazilio Kapunda Mbwilo ajiandae.

**MHE. KIJA L. NTEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kupata hii nafasi ambayo umenipatia ili kuchangia Bajeti ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaanza kwa kuwapongeza Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Waziri, nikianza na jambo ambalo liko *hot* kwa sasa, jambo la mafuta ambalo amehangaika nalo sana. Ninaamini siku moja alikuwa anasema amejaribu kupungua kidogo kwa sababu ya kutokulala kwa sababu ya jambo la Taifa la mafuta. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alikupa siyo tu ulale, uhangaike na wananchi wake ili uweze kutimiza malengo yake ya kuwapatia nishati safi ambayo ni mafuta ambayo yamempa shida sana Waziri kwa wakati huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwamini na tunamtegemea na Waziri, ndiyo maana anapotembea sehemu zote na unapozunguka sehemu zote, anatuhakikishia kwamba mafuta yapo ya kutosha kwa sababu baada ya lile lango linaloitwa sijui *Hormuz*, sijui *Harmon*, ambalo limefungwa, ametuhakikishia kwamba nchi yetu haiwezi kukosa mafuta ya kutosha. Tunamwamini Mheshimiwa Waziri kwa sababu, ametupa mlengo mwingine wa kutuhakikishia kwamba nchi yetu haiwezi kukosa mafuta pamoja na kwamba yamepanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka kwetu kule Katoro yamepanda bei ila ni kipi bora kukosa ama kupata lakini kwa bei ambayo kidogo imeongezeka. Sisi tunampongeza sana, tunaamini Waziri pamoja na msaidizi wake, dada yetu Mheshimiwa Salome Makamba wanafanya kazi vizuri. Hongera sana, Mungu awabariki. Tunawatia moyo na sisi watu wa imani tutaendelea kuwaombea, Mheshimiwa Rais aweze kuwaacha hapohapo waendelee kufanya kazi vizuri. Maana alivyowaunganisha ni sawasawa kama alioteshwa kwamba awaunganishe wao ili waweze kumwakilisha vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo la mafuta kwa sababu limeshakaa vizuri na Waziri amesimamia vizuri na tunaamini tutaendelea kupata mafuta ya kutosha katika nchi yetu. Jambo la kwanza, ninawapongeza sana, tumetembea

kwenye miradi mingi ambayo wameianzisha na imefanikiwa kwa kiwango kikubwa sana. Mojawapo, utengenezaji wa nguzo za zege ambao ufanisi wake ni mkubwa sana. Tunaamini, namna ambavyo wanazalisha nguzo 80 mpaka nguzo 100 na kitu, tunawaamini sana kwamba watafanikiwa na watasonga mbele zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ule mradi utakuja kutatua matatizo ya nguzo za miti ambazo zimekuwepo; ndiyo maana unaweza kusikia Waheshimiwa Wabunge wanasema mara nguzo zimeanguka, zimefanyaje, au zimechakaa, ni kwa sababu ya nguzo zile ni za miti wakati mwingine zinaoza. Leo hii, kile kiwanda tunawaomba waendelee kuongeza ubora zaidi ili waweze kuzalisha nguzo nyingine zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanapopitishiwa bajeti hii, waweze kuongeza nguvu zaidi ili wazalishe nguzo nyingi zaidi ili nchi yetu ihame kwenye nguzo za miti, twende kwenye nguzo imara za *concrete* (zege) ili watu wote waweze kunufaika zaidi. Sisi Geita ametutoa kwenye janga kubwa sana, tulikuwa tunapata *megawatts* nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu chukulia Geita ile yote tunapata *megawatts* nne, ndiyo maana umeme ulikuwa ni wa shida, wa changamoto, lakini leo tunapata *megawatts* (sijui hata hizi *megawatts* ni jina maarufu sana) tunapata *megawatts* 90 na zaidi katika Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wameweza kututoa kwenye *megawatts* nne mpaka kwenye *megawatts* 90, sisi wananchi lazima tuwaunge mkono ili waendelee kufanya kazi vizuri. Leo *GGM* anapata umeme wa kutosha katika kazi zake na huyu *GGM* kwa upande wa Waziri wa Madini, anatupatia kitu kinaitwa *CSR* ambacho kinatusaidia jamii yetu. Wao wamempatia umeme wa kutosha na wakatuambia siku moja kwamba wanahakikisha kwamba kufika 2030 huenda *GGM* akajitegemea, akawa na *substation* yake ya kupokea umeme na wananchi wa Mkoa wa Geita wakajitegemea wao wenyewe. Sisi tunawategemea sana ili waweze kutuvusha, kutupeleka mbali zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Umeme wa Kishapu ambao wanazalisha *megawatts* 50 na wameshaziingiza kwenye Gridi ya Taifa. Tunawapongeza sana kwa sababu Mheshimiwa Rais amewaamini ndiyo maana wanafanya kazi nzuri. Pia, bado wanaendelea na ujenzi wa kuongeza *megawatts* 100 nyingine. Hii nchi tunatakiwa tusiwe na hofu ya umeme siku nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wanaendelea kuzalisha kwa mfumo huu na wanaenda tena kuzalisha *megawatts* 100 kwa kutumia mashamba ya *solar*, tunawaombea waendelee kujishika na kujituma zaidi ili waweze kufanikisha zaidi, lakini bado wana mradi mwingine ambao uko Ibadakuli ambao ni mradi mzuri sana na unaendelea kujengwa. Tunaamini baada ya bajeti hii, watakwenda kuongeza nguvu zaidi ili waweze kukamilisha. Watu wa Simiyu wanasubiria umeme, watu wa Shinyanga wanasubiria huo umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, baada ya bajeti Mheshimiwa Waziri hii tunawaomba waende wakakamilishe ule mradi ili uweze kukamilika na watu wa Simiyu na wa Shinyanga waweze kupata umeme wa kutosha. Katika dunia ya leo, watu wengi hatuwezi kuamini kwamba kuna umeme ambao wamezalisha wa *solar* maana tumezoea *solar* kuziona kwenye majumba yetu, tunawasha kataa kamoja. Ila Wizara wameweka mashamba ya fedha nyingi yanayozalisha huo umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine zuri ambalo Mheshimiwa Waziri amelifanya; mimi ninatokea Mkoa wa Geita, mkoa wa wachimbaji na mimi kabla sijawa Mbunge nilifuatilia umeme katika Machimbo ya Chato, Chato kule Msasa. Tulipata umeme wa kutosha na leo tunachimba kwa kutumia umeme, lakini bado. Hata juzi pia nimepokea simu kwamba tumeletewa umeme tayari kwenye mgodi, lakini tuna mapungufu kidogo, ya nini? *Solar* ni ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwomba tu Mheshimiwa Waziri atuongezee; sisi umeme wameshatuletea kwenye machimbo, tunaomba watuongezee *transformer* kubwa ambazo zinaweza kuendesha migodi mingi zaidi, tofauti na zilizopo kwa sasa. Tunawaamini sana watakwenda kutekeleza kwa sababu

ndiyo walioshikilia shilingi, wana watu wanaitwa *REA* wanaofanya kazi katika sehemu zetu zote. Katika kata zangu 11 zote za Jimbo la Katoro kuna umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wamekuja na hoja ya kutuongezea umeme katika vitongoji vyetu. Mheshimiwa Waziri ameweka banda pale nje, nimetembelea, ukifika kuna kompyuta inawashwa unaangalia vijii vyako vyote vilivyo na umeme na ambavyo havina umeme. Huu ubora tumeuona kwa Mheshimiwa Waziri. Kwa sababu wamepata janga hili ambalo huenda halijawahi kutokea tangu mwaka 1997 sijui tisini na ngapi la kukosa mafuta, ameweka historia nzuri ya kusimamia vizuri. Mungu ambariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vijiji vyetu vyote vile ambavyo havijapata umeme katika Jimbo la Katoro, tunamwomba sana baada ya bajeti hii atusaidie akatuunge mkono. Tunaamini Mheshimiwa Rais amemwagiza kutuunganisha kwa sababu ni kijana na ndiyo maana ameweka kijana ili aweze kufika kila sehemu kuwaona wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunawaomba, baada ya bajeti hii, tunaamini bajeti yake itapita kwa sababu hakuna Mheshimiwa Mbunge anayepinga bajeti yake, hakuna Mheshimiwa Mbunge anayekataa bajeti ya Wizara ya Nishati kwa sababu kazi waliyoifanya au walikotutoa ni mbali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, baada ya kusema hayo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri na msaidizi wake, Mheshimiwa Salome Makamba, sisi kwetu kule nyumba nyingi ni za nyasi na za tope, waje watuunganishie umeme baada ya bajeti yao ili watu wetu, watu wa Mheshimiwa Samia waweze kunufaika na umeme wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ni *champion* wetu wa nishati safi ya kupikia. Huyu mama amefanya kazi nzuri, tunaendelea kumpongeza. Hata ukipita kwenye mabanda huko kuna masufuria na majiko, ambayo yana sumaku. Ukienda kupika leo

unapika kwa kutumia sumaku na sufuria unaivisha chakula chako, hiyo ni kazi ya Dkt. Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, tumekwenda kwenye Shule ya Sekondari ya Kondoa ambapo wanapikia nishati safi ya kupikia. Tumeona namna Dkt. Samia Suluhu Hassan alivyoamua kusaidia shule za *boarding* na ambazo siyo za *boarding* kwa kuzipatia nishati safi ya kupikia. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachowaomba, ni baada ya bajeti yenu hii kupita, sijui ni leo au kesho, ni leo hii. Ninaamini Mheshimiwa Waziri baada ya hapa kwa sababu, yule Mheshimiwa Salome ninamwona mara nyingi; wanatembea, Waziri yuko huku, Naibu Waziri yuko huku, waende wakafanye *research* zaidi, shule wazipelekee nishati safi ya kupikia zipate huduma ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, baada ya kusema hayo, tunakushukuru sana na tunawaunga mkono. Mungu awabariki sana, tunawaombea bajeti yao ipite kwa kishindo. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kija, ahsante sana. Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, atafuatiwa na Mheshimiwa Bazilio Kapunda Mbwilo. Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, ajiandae.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza naanza kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ya kati ya Wizara zake, Wizara hii ameiweka kuwa sehemu ya mboni ya jicho lake. Kwa hiyo, ninampongeza sana kwa sababu, kazi ambazo zimefanyika kwa Wizara hii zimeonekana na zimetoa tija kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Waziri na Naibu wake kwa kazi kubwa kwa muda mfupi huu ambao wamefanya kazi kwenye Wizara hii. Ninawapongeza kwa sababu, hata tukihitaji ufafanuzi wa mambo ya nishati, kwa maana ya umeme

*REA* Vijijini, wako tayari kusikiliza ushauri wetu na wanatupokea kwa haraka sana. Ninawapongeza sana, endeleeni kuchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi wa Taasisi hizi, hasa *REA* pamoja na *TANESCO* kwa kazi kubwa ambayo inaendelea kufanyika. Wengi wamezungumza hapa, umeme ni hitaji la wananchi duniani na sisi hapa Watanzania tunahitaji umeme wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mabunge ya nyuma yanapita *TANESCO* ilikuwa inalaumiwa sana, lakini leo *TANESCO* tunaipongeza sana kwa kazi nzuri ambayo inaendelea. Umeme *REA,* leo tumekwenda takribani vijiji, karibu tunataka kumaliza, kwangu kule nimebakiza Kijiji kimoja tu cha Ijinga ambacho kiko kisiwani, lakini tunaendelea kuongea na Mkurugenzi wa *REA* na tayari mkandarasi atakayeweka *solar* kwenye kijiji hicho amepatikana. Kwa hiyo, ninaamini kwamba, tunakwenda kumaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme huu uliposogea kwenye vitongoji uchumi wa wananchi wetu umekuwa sana kwa sababu, kila kitongoji ambacho umeme umefika wananchi wamejenga viwanda vidogo vya kukoboa mpunga. Leo vijijini wanapata bei ileile ambayo walikuwa wanaipata wakipeleka kwenda kuuza mjini, kwa hiyo, imebadili kabisa mambo ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, umeme kwenye vitongoji unahitajika. Mimi kule Magu nina vitongoji 508 tumeweka vitongoji 217, sasa hivi tayari vitongoji 89 viko kwenye mpango ambao ni *REA* hii inaendelea. Kwa hiyo, vitakuwa vimebaki vitongoji 202. Ninaomba sana Serikali kwa sababu, ni hitaji la msingi kwa wananchi, vitongoji 202 viwekwe kwenye mpango ujao, ili tuweze kumaliza. Hapo tutakuwa tumeleta uchumi sana kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Mwanza, Magu, ndiko eneo ambalo sasa hivi lina viwanda vingi, kwa hiyo, umeme wakati wote unaendelea kupungua. Ninaipongeza sana Wizara kwa

kuweka mpango wa kujenga *substation* pale Matela; pale Matela kuna Kiwanda kikubwa cha Chuma ambacho mwekezaji kwa kweli, amejitahidi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, palepale Matela ndipo ambapo tunataka kuweka *Industrial Park* ya Mkoa kwa hiyo, *substation* hii itasaidia sana kuhakikisha kwamba, umeme unakuwa wa uhakika. Tunapoipongeza Serikali na Wizara, tunaona hivi vitu ni *tangible* kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo la mafuta. Huwa tunazungumza kila mwaka kwamba, Mbuga ya Wembere kuna mafuta, Ziwa Rukwa kuna mafuta, Ziwa Nyasa kuna mafuta. Ufike wakati sasa haya mafuta yachimbwe. Tunapoelekea hatutayafanyia kazi, kama leo magari yanatengenezwa ya gesi. Tumepita kwenye mabanda pale, wanatengeneza magari 100% ya umeme, maana yake ni kwamba, tutakuwa na rasilimali ambazo hazitakuja kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ndipo Wizara inatakiwa iwekeze macho na namna gani tuchimbe haya mafuta yatusaidie, kama ambavyo wenzetu wa Hoima, Uganda, wanavyochimba. Tukichimba haya mafuta yana *products* nyingi, kwanza tutapata lami humohumo kwenye mafuta, tutapa grisi humohumo kwenye mafuta, tutapata *oil* humohumo kwenye mafuta, tutapata bidhaa za plastiki humohumo kwenye mafuta na tutapata bidhaa nyingi zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunapotazama siyo mafuta pekeyake ni vitu vingi ambavyo vinaendana na mafuta. Kwa hiyo, ninaishauri sana Serikali, tunayo mipango mingi ya muda mrefu, lakini kwenye jambo hili la mafuta kwa sababu, ndilo litakalokwenda kuchochea uchumi na kuondokana na malalamiko yanapotokea majanga kule duniani watu wanagombana, wenye uwezo, sisi tunakua tuko salama kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hatuna uwezo leo kwenye mipango ya muda wa 2025 - 2030 imo, lakini mpaka 2050 nione nchi tunawekeza kwenye suala la uchimbaji wa mafuta, ili

kuondokana na mambo mengine. Nchi hii inakua, lakini nchi hii hii inategemewa na nchi nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Uganda wanachimba mafuta, wanasafisha *crude oil,* bado wanajenga *refinery* kule, itasaidia sana kwenye ukanda wetu wa Afrika Mashariki na Kati. Bado sisi, kama Tanzania, nchi kubwa ambayo imebarikiwa rasilimali ni vizuri tukaweka akili zetu kuhakikisha kwamba, mafuta haya tunayachimba, ili yaweze kuwanufaisha Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ama kuweka mfuko wa maandalizi hata kama ni wa miaka kumi tupate fedha nyingi za kuchimba, ama tuweke utaratibu. Hapo Waziri akope, kukopa siyo dhambi, kukopa ni *plan,* kukopa ni mafanikio, kwa hiyo, bado ninataka mafuta ambayo yameonekana Wembere, kama yapo na kwenye Maziwa yetu kama yapo na kwenye Bahari, kama yapo, yachimbwe sasa kwa wakati, sisi ni viongozi wa nchi hii tusisubiri wengine waje.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muda ambao tunatakiwa, kama nchi, tuamue tusiweke mipango ya muda mrefu kwenye karatasi tu, ambayo haitekelezi. Kwa hiyo, ninaipongeza sana Wizara na ninaipongeza Serikali kwa kuweka utaratibu huu na mipango ambayo inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jana kuna Mbunge hapa amezungumza, sisi kule vijijini tuna viwanda ambavyo vinasindika kwa muda mfupi. Hata pale Babati vile viwanda vya alizeti vinasindika alizeti kwa muda wa miezi mitatu, mbegu zinakatika, lakini kuna chaji ya 75% ya *kVA* kwa gharama ambazo ametumia msindikaji. Hiyo inawapa gharama wasindikaji wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuangalie hii chaji ya *kVA,* iliwekwa wakati mitambo yetu ya kuzalisha umeme inatumia mafuta. Leo tunatumia mitambo ya kuzalisha umeme; ipo ya jua ambayo ni *solar,* ipo ya maji na ipo ya joto ardhi. Kwa hiyo, ninaomba sana, kama leo tunazalisha umeme kwa njia nyingi, tuone namna ambavyo tunaweza kuiondoa hii, ili kuwasaidia wawekezaji wazawa waweze ku-*compete* na bidhaa zinazozalishwa nje kwa sababu, ni gharama kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana, kwenye suala la nishati ya kupikia akinamama na ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuona hili jambo linastahili akinamama wapate nishati mbadala ya kupikia. Sasa yako maeneo, kwa mfano makaa ya mawe; yako maeneo kule vijijini mwananchi hawezi kupata, yaani anapotaka kupika kwenye lile jiko hawezi kupata haya makaa ya mawe! Akanunue wapi? Sana sana yanauzwa mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tungeona sasa nishati mbadala hii inafika vijijini kule. Kama kuna ma-*agent* wanasambaza hizi bidhaa wapewe maeneo waweze kufika vijijini, ili akinamama waweze kutumia majiko haya ambayo yanatumia gharama ndogo kuhakikisha kwamba, maisha ya Watanzania yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la gesi ya kupikia nadhani sijajifunza vizuri sana, lakini bado gesi hii inatakiwa iwe kwenye vipimo vya chini. Mtu ana shilingi kadhaa anakwenda kununua lita moja anapika, ametoka kwenye kibarua chake anapitia lita moja ya gesi anakwenda kuweka kwenye jiko anapika, kesho tena ndiyo kunakucha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuangalie namna ya uwekaji kwenye vipimo hivi, ilimradi watu wote waweze kununua hii gesi kwa sababu, ipo gesi ya lita tano na lita 10, ni wachache ambao wanaweza kumudu hizo gharama. Tuone namna ambavyo Serikali itafanya, tumepiga hatua kubwa sana, ili kuhakikisha kwamba, wananchi wanaendelea sasa na nishati ambayo inafaa kwa maisha ya Watanzania na kuondokana na majiko ambayo tunatumia kuni nyingi. *(Makofi)*

Mheshimwa Naibu Spika, kule usukumani ukifika mama macho yake ni mekundu, anaambiwa huyu ni mchawi kumbe ni moshi. Moshi ule unapopika kila siku macho yanageuka. Kwa hiyo, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais, Wizara, Mheshimiwa Waziri pamoja na wanaowasaidia, kwa namna ya pekee ambavyo wanaendelea kuisaidia Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiswaga, ahsante sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Bazilio Kapunda Mbwilo, atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi. Mheshimiwa Dkt. Godwin Olyce Mollel, ajiandae.

**MHE. BAZILIO K. MBWILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ambayo nimekuwa nikiisubiri sana. Ninaanza kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake, andiko lao ni zuri sana na kama litatekelezwa jinsi walivyoliandika nadhani litatupatia mafanikio mazuri sana katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani haziishii kwao, ninawashukuru zaidi kwa ile timu ya wafanyakazi wa *TANESCO* pamoja na *REA,* waliyoniletea kwenye Wilaya ya Nkansi, timu ile ni nzuri sana inafanya kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakati ninahitajika kujibu maswali ya wananchi kijijini, mwambao mwa Ziwa Tanganyika. Nikiwapigia simu hawa wenzangu wa *REA* na *TANESCO,* saa nyingine wananimbia tutakwenda leo, kama siyo leo kesho. Nikiinua simu kweli hiyo leo au kesho wanakuwa wamekwenda. Ile timu ni nzuri sana na ninaomba Mheshimiwa Waziri asii-*disturb,* iendelee kubaki kulekule Wilayani Nkansi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri baada ya hilo umepewa sifa nyingi sana kwa mpango mzuri, hasa wa kuhakikisha unaendelea kuwa na umeme hata wa ziada, lakini Mheshimiwa hapo ningependa anieleze, je, ameshafanya utafiti katika Maporomoko ya Kalambo?

Mheshimiwa Naibu Spika, yale ni maporomoko ya pili kwa *height* ndani ya Bara la Afrika na ni ya kwanza kwa Afrika Mashariki yana mita 235. Sasa leo tuna miaka mingi hatujaweza kufanya utafiti pale, kama utafiti utafanyika, ninaamini tutapata umeme mwingi sana. Tena pale ni *single drop,* sina uhakika kama Mheshimiwa Waziri amefika, ninatamani siku moja afike pale Kalambo *Falls* aone bahati tuliyonayo sisi Watanzania, lakini hayajafanyiwa kazi. Kwa hiyo, katika ku-*summarized* ninatarajia nione ameifanyia kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, sasa ninataka nirekebishe, Waziri amesema kwamba, katika Mkoa wa Rukwa vijiji vyote vina umeme, siyo kweli! Mimi ndiye Mbunge wa Nkansi Kaskazini, kuna kijiji kimoja kinaitwa Mandauhuru, kiko Kata ya Mkinga. Kijiji hicho kipo kisiwani na hakijapata umeme bado.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *Lake Tanganyika* tuna vijiji viwili tu, ndani ya ziwa, Mandakerenge, ninashukuru sana, wamenipatia umeme, lakini Mandauhuru bado. Wataalam wetu wametuambia kwamba, Mandauhuru kitapata umeme wa *solar*. Sasa umeme siyo taa peke yake, umeme ni kichocheo cha maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii mwananchi wa Mandauhuru hata akitaka kufanya *welding* jembe lake, ili aende shambani, analazimika kutoa shilingi 2,000 kuvuka Kerege, kuvuka Mkinga na shilingi 2,000 kurudi. Vilevile bado akinamama wanabeba mahindi kwenda kusaga huko Mkinga, kijijini kwao hakuna na hivi sasa tumeanza kujenga dispensary katika hicho kijiji, sasa itahitajika friji. Wakitupa umeme wa *solar,* kweli utaweza kuendesha friji?

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani kwa uzoefu tulionao kule. Kwa hiyo ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, wale watu wamejisikia unyonge…

**MHE. KIJA L. NTEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. BAZILIO K. MBWILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakisikia taarifa…

**MHE. KIJA L. NTEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bazilio, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa, yuko wapi?.

**MHE. KIJA L. NTEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, niko huku. *Engineer* Kija Ntemi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Ntemi haya.

**TAARIFA**

**MHE. KIJA L. NTEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi uliopo Kishapu wa Kufua Umeme Kupitia *Solar* ni mradi unaozalisha umeme na sasa unazalisha *megawatt* 50, ambazo zinaingizwa kwenye Gridi ya Taifa. Ni umeme wa uhakika siyo kwamba, umeme wa *solar* hauwezi kuendesha friji. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, umeme unazalishwa kwa mfumo mzuri kabisa na unakuwa umeme wa uhakika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana. Mheshimiwa Bazilio, Taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. BAZILIO K. MBWILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei hiyo Taarifa. Siipokei kwa sababu, wataalam wetu wametuambia, kwanza wanaanza na umeme wa *solar,* halafu huo mwingine utafuata baadaye. Wametuambia kabisa hauwezi kuendesha mashine za kusaga, huo umeme wa *solar,* hauwezi kuendesha mashine za *welding*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ndiyo maana wananchi wamesema, kama ni huo mbona *solar* tunazo na wakati mwingine siku mbili mvua inanyesha kule, mawingu yanatanda, mionzi ya jua haipo, kwa hiyo, *solar* inakuwa *down*. Ndiyo maana wakasema kama ni huu wa *sola,r* basi sisi tubaki na unyonge wetu. Kwa nini Mheshimiwa Waziri kijiji changu kibaki na unyonge? Tutasikitika sana. *(Makofi)*

**MHE. ALI HAIDAR MADEWEYYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bazilio, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa. Karibu.

**TAARIFA**

**MHE. ALI HAIDAR MADEWEYYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe Taarifa Mchangiaji. Mwaka jana Mheshimiwa Aweso tulizima mitambo ya dizeli Mwanza na mpaka sasa hivi

tunatumia *solar,* kwa ajili ya ku-*operate* ile mitambo. Umeme wa *solar* ni imara na ni maradufu. Ninaomba kumpa Taarifa mchangiaji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bazilio, Taarifa hiyo, unaipokea kutoka kwa Mheshimiwa Madeweyya?

**MHE. BAZILIO K. MBWILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei kwa sababu, siufahamu huo mradi na je, kwake ana umeme wa *solar*? Kama angeanza kwake kufunga umeme wa *solar* angenisadikisha kwamba, umeme huo unafaa, lakini sidhani kwamba, yeye ana umeme wa namna hiyo. Ninaomba niendelee. *(Makofi)*

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Taarifa huwa ni mbili kwa hoja moja, Mheshimiwa Sanga.

Mheshimiwa Mbunge endelea.

**MHE. BAZILIO K. MBWILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninakuja tena kwenye ombi lingine, kwa sababu Nkasi iko *highland* na *lowland* kando kando ya Ziwa Tanganyika, hapo katikati ni Msitu wa Lwafi pamoja na ile *game reserve*. Hapo nguzo zinaanguka mara kwa mara kutokana na moto ambao unachomwa labda makusudi au kwa mpango maalum, lakini hizi nguzo zinaliwa na mchwa. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri eneo hilo tulibadilishie nguzo.

Mhshimiwa Naibu Spika, siyo hilo tu kandokando mwa Ziwa, Ziwa Tanganyika sasa limefurika na maji yanakuja nchi kavu, kwa hiyo, vijiji vinalazimika kuhamisha makazi kutoka walipokuwa karibu na maji kuja juu. Huko tutakapohitaji kutengeneza ninamwomba sana Waziri, tuweke nguzo za zege na siyo tena zile tulizozizoea.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi wa *TANESCO* na *REA* wanapata shida sana hasa kandokando ya Ziwa, zile nguzo wanazisafirisha kwa boti kwa sababu hakuna barabara katika

eneo lile. Kwa hiyo, ninaomba, tunayo boti moja ipo Kata ya Kirando, lakini ninaomba sana tupate boti ya pili iende walau ikawe *stationed* Kabwe ili hayo yaweze kusaidiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, watumishi wetu hao niliowasifia hawana vyombo vya usafiri vya kutosha, wanazo gari tatu tu kwa Wilaya nzima, hayatoshi hayo magari. Wanayo magari matatu na bajaji na pikipiki, ninamwomba sana atakapokuja ku-*summarize,* ninaomba sana *include* hao watu waweze kupata usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ila siyo kwa umuhimu, tumekuwa tukiona kando ya Ziwa Tanganyika ndege zinapita tunaambiwa hawa ni *Beach Petroleum* wanakuja kufanya utafiti wa mafuta. Hiyo ilikuwa mwaka 2010 – 2013 hivi, hatujapata kusikia kwa sauti yoyote ya Serikali kuhusu matokeo ya utafiti huo. Kama tunavyoona, Tanzania tumebarikiwa wenzangu wametoka kuongea, tumebarikiwa sana kuwa na *resources* nyingi siamini kwamba hatuna mafuta, siamini! Huenda *speed* yetu kama nchi ndiyo imekuwa *slow* hatujaweza kufanya utafiti wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa timu hiyo nzuri ya vijana wawili wenye nguvu kabisa, hebu katika hii miaka mitano wafanye utafiti na ikiwezekana watuambie mafuta yako wapi, hao wakubwa wakipigana sisi tunaendelea na mafuta yetu. Inasikitisha kuona Nchi kama Tanzania tunakosa mafuta wakati tunazo rasilimali nyingi za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa muda. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Bazilio. Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi tutamalizia na Mheshimiwa Dr. Godwin Oloyce Mollel.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Wizara ya Nishati ambayo iko mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumpongeza Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri sana ambayo anaendelea kuifanya katika nchi yetu. Tutakuwa wapungufu wa shukrani kama tutashindwa kumshukuru Mheshimiwa Rais hata katika hili suala la mafuta ambalo limeleta mtikisiko katika dunia, lakini katika nchi yetu sisi bado tumeendelea kuwa imara na kwamba tuna hifadhi ya kutosha. Mikakati na mipango ya Serikali inaonesha kabisa kwamba kuna dhamira ya dhati ya kuhakikisha kwamba kwa kiasi kikubwa tunadhibiti mfumuko wa bei ambao unaweza kusababishwa na ongezeko hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya salamu hizo ninaomba pia nimpongeze sana Waziri, Ndugu yangu Deo Ndejembi pamoja na Mheshimiwa Wakili Msomi Salome Makamba na watendakazi katika ngazi ya Wizara kwa maana Katibu Mkuu Mramba, pamoja na Katibu Mkuu Nishati ndugu James Mataragio na watendakazi wote katika Idara zote ambazo ziko chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nikiri kwamba katika Wizara zetu zote hii inaweza ikawa ni Wizara ya mfano, kwa maana taasisi zake zina uwezo mkubwa sana wa kujisimamia, ndiyo maana michango ya Wabunge humu ndani kila mmoja anatoa ushuhuda wa namna ambavyo taasisi zinazosimamiwa chini ya Wizara hii zinavyotoa ushirikiano kwa Wabunge, lakini pia na wadau wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kwenye suala la mafuta, taasisi yetu ya *EWURA* ni miongoni mwa taasisi ambazo wenzetu katika nchi nyingine za Afrika wanakuja kujifunza namna *EWURA* wanavyoweza kusimamia katika eneo hili la nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutambue, kama siyo uwepo wa *EWURA* maana yake vita ile ya kule Mashariki ya Kati ilivyoanza tarehe 28 Februari, siku ileile bei ya mafuta ilipaswa kupanda, lakini kwa mikakati na mipango madhubuti ambayo imewekwa na taasisi yetu hii tumepata angalau muda wa kujipanga na bei zilikuja kupatikana baada ya mwezi mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ndiyo utaratibu wa kawaida wa *EWURA*, kwamba kila Jumatano ya kwanza ya mwezi wanatangaza bei. Kwa hiyo, wakati mwingine kwa kuwa hakukuwa na changamoto watu hawafuatilii, lakini ninawaasa Wabunge taasisi zetu hizi zinatolewa mfano na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitoe mchango wangu kwa Wizara. Katika jambo hili tumepata funzo, tunayo *storage tank* ambazo tunazo katika nchi yetu zinazo uwezo wa kuhifadhi lita bilioni 1.7. Mafuta haya pia yanachanganya na mafuta yanayokwenda nje ya nchi. Mafuta tunayotumia ndani ya nchi ni lita milioni 500. Kwa hiyo, ukiangalia kwa wepesi kwamba *storage tank* yetu kwa milioni 500 hizi tungekuwa tuna uwezo wa kuhifadhi kwa miezi mitatu, lakini 1.7 ni pamoja na yale yanayokwenda nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunajenga *single receiving terminal* kwa ajili ya mafuta yote yaingie katika ile inayojengwa na Mamlaka ya Bandari kisha yapelekwe katika *storage tank*. Ninaiomba Wizara na Serikali kwa ujumla wake ichukue jukumu sasa la ku-*decongest* Jiji la Dar es Salaam. Hizi *strategic facilities* tuzijenge nje ya Jiji la Dar es Salaam. Kwa mfano, tunaweza tukaanza Makambako ili tupunguze malori yanayotoka Malawi, Zambia na kwingineko yaishie kule Makambako.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza tukatumia uwepo labda wa bomba la *TAZAMA* au tukaanzisha kitu kingine, lakini kwa *corrido* ya katikati, Dodoma tuwe na *storage facilities* Kahama, tuwe na *storage facilities* na kule Mwanza ambako tunaelekea kwenye kupitia Ziwa Victoria, tunaweza tukapeleka mafuta Uganda, tukapeleka mpaka hata Sudani ya Kusini.  Yote haya ni mipango ambayo tunatakiwa tuizungumze ndani ya Serikali na tuweze kuleta tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nirejee Jimboni kwenye Mamlaka ya Usambazaji Umeme Vijijini – *REA*, hawa nao wanafanya kazi kubwa sana na iliyotukuka. Kwa kweli tunawapongeza sana Mkurugenzi Mtendaji na timu yake yote, tunawashukuru sana kwa namna ambavyo tunashirikiana katika kusukuma gurudumu la maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Lushoto kwa Wilaya nzima yenye Majimbo matatu, tuna vitongoji takribani 400 bado havijapata nishati, tunaomba sana katika mipango hii tuhakikishe kwamba vile vitongoji vinapata nishati ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo mradi wa gridi imara, tunacho kituo cha kuongeza nguvu pale Bumbuli kinajengwa ambacho ni cha KV 132. Tunaomba sana mkandarasi mpaka sasa hajaingia *site*. Tunaomba apate msukumo aende *site* ili aweze kuboresha upatikanaji wa umeme katika Wilaya ya Lushoto, ambako kwa kweli umeme unakatika sana kwa sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine tuliomba pale tupate nguzo na nguzo tunazohitaji sisi siyo nguzo za zege wala siyo za mbao. Sisi tunahitaji nguzo za chuma. Wilaya ya Lushoto ni milima, tukipeleka za nguzo za zege zinahitaji *cranes* katika kuzipandisha na jiografia ilivyo itakuwa ngumu. Kule tupate nguzo nyepesi za chuma ambazo zitakuwa rahisi na hazitasababisha huu umeme unaokatika mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nukta hii ninaomba sana wakandarasi wanaofanya vizuri tuwapongeze. Kule Lushoto na Mkoa mzima wa Tanga kwenye Awamu ya Pili ya usambazaji umeme kwenye vitongoji tulikaa miezi sita bila mkandarasi, kwa sababu kila mkandarasi aliyekuwa anapelekwa kwenye Mkoa wa Tanga hasa Wilaya ya Lushoto, kwa sababu ya jiografia ya milima alikuwa anaogopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, yupo mwamba mmoja anaitwa *Dem Construction* ambaye ni mzawa, akachukua ile kazi na akafanya kazi nzuri. Akaupandisha umeme kwenye milima, kwenye majabali, kwenye mabonde, sasa watu wa aina hii ndiyo watu ambao wanapaswa kupewa kazi katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo mara zote sana sisi tunawapenda wazawa, mara nyingi tunataka hawa watu ambao wanatoka mabara mengine, lakini ni muhimu sasa wenzetu hawa ambao wana uwezo wa kufanya kazi kwa tija, kazi kubwa katika maeneo korofi, tuwape kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ninalisema hata kwenye barabara. Kuna kampuni ya *Estim Construction* imejenga njia nane kutoka Kimara kwenda pale Kibaha, wamefanya kazi nzuri. Watu kama hawa zinapopatikana fursa kwenye Nchi za wenzetu kama *Comoro*, Msumbiji kule ambako bado wanahitaji hizo huduma tuwasukume waende huko kwa sababu pia wataleta fedha ndani, lakini ajira za watu wetu zitakuwa zinaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninatoa rai kwa Serikali, kwamba tuwajali wakandarasi wazawa wanaofanya kazi vizuri, Mara nyingi tumekuwa tunawaona wazawa kama hawawezi kazi. Hapana! Tunawaona wamethubutu na wameweza tuwawezeshe. Wanaoweza ndani ya nchi tuwape uwezo huo, lakini wale wengine ambao tunaweza tukawasukuma kwenye nchi jirani ambazo wenzetu wanatuamini pia tuwasaidie kupata kazi huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku zote mjenga nchi ni mwananchi, hizi kampuni za nje wakati mwingine tunajua ambayo yanatokea, tunaona mara kadhaa wakandarasi wananyang'anywa pasipoti, lakini kwa mzawa hilo haliwezi likatokea kwa sababu tuko ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi. Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel atakuwa mchangaji wetu wa mwisho kwa mchana huu. *(Makofi)*

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ni mara ya kwanza kusimama hapa baada ya uchaguzi mkuu na ule uchaguzi mdogo ambao umefanyika kwenye Wilaya yetu ya Siha, ninatumia nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Wilaya ya Siha kwa kuendelea kuniamini na kunipigania wakati wote hata kama mazingira yanakuwa magumu kiasi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii pia kumshukuru Rais wetu, Mwenyekiti wa Chama chetu, Dkt. Samia Suluhu

Hassan kwamba jina langu lilipofika Kamati Kuu walilirudisha ili nipeperushe bendera ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona Wabunge wamechangia vizuri sana, wamesema mambo mazuri sana, lakini kwa aina ya Waziri na Naibu Waziri wake ambao tunao pale nikiwaangalia sina kikubwa cha kuwaambia na cha kuwashauri, kwa sababu nimewafuatilia vizuri sana, wanafanya kama matarajio yetu sisi wengi na kama ambavyo sisi wengi tungefikiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kuwaambia wale wachache ambao wanaweza wakawa wanafikiri tofauti, niwaambie kwa nini sisi leo Bunge hili na Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunaenda kumpa bajeti yake kaka yetu Mheshimiwa Ndejembi pamoja na jembe lake Naibu Waziri Makamba, waende wakafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaenda kufanya hivyo kwa sababu ya ni nani yuko nyuma yao. Ni nani yuko nyuma ya Mheshimiwa Ndejembi na ni nani yuko nyuma ya Mheshimiwa Makamba? Tusijisahaulishe tukumbuke kwamba Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan baada ya kuondoka Rais wetu mpendwa Dkt. Magufuli, aliipokea hii nchi na akatuvusha salama na nchi yetu ikawa na mshikamano na umoja. Huyo ndiyo yuko nyuma ya kaka yangu Mheshimiwa Ndenjembi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huyo ndiyo Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye Dkt. Magufuli aliacha Bwawa la Nyerere likiwa chini ya 38% na akaja akalimaliza na leo limekwisha linafanya kazi, huyo ndiyo Dkt. Samia ambaye sababu tunayom-*support* leo na tuna uhakika kilicholetwa hapa kinaenda kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tusijisahaulishe pia kwamba, Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ukiangalia *SGR* ilianza aliikuta ukijumlisha *lot* zote unakuja kugundua Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan yeye ndiye ametafuta 70% ya fedha zilizomalizia *SGR* na leo tunakwenda masaa matatu Dar es Salaam kutokea Dodoma kutoka masaa nane. Huyo ndiyo Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye leo tumesimama kwa kujiamini na hatuna wasiwasi

tunaenda ku-*support* bajeti ya Wizara ya Nishati, kwa sababu tunajua ni yule yule aliyetuvusha kuanzia mwaka 2022 mpaka leo, ni yeye anaenda kufanya hii kazi na ni yeye anaenda kumwezesha kaka yangu Ndejembi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tusisahau vile vile kwamba, Rais huyu Dkt. Samia Suluhu Hassan ni yeye ambaye alitukuta kwenye mgogoro mkubwa wa ugonjwa wa *COVID-19* na tukiwa na mambo mbalimbali kimataifa na kila mahali, yeye akaturudisha kwenye mshikamano na akaendeleza ajenda ya Tanzania. Akatumia fursa hiyo, akapata trilioni za fedha akatumbukiza kwenye sekta ya elimu, sekta ya afya, sekta ya maji na kwenye utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akanunua 97% ya teknolojia tulizokuwa tunazifuata nje ya Tanzania na akawekeza kwenye miundombinu, matokeo yake kilichotokea ni kwamba vifo vya akina mama vikashuka kuanzia 556 mpaka 104. Maana yake ni nini? Dunia ikamtafuta na ikaangalia dunia yote, nchi zote za duniani akaibuka yeye kidedea akachukua nishani hiyo ya ushindi huo. Ikatufanya Tanzania tukawa nchi ya saba duniani kupata hiyo nishani, ndiyo huyo leo hapa tunamtegemea akafanye kazi hii ya nishati *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, akatufanya kwa Afrika tukawa nchi ya kwanza kupata hiyo nishani, ndiyo huyo Rais leo tunamtegemea akafanye hii kazi ambayo tutaenda kuipitisha kwa juhudi ya hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais huyu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akawa mwanamke wa kwanza duniani kupata hiyo nishani, kwa maana ya Rais wa kwanza mwanamke kupata hiyo nishani. Hayo ameyafanya nyuma hata leo yanatufanya hiki ambacho kiko mbele yetu, tunao uhakika kwamba kinaenda kutekelezeka. Ndiyo maana hata ukiangalia mwaka 2022 ulitokea kwenye mafuta mtikisiko kama tulioupata leo, lakini akapiga mahesabu yake na tukavuka salama kuliko nchi yoyote iliyotuzunguka hapa Afrika Mashariki, leo ni yeye huyu anakwenda kutuvusha sehemu nyingine zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ni huyo baada ya kutumbukiza fedha kwenye utalii ni yeye huyu aliyesababisha ukienda kaskazini ambapo kuna utalii kulikuwa na mambo yanaitwa *low season* na *high season*, ikawa watalii wanakuja wakati wote hakuna cha *low season* na *high season* na watu wa utalii ni mashahidi jinsi ambavyo hela nyingi zimeingia kwenye eneo la utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niseme ni huyu Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ametusaidia amefanya hilo la utalii likaenda vizuri. Hata hivyo, niseme, Waziri wetu Ndejembi, huyu Waziri Waheshimiwa Wabunge ni Waziri ambaye anajua Wizara anayoisimamia ina maana gani kwenye siasa zetu kule Majimboni kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa kwenye uchaguzi mdogo Siha, yeye mwenyewe bila mimi kumtafuta alinipigia akaniambia kwako kuna uchaguzi, ninasafiri ninamtuma mtu aje akusaidie, akamtuma Salome Makamba, Mheshimiwa Salome Makamba amekuja amepiga. Aliporudi akanipigia akaniambia ninakuja nikamwambia usije, ushatuma ashasafisha kila kitu nikiwa na vitongoji 40 havina umeme, akaondoka ameacha vitongoji 14 tu havina umeme. Huyu ndiyo Mheshimiwa Ndejembi ambaye leo tunaenda kum-*support* hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ninasema tunam-*support* kwa sababu ana shirika lake la *TANESCO* ambalo linaongozwa na Lazaro Twange, Wabunge ni mashahidi, hata jana tu nilikutana na mwananchi mmoja akaniambia niliwapigia waje wanifungie umeme kwangu, nilivyowapigia wakaniambia ni ramani hujatuma. Ramani ilivyotumwa wakanipigia wenyewe na umeme umefungwa kwangu. Hao ndiyo Wakurugenzi Lazaro Twange ambaye akiingia sehemu maana yake kwenye hilo shirika, Rais anasifiwa ana-*relax*, Waziri anasifiwa ana-*relax*, ndiyo aina ya Wakurugenzi ambao wako hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ndugu zangu tusipate shida. Tuna Wakurugenzi ukienda *REA*, *REA* leo wanakuja nyumbani kwangu kuongea na mimi kujadili wananiambia tumetumwa na Mkurugenzi Mkuu tuje tujadili na wewe kuhusu Jimbo letu, maana yake ni nini? Waziri aliyeko na Wakurugenzi wake wanatambua

maana yake nini inapofika umeme kwenye siasa za Wabunge na wananchi kule. Hao ndiyo Mawaziri na ndiyo maana leo tunaenda kumpitishia Mheshimiwa Ndejembi bajeti yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaomba Wabunge twende tupitishe na sisi Jimbo la Siha tulishapitisha kutoka mwezi uliopita, kwamba wewe unatakiwa uendelee uende mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuna maneno mengine wanasema sijui Heche kasemaje, sijui nani kasemaje. Mimi na Mheshimiwa Makamba tulikuwa huko na akina Heche tunajuana vizuri, wala Mheshimiwa Heche akitusumbua, tunamtuma Mheshimiwa Makamba anamtosha Heche, anamalizana naye asubuhi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu Heche ambaye ukimsikiliza sana amejichanganya, anafikiri sasa hivi Tanzania tuko kwenye hali ya kugombea uhuru, yaani tunamwondoa mkoloni, ameshindwa kuelewa kwamba tulishapata uhuru mwaka 1961, sasa hivi tunapambana kwenye *idea* za kujenga uchumi wa nchi. Sasa tu kama ubongo wake umeshindwa kuelewa hilo, ndiyo atatushauri mambo magumu magumu kama ya umeme na namna ya kuhakikisha bei za mafuta zinakwenda vipi? Hao tuachane nao, twendeni tukaijenge nchi yetu, twendeni tuka-*support*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna maumivu machache ambayo tunayapitia, leo wenzetu kwenye hizi nchi ambazo zimeleta shida wanapoteza watu, wanapoteza fedha, lakini wanapambana kwa ajili ya kesho ya nchi yao. Sisi leo tunasema hapa hata kama kutakuwa na maumivu kidogo tutapitia, tuko tayari kuumia kidogo kwa ajili ya kesho ya Taifa letu na hatutarudi nyuma kwenye miradi ambayo inatengeneza kesho ya Taifa letu, eti kwa sababu ya kuogopa maumivu kidogo tunayopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamalizia kwa kusema kwamba nchi zote zenye usalama wa nchi, nchi zote zilizotuzunguka ninaomba tu dakika moja. Nchi zote zilizotuzunguka ziliingia kwenye shida kwa sababu waliruhusu wajinga wachache

wamchokonoe chokonoe Rais na wachokonoe taasisi inayoitwa Ikulu. Ninataka leo Wabunge niwaambie tukubaliane kwenye hili Bunge, anayemgusa Rais wetu, anayegusa taasisi inayoitwa Ikulu huyo ni adui wetu sisi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka tumwone Rais wetu akifanya kazi, akichapa kazi na akileta heshima ambayo ametuletea kwa miaka mitano na haruhusiwi mtu yeyote kumvuruga na kumwondoa, tunategemea makubwa kuliko haya kwa hii miaka mitano. Tunataka twende kwa huo mwelekeo aliokwenda kwa miaka minne, kama miaka minne amefanya makubwa hivi, tusubiri miaka mitano. Hakuna *destruction*, tusimame wote kwa pamoja, ni adui wetu sisi wote yeyote atakayetaka kumvuruga na kuigusa taasisi inayoitwa Ikulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, huyu ni mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu, tukirejea Saa 11 tutaendelea na Mheshimiwa *Engineer* Fadhili Sandali Chilombe, Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mheshimiwa Lucy Edward Mwakyembe na tutaendelea na orodha jinsi ambavyo tutakuwa tunachangia.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema haya, basi ninasitisha shughuli za Bunge hadi Saa Kumi na Moja Jioni.

*(Saa 7.01 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Naibu Spika (Mhe. Daniel B. Sillo) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, tunaanza na Mheshimiwa *Engineer* Fadhili Sandali Chilombe, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Mustafa Kawamba, na Mheshimiwa Jonas William Mbunda ajiandae.

*(Hapa Microphones zilizima kwa muda mfupi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa tuendelee.

**MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE**: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Nishati alikuwa anasema taa ziliwaka ili kuonesha kwamba, majimbo yote yana umeme, ndiyo maana ziliwaka zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na kuwa mchangiaji wa kwanza jioni ya leo. Mimi ni Mbunge, anayetoka kwenye maeneo ambayo...

*(Hapa microphones zilizima kwa muda mfupi)*

**MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE:** Mheshimiwa Ado, hebu niachie basi! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitunzie muda wangu, maana naona Ado anafanya vitu vyake hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetoka kusema kwamba mimi ni Mbunge anayetoka kwenye maeneo ambayo hayajaunganishwa na Gridi ya Taifa, lakini Serikali inafanya jitihada kubwa na tayari kazi imeshaanza kule. Katika kipengele hiki ninaomba nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uthubutu wake wa kuamua kutuondoa watu wa Kusini katika hali ile tuliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi Wabunge wenzangu wanaotoka Kusini walisema na wameipongeza Serikali pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, nami niungane na Mheshimiwa Waziri. Wakati tunaanza Bunge hili, mradi ule unaojengwa kule Tunduru na maeneo mengine ulikuwa umekwama kwa sababu ya changamoto ya malipo; lakini Waziri alikuja akafanya ziara, akapambana na mkandarasi na wakati huo akapambana na upande wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri akamwendea Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Rais alimwelewa; zikatoka fedha kwa mara ya kwanza shilingi bilioni 30. Hivi karibuni tena zimetoka shilingi bilioni tatu na kufanya jumla ya fedha zilizolipwa katika kipindi hiki kisichozidi wiki mbili kuwa shilingi bilioni 33. Hiyo ni dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi ule mpaka hivi tunavyoongea kwenye kile kipande cha Tunduru–Songea, ambacho kinahusisha ujenzi wa *line* ya kilometa 214 na ujenzi wa *substation* wa *megawatt* 120 ndani ya Mji wa Tunduru kinagharimu shilingi bilioni 150.7. Kati ya hizo kama nilivyosema shilingi bilioni 55.7 zimekwishalipwa tayari. Unaweza ukaona ni kwa namna gani Mheshimiwa Rais, amejipanga na amedhamiria kuhakikisha kwamba jambo hili linafikia mwisho wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, ninaomba nishauri; lakini kabla sijashauri, ninaomba nianze kwa kuunga mkono hoja, nisije nikasahau, kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati, kwa hiyo nina *interest* huko. Ninaunga mkono hoja ili niweze kuchangia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nishauri mambo mawili kama muda utaniruhusu. Jambo la kwanza, ukiangalia taarifa, taarifa zinaonesha hivi, mwaka 2010 *line* ya msongo wa *kilovolt* 33, nchi nzima ilikuwa ni kati ya kilometa 10,000 hadi 12,000 nchi nzima. Ilipofika 2015 *lines* hizi ziliongezeka zikafika kilometa kumi na

saba elfu na ishirini na moja. Ilipofika 2020, *lines* hizi ziliongezeka zikafika kati ya kilometa 35 mpaka 40.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunavyozungumza ukiangalia ripoti ya Mheshimiwa Waziri anasema kwamba line za msongo wa *kilovolt* 33 nchi hii zipo themaini na tatu elfu, mia tatu tisini na moja nukta tatu mbili. Hii maana yake ni nini? Serikali imefanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha kwamba umeme unasambaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa lipo tatizo hapa ambalo ndilo ninalolilenga kulishauri, ambalo *TANESCO* wanatakiwa wanisikilize na ikiwezekana walichukue wakalifanyie kazi. Njia wanayoitumia *TANESCO* kutafuta tatizo umeme unapokatika imepitwa na wakati. Kinachotokea ni kwamba, umeme ukikatika wanaunda timu zinakwenda kufanya kitu kinaitwa *line patrol*.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri ni kwamba *technology* iliyopo toka mwanzo umeme ukikatika huwa inaeleza kwamba hapa umekatika kwa sababu aidha kuna *over current* ama kuna *earth fault* na vitu vya namna hiyo. Hata hivyo, kujua kwamba sasa tatizo hili lipo wapi huwa halijulikani. Kinachofanyika ni watu kumwagwa kwenye *line* kuanza kutembea hatua kwa hatua, nguzo kwa nguzo kutafuta tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhara yake ni kwamba tatizo likitokea linachukua muda mrefu mno kutatuliwa; lakini jambo la pili ni *risk* hata kwa wale wafanyakazi. Njia hii ilikuwa inafaa wakati ule ambapo *line* zilikuwa na urefu labda wa kilometa 50 au kilometa 60 kutoka kwenye *source*. Sasa hivi zipo *line* zina urefu wa kilometa 1,000 na zaidi. Tukitumia njia hii tutakuwa tunaendelea kupoteza muda na mapato mengi kwa shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu, *TANESCO* waanze ku-*digital* hizi *lines*. Zipo *technology* zinazoonesha kwamba tatizo likitokea lipo mahali fulani au lipo umbali fulani kutoka hapo *substation* ilipo. Kwa hiyo ili ku-*maximize profit* na kuhakikisha kwamba hatupotezi *revenue* na kuleta *disturbance* nyingi kwa wateja, niwaombe *TANESCO* wafikirie uwezekano wa ku-*digital* hizi *lines* kwa sababu *technology* inataka hivyo. Huo ni ushauri wangu wa kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wa pili, ninataka niungane na Profesa Muhongo na dada yangu pale, ninamsahau huyu; alisema kuhusiana na *issue* ya uzalishaji wa umeme hapa asubuhi. Kwamba hivi; ukisoma taarifa ya Waziri inasema hivi leo Tanzania uwezo wetu wa kuzalisha umefikia *megawatt* 4,522.54; hiyo ndiyo taarifa ya Mheshimiwa Waziri inavyosema. Ameenda mbali zaidi, akachambua, kwenye ukurasa wa 15 wa taarifa yake. Anasema, 60.3% ya ule umeme unatokana na maji, asilimia 1.44 unatokana na jua.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii kila mtu; Mbunge, mwananchi, kiongozi tume *relax* kwamba tuna umeme wa kutosha na ni sahihi tuna umeme wa kutosha; lakini umeme ulipotulia matumizi nayo yamepanda. Shida ninayoiona, kwa kuwa *base load* yetu sisi, matumaini yetu makubwa yapo kwenye umeme wa maji. Tafsiri yake ni kwamba siku ambayo mvua itaacha kunyesha tutarudi kwenye *crisis* ile ile; na safari hii itakuwa mbaya zaidi kuliko wakati mwingine wowote kwa sababu matumizi yamepanda sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mtu anajua, ukiachilia mbali tafiti, kila mtu anafahamu kwamba ukiona hakuna mvua maana yake kuna jua. Ushauri wangu, Serikali iweke msisitizo mkubwa sana kwenye chanzo cha *solar* kuliko chanzo kingine chochote. Ninaposema Waziri aweke msisitizo yapo mambo mawili ninashauri yafanyike. Moja, kuongeza *speed* ya uwekezaji unaofanywa na Serikali kwenye *angle* hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafahamu kwamba ipo miradi inaendelea na tafiti zipo. Tafiti zinaonesha kwamba nchi hii kwa mwaka tunaona jua kati ya masaa 2,800 hadi 3,500 kwa mwaka mzima. Niliwahi kusema hapa, Ujerumani wanaona 1,400 hadi 1,800 lakini wanazalisha umeme *megawatt* 38 *point,* mara karibu tisa ya umeme tulionao sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuna uwezo wa kuona jua kati ya masaa 2,800 hadi 35. Kwa hiyo ningeomba Serikali iweke msisitizo kwenye *angle* hiyo. Katika kuweka msisitizo iongeze *speed* kama nilivyosema na tuanze utaratibu wa ku-*sensitize* matumizi ya *solar* kwenye nyumba ya watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano, nina-*declare interest,* mimi nina shamba ninalima kule, ninamwagilia kwa *solar.* Nyumba ya shambani nimeezeka *solar*, ile *solar* ni *roofing material,* lakini pia inazalisha na umeme kwa ajili ya kufanya shughuli za kazi yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano mdogo tu. Wote hapa tumepanda *SGR*. Ukienda Morogoro kuna lile jengo linaitwa Jakaya Mrisho Kikwete, wale watu kwa mwezi wanatumia *unit* 58,000 hadi 59,000 katikati, *average* yao hiyo; wanalipa umeme shilingi milioni 11 hadi milioni 12 kila mwezi. Jengo lile ukiliangalia kwa urefu linaweza likafika mita 100, upana linaenda kati ya mita 25 hadi 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri yake ni kwamba *surface area* kule juu inaanzia *metre square* 2,500 au 3,500 au 3,000. Maana yake ni kwamba, lile jengo likiwekwa *roofing material* za *solar* tutapata *unit* kuanzia 72 elfu hadi 100,068, kitu ambacho kitawafanya wale watumie umeme ule pale wa-*save* na gharama. Hivi vitu vinatakiwa Serikali i-*sensitize;* na watu pekee wa kuwakabidhi kazi hii ni *REA* kwa sababu *REA* wana uwezo wa kuanzisha hii kitu wakafika mwisho wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ninaenda kumaliza mchango wangu, ninaomba nitoe pongezi kwa watu wachache. Kwanza Mheshimiwa Waziri, tumekwishasema na wengi wamempongeza, kwa hiyo sitaki nirudie sana. Ninaomba nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, *Eng*. Mramba.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Eng*. Mramba, ni zaidi ya Katibu. Ninasema hivyo kwa sababu 95% ya wafanyakazi wa *TANESCO* mnaowaona nchi hii wametoka mikononi mwa Mramba. Yule mtu ameanza akiwa *Engineer* mdogo hadi akafikia *level* hiyo; na ndiyo maana unaona tasnia hii inakwenda vizuri kwa sababu yake, anaujua umeme kupita watu wanavyofahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu mwingine Mkurugenzi wa *TANESCO*, *Engineer* wa bandia Mheshimiwa Twange, ninamwita *Engineer* wa bandia kwa sababu yeye sio *Engineer*...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja, naona kengele imelia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, mchango wa kiuhandisi nimeusikia.

Mheshimiwa Juma Mustafa Kawamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Jonas William Mbunda na Mheshimiwa Lucy Edward Mwakyembe ajiandae.

**MHE. JUMA M. KAWAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ninashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia mimi na Waheshimiwa Wabunge wote kuhudhuria kikao hiki cha Bunge jioni hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda nimpongeze na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, jemedali na mzalendo wa kwanza wa Taifa hili kwa kazi nzuri ambazo anaendelea kuzifanya ndani ya sekta hii ya nishati nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niipongeze Serikali kupitia Wizara ya Nishati kwa kazi nzuri ambazo wanafanya. Waheshimiwa Wabunge wote wamesimama hapa kila mmoja anatoa ushuhuda kwa mambo mazuri ambayo Wizara hii wanaendelea kuyafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaziona jitihada za Serikali kwenye kuhakikisha kwamba tunapata umeme wa uhakika nchini. Hadi kufikia Machi, 2026, nchi yetu iliweza kuzalisha megawati 4,222.54 kutoka megawati 4,031.71; tunaona ni jinsi gani ongezeko la 12.17% zimeongezeka ndani ya gridi ya Taifa ya nchi yetu. Hii inaonesha kwamba Serikali imeendelea kuwekeza kwenye nishati ya umeme nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona Serikali imeendelea kuwekeza kwenye suala la miundombinu. Hadi kufikia Februari, 2026 vitongoji 39,003 vilikuwa vimeunganishwa na umeme ndani ya nchi hii, ni sawasawa na 61%. Jitihada hizi tunaona ni jinsi gani Serikali ilivyojikita kwenye kuhakikisha tunapata umeme wa uhakika nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio haya, lakini ndani ya Jimbo langu la Igalula bado kuna changamoto zifuatazo. Tunaona kazi nzuri ambazo wanaendelea kuzifanya watu wa *REA* nchini, lakini ndani ya Jimbo langu la Igalula bado kuna changamoto. Kuna baadhi ya vijiji na vitongoji havijafikiwa na umeme kikamilifu. Kwenye mpango huu wa Serikali 2026/2027...

*(Hapa Microphone Ilizima kwa Muda Mfupi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, endelea.

**MHE. JUMA M. KAWAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Jimbo langu la Igalula bado tuna changamoto ya upatikanaji wa umeme kikamilifu vijijini na kwenye vitongoji. Katika bajeti hii ya Serikali Mwaka wa Fedha 2026/2027, ndani ya Jimbo langu la Igalula nimepata vitongoji 48 tu kati ya vitongoji 140 ambavyo bado havijafikiwa na umeme huu wa *REA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Wizara kwa sababu Mama amesema Watanzania tunatakiwa tupate tabasamu na sisi wananchi wa Jimbo la Igalula tumeshaanza kupata tabasamu. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri kupitia Wizara yake hii ya Nishati, atuongezee basi kutoka hivyo vitongoji 48 walau na sisi tufikie vitongoji 80 tuanze kulifaidi tabasamu la Mama kupitia Wizara ya Nishati kama vile ambavyo tunaendelea kufaidi kupitia Wizara nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kukatikakatika kwa umeme bado ni changamoto kubwa sana ndani ya Jimbo la Igalula, kuna changamoto kubwa ya kukatika kwa umeme ndani ya Jimbo la Igalula hasa kwenye maeneo ya vijijini na kwenye vitongoji licha ya uwepo wa umeme wa uhakika wa megawati

45,220.54, lakini ndani ya Jimbo la Igalula bado tumekuwa na changamoto ya kukatikakatika kwa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inatokana na *line* yetu ya Halmashauri yetu ya Wilaya ya Uyui kuwa ni ndefu. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali kupitia Wizara ya Nishati itufungie *switching station* katika Kijiji cha Mpumbuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii *switching station* itasaidia kuweka utofauti wa umeme huo unaweza kwenda kwenye Kata tatu. Ina maana Kata ya Loya iwe inaweza kujitegemea, Kata ya Tura iwe inaweza kujitegemea na Kata nyingine ambazo zinashabihiana nazo, lakini kwenye Kata ya Goweko na yenyewe iwe inaweza kujitegemea kwenye kata ambazo inashabihiana nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninaomba nichangie kwenye suala la nishati safi. Wakazi wangu wa Jimbo la Igalula 96% wengi tunatumia kuni na mkaa, licha ya kuathirika kiafya, lakini suala hili linaathiri sana hali ya kuchafua mazingira na kuharibu mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali iongeze bidii ya kusambaza nishati safi hasa vijijini, ikiwa sambamba imeambatana na kutuletea majiko banifu na gesi zenye bei nafuu ili tuhakikishe wananchi wangu wa Igalula wanafaidika na majiko haya banifu na gesi za bei nafuu waweze kutumia kwenye maisha yao ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, athari za kupikia mkaa na kuni, moja ya malengo ya Wizara nimeangalia kwenye randama yao wanasema ni kupambana na magonjwa yasiyoambukiza. Sasa watu kwa kupikia huu mkaa na kuni wengi wanapata magonjwa ya mfumo wa hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninawaomba Wizara kama vile kwenye mipango yenu ya ndani ya Wizara kupambana na magonjwa yasiyoambukiza, tunaomba na sisi sasa vijijini watulete majiko banifu yenye bei nafuu na gesi zenye bei nafuu ili

kuweza kuwaokoa wananchi hawa ambao wanapikia majiko ya mkaa na kuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichangie suala la mafuta nchini. Wote tunakubaliana suala hili ni tatizo la kidunia, halijatokea Tanzania tu bali limetokea dunia nzima na haya ni kutokana na mapigano ambayo yanaendelea kwenye hizo nchi za wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nishauri kwenye suala hili tuweze kurejea mawazo ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliyoyafikiria mwaka 1960 mpaka mwaka 1966 kwa ajili ya kuweza kujikwamua kiuchumi ndani ya Taifa letu, alifikiria kuhusu suala la *TIPER.* Kampuni hii ilikuwa ni muunganiko kati ya Tanzania na Nchi ya Italy. Baba wa Taifa wa nchi hii alikuwa na mawazo Taifa letu hili la Tanzania tuweze kuzalisha mafuta yetu wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunaona Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Hayati Mheshimiwa John Joseph Pombe Magufuli kulikuwa na tatizo la umeme hivi hivi nchini, lakini kwa mawazo mazuri ya Hayati Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan walikaa pamoja wakafikiria ndiyo maana leo tunaona Bwawa la Mwalimu Julius Kambarage Nyerere limetokea na limekwenda kumaliza kabisa shida ya umeme nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninashauri kama Wizara waweze kwenda kuyarejea maono ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambayo aliyawaza mwaka 1960 kwa ajili ya kupambana na kuhakikisha kwamba sisi kama Taifa tunakuwa na mafuta yetu hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu namba mbili tuhakikishe kwamba tunatengeneza mpango mkakati wa kuhifadhi mafuta ndani ya nchi walau uwe na muda walau wa mwaka mmoja wanaita *petroleum reserving strategy.* Tuwe na mpango mkakati wa kuhifadhi mafuta walau ndani ya mwaka mmoja. Siyo wa sasa hivi, *reserve* yetu ya mafuta inaonekana ni ya miezi mitatu tu. Sisi kama Taifa inabidi tubadilike sasa tuwe na

*reserve* ya mafuta ya kuanzia walau ndani ya mwaka mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nishauri Wizara ya Nishati waje sasa na mpango mkakati kwa sababu tunajua mafuta yakipanda bei na vitu vingine na vyenyewe vinapanda bei. Tunajua sasa hivi maisha ya wananchi pia kwenye bidhaa nyingine yamepanda. Sasa kama Wizara ya Nishati ishirikiane na Wizara ya Fedha kuhakikisha tunapunguza athari za kupanda kwa bidhaa nyingine kutokana na hizi athari za kupanda kwa mafuta nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge, kwa mchango wako. Mheshimiwa Jonas William Mbunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Edward Mwakyembe, Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, ajiandae.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika bajeti ya Nishati. Nianze na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na kunipa nafasi ya kuchangia leo katika bajeti ya nishati, lakini pia kabla sijasema chochote niseme kwamba, ninaunga mkono hoja kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati hii ya Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyojitahidi kusimamia katika sekta hii ya nishati na kutoa fedha nyingi na kujenga miradi mbalimbali kwa ajili ya kusaidia kuzalisha umeme na shughuli nyingine zinazohusiana na nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na upande wa kuangalia majukumu ya Wizara ya Nishati hasa *TANESCO.* Jukumu la *TANESCO* ni kuhakikisha kwamba wanazalisha umeme, wanasafirisha na wanasambaza. Ninaomba katika maeneo haya

nianze na kumshukuru Mheshimiwa Deo Ndejembi, pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Salome Makamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru pia Makatibu Wakuu *Engineer* Mramba na Dkt. Mataragio pamoja na wasaidizi wao wote ma-*CEOS* kwenye sekta mbalimbali kwa jinsi wanavyojitahidi kufanya kazi vizuri na kusimamia kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata umeme wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukiangalia katika majukumu ya *TANESCO* jukumu la uzalishaji tunaona kabisa sasa hivi kwenye uzalishaji kulingana na taarifa ya Mheshimiwa Waziri tumefikia megawati 4,522, lakini ukienda kwenye matumizi tumefikia megawati 2,199. Ukiangalia kwa ujumla unaona kabisa kwamba kuna ziada ya umeme ambao tunaona upo kulingana na vyanzo vyetu vya uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiingia kwa undani zaidi ukafanya uchambuzi unaona kabisa kwamba ziada hiyo imetokana na kutokuwa na uwezo mkubwa wa kusafirisha umeme na kugawa kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika eneo hili la uzalishaji na matumizi, ninaomba niishauri Wizara, niishauri Serikali iendelee kuongeza nguvu na jitihada za kusafirisha umeme na kugawa katika maeneo mbalimbali kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye upande wa uzalishaji kulingana na taarifa ya Waziri ukurasa wa 13 umeonesha vyanzo mbalimbali vinavyotusaidia sisi kuzalisha umeme. Ukiangalia chanzo cha maji tunazalisha 60%, gesi asilia 31.28%, mafuta 1.28%, tungamo taka 3.31%, upepo 0.08%, jua 1.70%, makaa ya mawe 1.95% lakini jotoardhi hatujazalisha chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwa undani kuna umuhimu mkubwa wa Serikali kufanya jitihada ya kuhakikisha kwamba tunazalisha umeme kupitia gesi asilia, lakini kupitia upepo, jua, makaa ya mawe na jotoardhi. Ninasema hivi kwa

sababu ni vitu ambavyo tunavyo na tumepata neema hizi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mara ya mwisho Mheshimiwa Waziri anakumbuka tulienda kwa ndugu zangu watani zangu Kishapu. Mimi nilifika pale niliona, sisi tumezoea kulima mahindi, tunasema mashamba ya mahindi na mashamba ya kahawa, lakini tulipoenda Kishapu tuliambiwa kuna mashamba ya *solar,* zimesambazwa *solar* na zimewekwa kabisa kuna mashamba matatu; shamba la kwanza, shamba la pili na shamba la tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niiombe Serikali iendelee kuongeza nguvu na jitihada ya kuzalisha umeme kupitia hivi vyanzo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Kishapu kwa sababu tuliona mpango wao, ni kuhakikisha kwamba wanazalisha megawati 150, megawati 50 zimezalishwa zimeingizwa kwenye gridi ya Taifa, lakini tuiombe Serikali ikaendelee kuzalisha megawati 100 ambazo ziko kwenye mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya msingi hapa ni tutumie vyanzo vilivyopo katika maeneo yetu ambavyo tukianza kuzalisha umeme vitatupa umeme wa kutosha na tutaendelea kuwa na umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hoja ya mafuta wenzangu wengi wameongea; kwanza, kuna changamoto ya upandaji wa bei. Tuiombe Serikali kwa sababu janga hili ni janga la kidunia sisi tupeleke nguvu kwenye kuhakikisha kwamba kuna upatikanaji wa mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine changamoto hii tunaweza tukaiona kama ni changamoto lakini upande wa pili tunaweza tukaitumia kama fursa ya kuona kwamba sasa ni wakati sahihi wa kuhakikisha kwamba tunafanya utafiti wa kuvuna mafuta ya kwetu lakini tunaongeza nguvu ya kuendelea kugawa gesi *(CNG)* na kuhakikisha kwamba tunahakikisha kwamba tunapata umeme wa kutosha kupitia katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii imeunda kampuni tanzu nyingi, ukipiga hesabu zinafika karibu 10 na Ma-*CEO,* ninafikiri wapo, lakini niwapongeze kampuni tanzu zinafanya vizuri. Nimwombe Waziri, niiombe Serikali kwa kushirikiana na Msajili wa Hazina waendelee kusimamia kuhakikisha kwamba makampuni haya yanafanya kazi vizuri ambayo inaleta tija kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niingie sasa kwa wananchi wa Jimbo langu la Mbinga Mjini waliniagiza kwamba ukipata nafasi ya kuongea kwenye Wizara ya Nishati, kuna mambo ya msingi ya kusema.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, katika Jimbo la Mbinga Mjini linapokea umeme kutoka Songea. Umeme unasafirishwa kutoka Songea mpaka Mbinga hadi Nyasa. Kwa umbali ule wananchi wale wameniambia mpango wa Serikali ambao ulikuwepo wa kujenga kituo cha kupoza umeme pale Mbinga, niiombe Serikali iweke kipaumbele ihakikishe kwamba kituo kile kinajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali ya sasa hivi kuna mazingira ya kukatikakatika kwa umeme kwa Mji wa Mbinga Mjini. Kwa hiyo, niiombe Serikali kupitia kampuni yetu ya *TANESCO* iweke uimarishaji wa miundombinu na kuhakikisha kwamba wananchi wale wanapata umeme kwa wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, niseme kwamba tunampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa kinara na mwanzilishi wa nishati safi. Nimeona maeneo mbalimbali wenzetu wameanza kufurahia hiyo fursa, kuna shule za sekondari, kuna maeneo na taasisi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe sisi Mbinga tunazalisha makaa ya mawe tuna uhakika wa kupata mkaa unaotokana na makaa ya mawe. Kwa hiyo, niiombe Serikali kupitia *REA* waanze kupeleka umeme, kupeleka nishati mbadala katika Shule ya Sekondari ya Makita, lakini pia kuna vituo vyetu vya Magereza ya Mkwaya na Gereza la pale Mbinga Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache ambayo nimeongea, ninaomba niunge mkono hoja na niendelee kuwapongeza sana wenzetu wa Wizara ya Nishati. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge. Mheshimiwa Lucy Edward Mwakyembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza na Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, ajiandae.

**MHE. LUCY EDWARD MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuongea kwenye hoja iliyowasilishwa mezani ya Wizara ya Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati ndugu yangu Mheshimiwa Ndejembi, lakini pia Naibu Waziri wa Nishati ndugu yangu Mheshimiwa Salome Makamba pamoja na Menejimenti yote ya Wizara ya Nishati. Kazi yao ni nzuri na wasilisho lao ni nzuri. Kwa kweli nikiamini Wabunge wote humu ndani wamefurahia kazi nzuri ambayo wameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maeneo matatu ya kuchangia, lakini maeneo mawili nitawasilisha kwa maandishi. Eneo moja kwa jioni hii ndiyo nitakaloweza kuliwasilisha. Eneo ambalo nitapenda kuchangia ni habari ya nishati safi ya kupikia. Kwenye upande wa nishati safi ya kupikia eneo hili ni muhimu sana na eneo hili nimeona nishati hizi zinahamasishwa sana kwa wanawake, ikiwemo wanawake wa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wa vijiji, nimeona bado hawajapata elimu ya kutosha kwa ajili ya kutumia nishati hii safi ya kupikia. Tumepeleka majiko ya nishati safi kwa kupikia, majiko ya gesi, lakini pia majiko yenye kutumia mkaa maalum wa nishati safi, ila eneo hilo bado wananchi hawajaelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ushauri kwenye upande huo, kama itaonekana inafaa, kwenye Wizara ya Nishati ikiongozwa na ndugu yangu Mheshimiwa Ndejembi, kuwa mpango huu ukiwezekana wa kuhakikisha elimu hii inawafikia wananchi au wanawake waliopo kule vijijini pamoja na familia kuandaa mkakati maalum wa kuweza kuwafikia wanawake hawa. Na

mkakati huo kama itawezekana ungepangwa maalum kuufikisha kwa kutumia viongozi wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Viongozi hao ninaamini wanaongozwa na Mama yetu Mary Pius Chatanda, ambaye ni Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania. Viongozi wanawake hao wakiwemo na sisi Wabunge humu ndani ili kuifikisha elimu ile na wananchi wale kuweza kufikia malengo ya kutumia nishati ile iliyo safi na salama kwa kupikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishati hii ipo kule vijijini lakini shida iliyokuwepo mawakala wapo. Hawa wanawake wamefikishiwa majiko ya gesi kwa ajili ya kutumia kule, mtungi ule wa gesi alipoupata mara moja tu, mwanamke yule hajawahi kuupata tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale wanaotumia ile mitungi ya gesi ni watu ambao wanajielewa. Pia walengwa ambao wamewekewa hii nishati safi ya kupikia wanakuwa hawaelewi, ametumia mtungi wake mmoja, ameumaliza, hakuweza tena kununua, lakini kungekuwa na timu ambayo ingeweza kuwahamasisha kata kwa kata wakaweza kutumia nishati hii, ninafikiri ingewezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini ninazungumza hivi? Ninazungumza hivi kwa sababu, hapa kulikuwa na mikopo ile ya 10% ambayo ilikuja ikasitishwa na Serikali. Wananchi wengi wakawa wamelalamika hususan huko vijijini, hawaelewi nini kinachoendelea. Vijana wanalalamika, wanawake wanalalamika, watu wenye mahitaji maalum wanalalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mama yetu Mheshimiwa Mary Pius Chatanda aliweka mkakati na kuliandaa jeshi lake pamoja na Kamati yake ya Utekelezaji kupita kwa wanawake kata kwa kata kwenda kuwaelimisha ni kitu gani kilichosababisha 10% ikashindwa kuendelea kutolewa na waliambiwa kuwa ikifika mwezi Julai, hii 10% itatoka na kweli muda ambao aliwahakikishia wanawake wale, vijana wale, pamoja na watu wale wenye mahitaji maalum, muda ulipofika waliona kweli mikopo imetoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzoni hawakuelewa, waliona Serikali imezuia mikopo na hawakujua ile mikopo imezuiwa kwa sababu gani. Baadaye tulikuja kwenye kipindi cha uchaguzi. kwenye kipindi cha uchaguzi Mheshimiwa mama Chatanda pamoja na Makamu wake Zainab Shomari kwa kule Zanzibar, walihakikisha wanawake 18,000,000 wa Kitanzania ambao wamefikisha umri wa kupiga kura wanafikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, walipanga mkakati ule kwa kweli jamani, wanawake wale 18,000,000 waliweza kufikiwa kwenye kujiandikisha daftari la kupiga kura pamoja na kwenda kupiga kura. Sasa mkakati huu Mheshimiwa Waziri ukitumika utatusaidia wanawake wa vijijini kwenda kuhakikisha kutumia nishati safi na salama. Sisi wanawake tuko, tutaendelea kujitoa kwa ajili ya kuelimisha kutumia nishati safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeyazungumza hayo kwa sababu nimeona kuwa mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa kinara wa nishati safi na salama. Alianzisha ajenda hii mwaka 2022, Novemba; akaibeba ajenda hii iwe ya Tanzania, lakini ikiwezekana iwe ya dunia na alihitaji kufikia wananchi 80%, ikifika mwaka 2034 wawe wanatumia nishati safi na salama hasa ya kupikia, maana yake nini? Kile nilichokishauri tukikitekeleza, basi 80% itakuwa ni rahisi sana kuifikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumemwona mwanamke jasiri huyu mama Samia, amepewa hata *degree* ya heshima ya *PhD*, ameipata kupitia chuo cha Jimbo lile la Nasarawa kule Nchini Nigeria hivi karibuni. Hata juzi tarehe 21 Aprili, 2026 alikuwa na kongamano la akina mama na akina baba lishe, wakampa tuzo ya nishati ya malkia; tuzo ya malkia wa heshima kwa ajili ya nishati safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi tunamuahidi mama Samia kama wanawake wa Tanzania, tutaendelea kumuunga mkono kuhakikisha wanawake wote wa vijijini wanaelewa na kuifahamu nishati safi na salama na ikiwezekana kabla ya kufikia mwaka 2034, basi 80% aliyoitaka iwe imepatikana. Hongera sana kwa mama Samia, sisi tuko nyuma yake na tutaendelea kuchapa

kazi na tutaendelea kuitetea Tanzania kwa ajili ya kutumia nishati safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nilimtaja Mheshimiwa Amjadi Ussi Salum Pondeza, atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani na Mheshimiwa Mariam Anzuruni Mungula ajiandae.

**MHE. AMJADI USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo nami niwe miongoni mwa wachangiaji wa Bajeti hii ya Wizara ya Nishati ambayo kwanza naomba ni-*declare interest,* ni Mjumbe wa Kamati hii ya Nishati. Kwa hiyo naunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipo hapa nataka nizungumze jambo moja tu; kwanza, napenda nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu wetu Mkuu, Wakurugenzi wa *TANESCO*, *REA*, Mameneja wa *ITIPCO*, *TPCM*, kampuni zote tanzu ambazo ziko chini ya Wizara hii kwa jinsi ambavyo wanatoa ushirikiano kuhakikisha Wizara hii inafanya kazi vizuri na inafanya yale ambayo tunatarajia wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji wengi wameongea kila aina ya sekta wamepongeza, lakini ninataka niendelee kupongeza utendaji wao wa kazi. Hata hivyo, zaidi zaidi ninapenda nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kutoa fedha nyingi katika miradi ya maendeleo ambayo karibu 98% na vilevile Mheshimiwa Rais kuendeleza kampeni yake ya nishati safi na salama ambayo imekuwa ndiyo yeye kinara katika Bara letu la Afrika, lakini katika nchi yetu imekuwa mara nyingi anapenda kuifanyia mema sekta hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama ninataka nimwambie kitu Mheshimiwa Waziri, lakini ninasubiri amalize…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa endelea.

**MHE. AMJADI USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa, ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri ni mmoja tu ambao nimesimama kwa ajili ya kumpa yeye, Wizara pamoja na watendaji wote wa wizara hii ya nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nizungumzie Mradi wa Umeme Jua ambao uko kule Kishapu unaozalishwa, lengo ni kuzalisha *megawatts* 150, lakini sasa hivi tunaweza kuzalisha *megawatts* 50 ambazo zinaingizwa moja kwa moja katika gridi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kiukweli ule mradi ni mzuri, mkubwa na ndiyo sasa hivi dunia inaelekea huko, maana jana tu nilikuwa ninatazama *channel* moja ya China, wenzetu wanashangilia miaka 200 ya kutokuzimika kwa umeme. Ninaamini na sisi tutakwenda tutashangilia japo miaka 20 chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Ndejembi na wasaidizi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba, umeme ule wa Kishapu unazalisha *megawatts* 50 sasa hivi na zinaingizwa moja kwa moja katika gridi ya Taifa. Kitu ambacho ni kizuri, lakini upande mmoja itakuwa si sawa. Pale tumeenda, kama Mjumbe wa Kamati kama nilivyo-*declare* mwanzo, lakini ule umeme unazalishwa bila kuhifadhiwa. Kwa hiyo, unazalishwa unaingizwa moja kwa moja katika gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba na ninapendekeza, umeme ule wakati tunazalisha mradi upo ndani ya zaidi ya 35% - 50% *megawatts* 50 zinaendelea. Ninaomba au ninapendekeza lazima ule umeme unaozalishwa uhifadhiwe na kuhifadhiwa maana yake ni kuhakikisha tunatafuta betri, ninajua ule mradi tumefadhiliwa na Serikali ya Ufaransa na *as part* ya 30% inatoa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini hiyo *battery bank* ilikuwa hamna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa tunapoelekea, tukiweza kuhifadhi kwa kutafuta betri au chanzo chochote kingine ambacho kitaweza kufanya tukaweza kupata betri za kuhifadhi umeme ule ambao unazalishwa pale Kishapu, basi ule umeme utaweza kuleta mapinduzi makubwa kanda ya ziwa lakini na

katika miradi mikubwa ikiwemo *SGR* yetu ambayo inaendelea upande huu wa kanda ya ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, ningependa kupendekeza jinsi tutakavyoenda katika bajeti ijayo. Kwa hiyo ninaunga mkono hoja. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Anzuruni Mungula na Mheshimiwa Emmanuel John Khambay ajiandae.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kibali hiki cha kuweza kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu tukiwa na afya njema. Kwa upekee kabisa niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayowafanyia Watanzania, kwa kazi kubwa anayowafanyia akina mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tumeona wenyewe alivyozindua kwenye majiko pale tulishuhudia na akavaa umama kabisa. Kwa hiyo, ni Rais wa kipekee kwa Watanzania; ninaomba tumpongeze sana Dkt. Samia Suluhu Hassan. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, lakini pia niwapongeze sana na watumishi wote wa *TANESCO* na *REA* hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vijana wanafanya kazi kubwa sana, ni vijana wanazunguka katika vijiji, vitongoji na maeneo mengi kubaini changamoto zote zilizopo kwa Watanzania hasa kwenye suala la umeme. Hongereni sana Mheshimiwa na Waziri kwa jinsi ulivyowalea vijana; mameneja ni wasikivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi pia kumpongeza sana Meneja wangu wa Halmashauri ya Ushetu, ndugu yangu George Magaba, amekuwa ni sehemu ya kuwasaidia sana na kuwasikiliza sana Wanaushetu, niwapongeze sana. Nimpongeze sana Naibu Waziri, amefanya kazi kubwa kwa muda mfupi, amezunguka sana kubaini changamoto za wananchi. Hongera kwao, wafanye kazi, wawasaidie Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa mradi mkuu wa umeme wa jua katika Halmashauri ya Ushetu ambao zaidi ya 11,500,000,000 zimewekwa pale, *megawatts* tano za umeme zinaenda kuwasaidia Watanzania na wananchi wa Ushetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu na Waziri ananisikia hapa; niliahidiwa kuwekewa Kituo cha Kupozea Umeme pale Nyamirangano. Ahadi sasa imechukua miaka mitatu. Ninaomba kupitia bajeti yao hii ambayo tunaenda kuipitisha, waende wakawatendee haki wananchi wa Ushetu. Umeme umeshakamilika, mradi umeshakamilika na juzi Naibu Waziri amefika amejionea mwenyewe kazi iliyofanyika vizuri, lakini hawakumaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamejenga na zahanati pale, Watanzania na Wanaushetu sasa watakwenda kuitumia. Ni mapenzi mema na mazuri sana ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa Watanzania. Nimepokea vijiji vyangu 112, vina umeme tayari vyote. Vitongoji vyangu ni 554, lakini vitongoji 285 tayari vina umeme na juzi wamenipa vitongoji 136; sasa kazi imebaki vitongoji 145, waje wamalizie wananchi wa Ushetu waweze kuona umeme wa kutosha na kumshukuru Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliomba sana suala la *transformer*, eneo la Ushetu hasa Mwabomba lina wachimbaji wengi, lina madini, nenda Kata ya Urowa lina wafugaji, lina wakulima wengi, lakini wengi wanajenga viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba *transformer* zinazoenda ziwe na nguvu, ziwe kubwa, zile ndogo ndogo wanashindwa, lakini zinalipuka na umeme unakosekana ndani karibu miezi mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuomba Mheshimiwa Waziri yupo hapa, wapeleke *transformer* kubwa kwa wananchi wetu hasa kwenye kata ambazo zinaonekana zina uwekezaji mkubwa ili makusanyo ya Serikali yaendelee kuwa makubwa kuingiza fedha nyingi Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana Mheshimiwa Waziri na kwa kweli niendelee kuwapongeza. Nenda Kata ya Burungwa *transformer* zile zinapasuka, Kata ya Urewe pale Bugomba A na Bugomba B pia nina kesi hizo za *transformer*. Kwa hiyo, ninaomba tu kwamba watuongeze *transformer* ziwe na uwezo mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliomba Mkoa wa ki-*TANESCO* Kahama, nililia sana na hili niendelee kuliomba leo mbele yenu. Kahama inahitaji Mkoa wa *TANESCO*. Hali ya Kahama Mheshimiwa Naibu Waziri amefika pale anashuhudia; makusanyo ya Kahama na halmashauri zake tatu kwa mwezi tunakusanya zaidi ya shilingi 7,370,000,000 kwa mwezi mmoja; kwa mwaka makusanyo yanaenda zaidi ya bilioni tisini.

Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi 90,000,000,000 zinakusanywa kwa muda wa mwaka mzima; kwa miaka mitatu zaidi ya shilingi karibu 280,000,000,000, lakini miundombinu ni mibovu, umeme unakatika kila mara, biashara za Watanzania katika halmashauri zetu tatu ni ya kusuasua. Kwa hiyo, sisi tumekuwa na biashara kubwa sana ya jenereta kuliko hata kulipia umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe, Kahama ina hadhi ya kuwa mkoa.  Nenda eneo la Dodoma, ni mashahidi hapa na ndiyo maana ninaongea kwa msisitizo kwa sababu, Naibu ni mashahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nenda eneo la Dodoma, kuna eneo linaitwa Dodoma pale Kahama, lina vijana wafanyabiashara waliowekeza zaidi ya 3,500 wako pale wametengewa eneo lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa changamoto inayowasumbua na kilio chao ni kukatikakatika kwa umeme, wanakula hasara mashine zinaungua. Kwa hiyo, niwaombe sana waje, afanye ziara Kahama, Mheshimiwa Waziri aje aione Kahama kwa macho.  Anapoona wafanyabiashara Kahama, zaidi ya benki 13 zipo Kahama, aende, hoteli kubwa kubwa akashuhudie zipo Kahama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kahama ni lango la wafanyabiashara kwa Nchi za Afrika Mashariki, zipo pale Kahama. Kwa siku Kahama inapitisha zaidi ya magari 300 yale makubwa makubwa na yale yanayolala pale ni ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, akituwekea Mkoa wa Ki-*TANESCO* mahali wanapokusanya shilingi 90,000,000,000 kwa mwaka, shilingi 280,000,000,000 kwa miaka mitatu, ukiweka umeme usiokatika Mheshimiwa Waziri atakusanya fedha kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niendelee kuishauri Serikali maeneo ambayo wana makusanyo makubwa hata kwenye vijiji vyetu, kwenye kata ambapo unaona kata hii ina makusanyo makubwa, wawekeze umeme wa kutosha usiokatikakatika, wakarabati miundombinu iwe imara.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ni la muhimu, tumewasha umeme katika maeneo mengi sana, lakini ningeomba Mheshimiwa Waziri, yeye ni mbunge mwenzetu, hebu watoe nafasi maeneo ambapo umeme umekamilika, Wabunge tukawashe wenyewe, tukamsemee Mheshimiwa Rais, kwa sababu tunapata taarifa tu umeme umeshawashwa Mbunge hajaonekana pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, nani ataisema siasa? Mbunge amekuja mwenyewe kuomba umeme hapa, Mbunge amekuja mwenyewe kuomba vitongoji vyake hapa, Mbunge amekuja mwenyewe kupitisha bajeti yake hapa. Sasa kama umeme umekamilika umefungwa vizuri kwa nini asiende Mbunge kwenda kuwasha?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha aweke vizuri hapa kwa Mameneja wa Mikoa na Wilaya, Wabunge tualikwe kuwasha umeme katika maeneo yetu, tukamsemee Mheshimiwa Rais, tushuhudie bajeti tuliyoipitisha katika Bunge letu hili; kwamba Wabunge tumewasha umeme katika maeneo yetu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri; lakini niendelee kumpa pongezi sana Mheshimiwa Rais, kazi wanayofanya Wizara ni kubwa, sisi tunawapongeza na tuko tayari kupitisha bajeti. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mariam Anzuruni Mungula atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Lukago Midimu na Mheshimiwa Emmanuel John Khambay ajiandae.

**MHE. MARIAM A. MUNGULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwenye bajeti ya Wizara hii ya Nishati ambayo mimi pia ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati ya Wizara hii ya Nishati. Ninaomba kuanza kwa kuipongeza Serikali kwa kuendelea kuimarisha uwezo wetu kama nchi wa upatikanaji wa nishati na kuendelea kuvumbua vyanzo vya nishati safi kwa sababu hii itasaidia sana katika kukuza uchumi wetu na kufikia malengo yetu ya Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2050.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Waziri wetu wa Nishati, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na viongozi wote wa taasisi zilizo chini ya Wizara hii ya Nishati. Sisi kama Wajumbe wa Kamati tulienda kutembelea miradi ya Nishati na Madini kwa kweli kazi inafanyika, wanafanya kazi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakumbuka Mheshimiwa Waziri aliongea kwenye Kamati, akasema kwamba mimi mwezi uliopita nina miezi minne baadhi ya wajumbe ambao ni wageni tukaanza kushangaa! Una miezi minne kweli au umekaa zaidi ya miezi minne kwenye hii Kamati. Sasa hapa juzi wakati anawasilisha na anaongea Mama yangu Mama Sita akarudia lile lile kwani huyu Waziri ana muda gani kwenye hii Kamati? Kwa hiyo, nimpongeze sana anafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuchangia katika maeneo mawili au eneo moja kuu la usambazaji wa nishati safi ya kupikia pamoja na gesi asilia. Kama tunavyofahamu Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kinara wa nishati safi ya kupikia na maono yake ni kwamba kama nchi ifikapo mwaka 2034 tufikie 80% ya kutumia nishati hii safi ya kupikia, ambapo

mwaka 2022 tulikuwa tupo kwenye matumizi asilimia sita na sasa hivi tupo kwenye 28% *point something. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya changamoto ambazo tunazipata kwenye matumizi ya nishati safi au usambazaji, inaonekana ni *capital* au kile kianzio, bajeti imekuwa kubwa kwa wananchi kuweza kutumia kwa mfano, yale majiko jadidifu yanaitwa. Kwa hiyo, uwekezaji kule umekuwa kwa mwananchi mmoja mmoja, umekuwa ni mkubwa sana, unahitajika mkubwa sana. Sasa ninaomba kutoa mapendekezo kwa Wizara mambo ambayo tunaweza tukafanya yasaidie katika usambazaji wa hii nishati safi ya kupikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kushauri kwamba Wizara iangalie uwezekano wa kuendeleza, tayari inashirikiana na sekta binafsi, lakini tuangalie uwezekano wa kushirikiana zaidi na sekta binafsi katika kusambaza hii nishati safi ya kupikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, tuna shule hizi za *VETA* katika mikoa yote ya Tanzania. Kwa hiyo, tukianzisha ushirikiano na Wizara ya Elimu na tukapelekea kozi kule, vijana wetu wakajifunza kutengeneza kwa mfano haya majiko, hii itasaidia majiko yale yatakuwa tayari yapo kwenye kila mkoa *locally* na itasaidia vijana wale kupata ajira. Hili likifanyika kwa kupewa ruzuku itakuwa bora zaidi, vijana watahamasika kwenda kujiunga na kufanya hizo kozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba vilevile, kuishauri Wizara yetu ya Nishati na ya Madini ziendelee kushirikiana kwa karibu. Tayari zina ushirikiano na kuna taasisi kwa mfano ile ya *TAEC* ambayo inafanya kazi na wizara zote mbili, ya uhamasishaji wa matumizi ya nishati. Sasa hizi wizara zetu mbili zikishirikiana kwa karibu wataweza kupata mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, ile mikoa ambayo ina Wizara ya Madini imefungua viwanda vile vya makaa ya mawe na Wizara ya Nishati ikienda kupeleka viwanda vya kutengeneza haya majiko yakawa karibu karibu itasaidia katika usambazaji vilevile na kuongeza ajira na hii itasaidia katika kukuza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia kuchangia kwamba, Serikali sasa iwekeze zaidi kwenye kujenga hivi vituo vya *CNG* vya Gesi. Ninaomba kwenda kwenye gesi. Katika kujenga hivi vituo tuanze kujenga vituo kwenye hii barabara kubwa ambayo inatoka Dar es Salaam kuja Dodoma. Kwa hiyo, Mikoa ya Pwani, Morogoro na Dodoma yenyewe ifikiwe na vituo vingi zaidi, ambavyo vituo hivi vitasaidia au vitahamashisha madereva wengi kuweka nishati ya gesi au kuhamia kwenye nishati ya gesi kwenye magari yao. Vilevile, ninaomba kushauri ili tuoneshe mfano, Serikali iwekeze magari yake au vyombo vyake vya moto vianze kutumia hii nishati ya gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Dar es Salaam vilevile tuna lile Bomba la gesi la Kinyerezi ambalo tayari imeanza kusambaza gesi ile majumbani maeneo ya Sinza, Mikocheni na maeneo mengine ya Mkoa wa Dar es Salaam. Ninaomba kushauri kwamba, hapa pia Wizara ishirikiane na sekta binafsi katika usambazaji wa gesi hii kwa majumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kushauri Wizara yetu ya Nishati ichukue mfano Wizara yetu ya Madini ime-*ringfence,* imetenga kazi 20 ambazo zinatakiwa kufanyika na Watanzania tu. Sasa na Wizara yetu ya Nishati ikitenga baadhi ya majukumu au ikitenga baadhi ya kazi zikafanyika na Watanzania; Kwa mfano, kwenye huu usambazaji wa gesi na nishati safi, hii itasaidia kuongeza kipato cha Watanzania, lakini vilevile itasaidia katika kuharakisha kusambaza hii nishati safi ya kupikia na gesi asilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninaomba na sisi kama Wabunge (viongozi) tuwe mfano kwa sababu wengi pengine majumbani bado tunatumia mkaa na kuni. Kwa hiyo na sisi vilevile tukijitahidi kuhamia kwenye nishati safi ya kupikia, haya majiko jadidifu na makaa, tutakuwa mfano katika kuhakikisha kwamba na wananchi wanafuata na kutumia hii nishati safi ya kupikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, ninaomba kuunga mkono hoja na ninashukuru kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ester Lukago Midimu, utafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel John Khambay na Mheshimiwa Masanja Kungu Kadogosa ajiande.

**MHE. ESTER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Kwanza kabisa nimpongeze Waziri kwa hotuba nzuri iliyosheheni matumaini ya Watanzania. Mheshimiwa Waziri, hotuba yake ni nzuri sana. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanazofanya, Mwenyezi Mungu awabariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza pia Makatibu Wakuu wanafanya kazi nzuri sana. Mheshimiwa Deo anafanya kazi nzuri sana, kila sekta anayopelekwa ana-*fit*. Alikuwa ardhi amefanya kazi nzuri na sasa hivi anafanya kazi nzuri sana, tumeziona. Juzi changamoto ya mafuta imekuja hawajalala, anataka kuhakikisha wananchi wanapata mafuta na kweli vituo vyote vina mafuta. Hongera sana kwa Mheshimiwa Deo na Mheshimiwa Salome, wanachapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze vile vile Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Mheshimiwa Rais wengi hawakutegemea kwamba atajenga hilo Bwawa. Mama amejenga na limekamilika na sasa hivi tunapata umeme wa uhakika, hata kama ukikatika ni dakika moja umeme unarudi. Zamani umeme ulikuwa unakatikakatika, ukweli usiopingika Mama ameupiga mwingi, Watanzania hawatakaa wamsahau Mama yangu, jina lake litaandikwa kwa wino wa dhahabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kupeleka umeme vijijini; juzi juzi tumeshuhudia mikataba imesainiwa, mikataba 30 nzuri zaidi wakandarasi 21 ni wazawa, wakandarasi tisa ni wageni. Mheshimiwa Deo anawapenda wakandarasi wazawa anataka wawe mabilionea, ninampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Mkoa wa Simiyu kuna ujenzi unaendelea wa kituo cha kupooza umeme. Kituo hicho tunamshukuru Mheshimiwa Rais ametupatia shilingi 64,000,000,000. Kituo kinaendelea, kimefikia 47%, tunaomba sasa Serikali

wajitahidi kutafuta fedha, ili kiweze kukamilika hicho kituo. Pia, kuna Kituo cha Ibadakuli Shinyanga ujenzi unaendelea, hata *SGR* inategemea huo umeme. Tunaiomba Serikali iendelee kutafuta fedha, ili iweze kukamilisha hicho kituo kwa sababu hata sisi Wanasimiyu hicho kituo tunakitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa vijiji vyote vya Mkoa wa Simiyu, tumepata umeme. Pia, katika hii mikataba iliyosainiwa, Mkoa wa Simiyu tumepata vitongoji 415 tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. Mchanganuo wake wa hivyo vitongoji: Wilaya ya Bariadi Vitongoji 85, Wilaya ya Busega Vitongoji 53, Wilaya ya Itilima Vitongoji 52, Kisesa Vitongoji 53, Meatu 55, Maso Mashariki 36 na Maso Magharibi 39. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya Mheshimiwa Rais ni dhamira ya dhati Ifikapo 2030 vituo vyote nchi nzima vitakuwa vimepata umeme. Mheshimiwa Rais Mungu akubariki sana una malengo mazuri na Mungu amwongoze Mama aendelee kupata fedha aendelee kutuletea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Rais upande wa nishati safi ya kupikia. Mheshimiwa Rais amekuwa *champion* wa nishati safi ya kupikia. Hata juzi juzi tulimwona anagawa majiko, Mheshimiwa Rais anafanya kazi nzuri sana. Ni ukweli usiopingika, Mheshimiwa Rais tumemwona amegawa majiko magereza, kwenye taasisi mbalimbali na kwenye shule za sekondari, Mheshimiwa Rais amefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sasa hili zoezi liwe endelevu. Ninaiomba Wizara iendelee kutoa elimu kwa wananchi wetu kwa sababu, haya matumizi ya nishati safi hawajayajua zaidi. Mwingine anaweza kwenda kununua mtungi wa gesi, akipikia, gesi ikiisha anauweka pembeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba tuendelee kutoa elimu. Vilevile, wananchi wetu ambao wapo kwenye kata, mwingine anakuwa na nia nzuri ya dhati kabisa kwenda kununua gesi, anakosa sehemu ya kwenda kununua. Ninaomba tuzidi kutafuta

mawakala wengi wa kutosha, tuweke kila wilaya mawakala wa kuuza gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati, mengi wenzangu wameyasema, siwezi kuyarudia, ninaipongeza sana Serikali, Mwenyezi Mungu awabariki sana Mheshimiwa Salome pamoja na Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel John Khambay, atafuatiwa na Mheshimiwa Masanja Kungu Kadogosa na Mheshimiwa Salome Makamba ajiande.

**MHE. EMMANUEL J. KHAMBAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami niungane na wachangiaji wengine kuchangia katika Wizara yetu hii ya Nishati. Nitumie nafasi hii kumpongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuwa kinara katika suala zima la nishati safi na kuitangaza nchi yetu kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia kumpongeza Waziri wa Nishati, Ndugu yangu Deo na Naibu Waziri, Salome Makamba na wasaidizi wao wote walio chini yao kwa jitihada ambazo wameendelea kuzionesha katika kupambana na changamoto ambayo imejitokeza kutokana vita vinavyoendelea, ambapo imepelekea gharama ya mafuta kuongezeka duniani kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuwapongeza kwa jitihada ambazo wamefanya kwa kutumia Shirika letu la Maendeleo ya *Petroleum* likishirikiana na Wakala wa Uingizaji wa Mafuta kwa pamoja kwa lengo la ku-*control* uingizaji wa mafuta nchini. Tumeona hata katika mataifa mengine, meli zimegeuzia njiani kutokana na udalali ambao umefanyika katikati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, maamuzi ambayo wameyafanya ni maamuzi sahihi ili kuweza kuisaidia nchi yetu kuendelea kuwa na upatikanaji wa mafuta wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kutumia nafasi hii kuendelea kuipongeza Serikali chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada ambazo wameendelea kuzichukua katika kuhakikisha nishati ya umeme nchini inapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kutoa rai kwa dhamana ambayo wamepewa kama vijana wenzetu na tunaona kabisa viatu vinawatosha, waendelee kuchapa kazi. Sisi kama Wabunge tutaendelea kuungana nao, lakini tuone namna ya kuendelea kutumia nishati ya umeme na nishati ya gesi katika suala zima la magari. Ni Dhahiri kuna magari sasa yanaendelea kutumia nishati ya gesi, basi tuendelee kuboresha namna ya upatikanaji wa gesi na magari nchini yaendelee kutumia nishati ya gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hii imekuwa ni darasa, ninaamini kwamba tukijipanua na kujipambanua kwa kina na kuwekeza miundombinu sahihi katika suala zima la gesi, ni imani yangu hata wakati mwingine pakitokea changamoto hii ya mafuta, nchi yetu itaendelea kusonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niendelee kutumia nafasi hii pia kuishauri Serikali chini ya Wizara ya Nishati. Tuendelee kuboresha mfumo wa upatikanaji wa nishati safi kwa ajili ya kupikia, ili nishati hii iweze kuwasaidia Watanzania katika makazi yao. Utaratibu uliotumika na *TANESCO* wa kuuza umeme kwa njia ya *unit*, niungane na mchangiaji mwingine ambaye alichangia pia kuhusiana na kuweka utaratibu katika utumiaji wa gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiweza kuwekeza kama ambavyo maeneo mengine tayari mfumo wa gesi umepelekwa kwenye makazi ya wananchi; tukaweka utaratibu ambao utasaidia katika maeneo yote nchini hata tuanze *study* na maeneo ya miji, tupeleke gesi, tuweze kuweka utaratibu ambao Mtanzania wa chini, wa kati na wa juu aweze kununua gesi hata kwa mfumo wa *unit*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwekwe mfumo wa *unit,* ili nikitaka kutumia *unit,* labda ninataka kutumia gesi ya shilingi 5,000 au ya shilingi 3,000 kama ilivyo kwenye nishati ya

umeme, basi kuwe kuna *access* ya kuweza kutumia pia katika suala zima la gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini tukifikia hatua hiyo, tutakuwa tumelikomboa Taifa letu kwenye suala la nishati safi, ambapo Rais wetu ameonesha nia ya dhati kabisa katika kuhakikisha nishati safi inaendelea kutumiwa na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuishauri Serikali pia kupitia Wizara ya Nishati. Tumeona Mradi wa Mwalimu Nyerere umeendelea kufanya vizuri na changamoto ya umeme nchini inaendelea kwisha kutokana na uboreshaji wa Gridi ya Taifa ambao unaendelea. Ninaendelea kuipongeza Wizara ya Nishati. Nitumie nafasi hii kuwapongeza, lakini pia na Mkurugenzi Mkuu wa *TANESCO* Ndugu yetu Lazaro Jacob Twange. Ni mtu mnyenyekevu, binafsi nimewahi kufanya naye kazi. Ninaamini katika ushirikiano wake nao, watakwenda kuisaidia nchi yetu katika suala zima la nishati ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo basi, tumeona kuna namna nyingine tena ya upatikanaji wa umeme ambao unaweza ukasaidiana na umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Kwa mfano, umeme unaotokana na joto ardhi. Tumeona na tutaendelea kuipongeza taasisi ambayo ipo chini ya *TANESCO* kwa namna ambavyo imeendelea kufanya utafiti. Tumeendelea kuona maeneo ya Natron, maeneo ya Mbozi na maeneo mengine ambayo *almost* yanaenda kuwa kama saba, ambapo tunatazamia mpaka 2034 tupate *Megawatt* 130.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa kina ukifanyika tunaweza kwenda kupata na *almost Megawatt* 5,000. Kwa hiyo, umeme utakaotokana na *geothermal* utasaidia nchi yetu kusaidiana na Bwawa la Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Kwa hiyo, tuendelee kuongeza jitihada katika kupeleka fedha hizo huko ili utafiti uendelee kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu umeme wa joto ardhi ni *renewable energy*, tuta-*extract* yale maji, lile joto, yale maji tutayarudisha tena ardhini kwa hiyo, ni *renewable energy*. Kwa hiyo, ni umeme ambao utakuwa wa uhakika, hauharibu

mazingira wala haukwamishwi na kitu chochote, ni tofauti na umeme wa kutegemea upepo au wa kutegemea jua. Kwa hiyo, binafsi ninaishauri Serikali iwekeze nguvu kubwa kwenye umeme wa joto ardhi kwa sababu, ni umeme ambao ni wa uhakika na utaenda kusaidia Bwawa la Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, sasa ninarudi katika Jimbo langu la Babati Mjini. Ninaendelea kuipongeza Serikali kwa jitihada ambazo imeendelea kuzichukua kuhakikisha umeme unapatikana katika Jimbo la Babati Mjini. Katika vitongoji 54, vitongoji 48 tayari vina umeme, vitongoji sita vipo kwenye *progress,* tunaendelea. Hivyo basi, ninatoa rai kwa Wizara ya Nishati kupitia taasisi yetu ya *TANESCO* au *REA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni zuri, kuhakikisha wananchi wanaendelea kunufaika na huduma ya umeme, lakini huduma inakwenda polepole. Ninaomba katika hayo maeneo jitihada za dhati ziongezeke tuweze ku-*cover* hayo maeneo na maeneo mengine katika Jimbo la Babati Mjini, ambayo yanahitaji umeme jazilizi yaweze kushughulikiwa, umeme upatikane, ili wananchi wa Jimbo la Babati Mjini waendelee kupata tabasamu ambalo Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, analitaka kwa wananchi wote, hususani watu wangu wa Babati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo ninatumia nafasi hii tena kuendelea kuwapongeza, waendelee kuongeza jitihada. Sisi, kama vijana wenzao tupo nyuma yao tunaendelea kuwaunga mkono, waendelee kupambana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua changamoto ya mafuta wakati mwingine inawanyima usingizi, lakini kwa hatua ambazo tayari wamekwishakuzichukua tunaamini kwamba, tunakwenda kupata mafuta ya kutosha, mafuta ya miezi mitatu hayatoshi. Tuendelee ku-*focus* mbele kwa sababu, hatuwezi kujua vita itachukua muda gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufikia hapo ninashukuru na ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Masanja Kungu Kadogosa, atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Makamba na Mtoa Hoja ajiandae.

**MHE. MASANJA K. KADOGOSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa fursa ya kuzungumza katika Bunge hili Tukufu. Ninaanza kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri sana, hasa kwa mipango aliyonayo, ambayo ameweza kutuonesha kwenye hotuba yake. Vilevile ninampongeza dada yangu Mheshimiwa Salome kwa kazi nzuri anayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri vilevile tukampongeza Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan na wenzangu wamezungumza sana hapa, kwa ku-*champion* suala la nishati safi. Hili, kama wenzangu walivyozungumza, ni suala ambalo tutamkumbuka sana katika Taifa letu na kuanza kuzungumza na sisi watu wa vijijini kufikia huko, siyo tu kwa Tanzania bali kwa Afrika pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo la mazingira ambalo tumezungumza jana, ni muhimu sana kuhakikisha tunaanza ku-*shift* kwenye nishati safi. Vilevile tumpongeze Mheshimiwa Rais kwa ushupavu wake kuhakikisha kwamba, Bwawa la Mwalimu Nyerere limekwisha na kuanza kutoa umeme kwenye Gridi yetu ya Taifa. Kama Mheshimiwa Mbunge mmoja hapa alivyozungumza kwamba, wakati anaingia ninafikiri alikuta lile bwawa lipo kwenye sijui 37%, sijui 38%, lakini mpaka sasa tumemaliza na tunapata umeme. Kwa hiyo, hilo ni jambo la kiushujaa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwetu Bariadi Vijijini ni wafaidika wakubwa sana na sisi tunaiunga mkono hii bajeti kwa sababu, siyo tu kwa sababu tunaiunga mkono, lakini tuna sababu za kutosha; vijiji vyetu vyote 84 vinapata umeme. Vitongoji vyetu 211 mpaka sasa hivi vina umeme na tuna vitongoji vingine 85, wameanza miezi miwili iliyopita. Tuna vitongoji kama 216 ambavyo tunaamini kabisa, Mheshimiwa Waziri, mpaka kufikia 2028 tutakuwa tumemaliza vitongoji vyote, kwa hiyo, atakuwa amenihakikishia yale mambo kurudi tena; si ndiyo hivyo jamani!

*Yes,* kwa hiyo, ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Bariadi Vijijini tumepata majiko haya machache, ninaamini kuna *phase* nyingine inakuja. Ninasema machache kwa sababu, tuliyagombania kwa hiyo, ninaamini hata Wizara iko-*aware* na hilo. Sisi tumeji-*tune* tayari kwamba, *phase* ya pili tena tutagombania na wananchi wa Bariadi Vijijini wana munkari sana ya kupata haya majiko ili kubadilisha maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa lengo la miaka mitano ambayo tumejiwekea, Wizara itatakiwa ku-*double,* kwa maana umeme tunaoupata sasa hivi inabidi wa-*double* mara mbili. Kwa hiyo, ni lazima kuwe na mikakati ambayo tayari umeshaizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ni lazima kuwe na ufuatiliaji wa karibu sana kwa sababu, *obvious* tunapojiwekea malengo ya miaka 25, kwa maana ya Dira yetu ya Taifa 2050, tunahitaji kuwa na megawati kama tulivyozungumza wakati ule wa mpango siyo chini ya 70,000. Sasa maana yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kwamba, tukienda mwendo wa ku-*double,* kama tunavyofanya sasa hivi, tuna-*double* 2030, lakini 2035 tuna-*double,* mpaka tutakapofikia 2050 ndiyo tutaweza kufikia hilo lengo tulilojiwekea la Kitaifa. Kwa hiyo, anaweza akaona kwamba, Mheshimiwa Waziri, ana kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishati; kwa namna yoyote tunajua kwamba, tukifeli kwenye nishati Dira ya Taifa haitekelezeki kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ninafikiri wanapozungumza na watendaji, bahati nzuri ana watendaji wazuri sana, nimefanya nao kazi. Nikianza na *Engineer* Mramba, alikuwa Mkurugenzi mwenzangu huko nyuma, lakini vilevile nimefanya naye kazi wakati nipo kwenye *private sector.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Matarajiwa vilevile ni *Engineer* mzuri sana, *you have the best engineer*s katika nchi hii, Bwana

Mramba na Matarajiwa. Hata wakuu wako wa taasisi, Twange mwenyewe nimefanya naye kazi kwa zaidi ya miaka 10, *Engineer* Seif, *best engineer* kwa hiyo, Waziri ana vijana wazuri. Siyo vijana wengine, lakini ana wasaidizi wazuri sana katika Wizara, nina imani kwamba, ukifanya nao kazi kwa karibu haya malengo ya Kitaifa tutaweza kuyafikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hili suala la *REA*. Sasa kwa malengo ambayo tunajiwekea *obvious* mpaka 2030 tutakuwa tumeshafikia vijiji vyote. Sasa ni lazima tuanze kufikiria baada ya kufikia vijiji vyote, *REA* itabaki na kazi ipi au kazi yake, kadri tunavyofikia malengo, inazidi kubaki ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni yangu na kwa ushauri wangu, hii taasisi ina *knowledge* kubwa sana, yaani ile *accumulation* ya *knowledge* ni vizuri sana wakaanza kujitayarisha kwamba, baada ya hapo vitu gani wataongezewa kufanya katika hili Taifa. Isije ikawa wanapomaliza kupeleka umeme vijijini basi wakaonekana *redundant*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taasisi nyingine ambazo ninamshauri Mheshimiwa Waziri; kuna *Subsidiary Companies* za *TANESCO*, mojawapo ni ya kutengeneza nguzo za *concrete*. Sasa yale malengo ni mazuri sana kwa sababu, yanatuondoa kwenye kukata miti, tunakuja kwenye *concrete,* lakini hata ukiangalia *lifeline* ya zile nguzo za *concrete* inadumu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho ninashauri ni mambo mawili, la kwanza ni katika mikakati yao. Wajiwekee mikakati ya makusudi kuona kwamba, miaka 10 au 15 tunaondokana na utumiaji wa nguzo za miti. Hiyo ina maana gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, watakapokuwa na *commitment* hiyo katika Taifa kuna mambo matatu yatatokea; la kwanza ni, *funding* kwenye *financial institutions* zetu, ina-*shift* kwa sababu, watakuwa wanajua kwamba, sasa hivi Wizara ina-*focus* zaidi kutengeneza. Maana yake ni kwamba, *entrepreneur* sasa watataka kutengeneza viwanda vya kutengeneza *concrete poles.* Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni, *electric discipline* Serikalini. Tunajiwekea miaka mitano, tusifanye tu kwa kusema tunaenda, miaka 15, miaka 20, tutakavyoona sisi wenyewe tuwe tuna-*move* kwenda huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni ina-*create pressure*. Mambo makubwa hayawezi kutokea katika Taifa bila ya kuwa na *pressure* ya kulifanya, kwa hiyo, ninafikiri nimshauri Mheshimiwa Waziri hilo. Lile la mambo ya mafuta nimelizungumza, nisingependa kulirudia hapa; hata upande wa mafuta ninapenda kuona kwamba, kuna-*shift* magari yetu, lakini *public transport* zetu zikitumia gesi na umeme na hiyo miundombinu waanze kujiandaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ninaunga mkono hoja na ahsante sana kwa kunivumilia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Salome Makamba, Mheshimiwa Naibu Waziri na Mtoa hoja atafuata.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye hii Hotuba ya Wizara ya Nishati. Kwa heshima na taadhima kwanza kabisa ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uwezo wa kufika siku ya leo, ikiwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia, nikiwa kama Naibu Waziri wa Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli, ninatumia fursa hii kwa kuwa, ni mara ya kwanza kuchangia katika hili Bunge. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuniamini na kunipa hii dhamana ya kumsaidia Waziri wa Nishati, kama Naibu Waziri wake. Dhamana hii ni kubwa na ni deni kubwa kwangu na namuahidi nitatumia weledi, nguvu na maarifa yangu yote kuhakikisha tunasukuma mbele hili gurudumu la Wizara ya Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee ninamshukuru sana Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, amekuwa *mentor* wangu mzuri, amekuwa mwalimu wangu, amenipatia fursa ya kufanya kazi na kupata uzoefu

mkubwa ndani ya muda mdogo. Waheshimiwa Wabunge wenzangu watakuwa mashahidi, nimekuwa ninazunguka huko mikoani mpaka kuna wakati ninajiuliza, Mheshimiwa Waziri, ninaenda sawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, anasema, songa mbele tumsaidie Mheshimiwa Rais kuhakikisha Wizara ya Nishati inakwenda mbele. Ninamshukuru sana kaka yangu kwa wema huu na kwa sababu, amenifundisha vizuri. Ninaamini na mimi nitakuja kuwa mwalimu mzuri kwa wenzangu wengine watakaonifuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Shinyanga kwa kuniamini na kunirudisha Bungeni kama mwakilishi wao. Maneno huumba, nilisimama hapa nikiwa kwenye kiti kile pale, wanawake walisema ulichokisema kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tutakurudisha na leo ninasimama tena hapa. Kwa heshima kubwa ninawashukuru Wanawake wa Mkoa wa Shinyanga kwa kunirudisha hapa niendelee kuwatumikia katika huu upande wa Naibu Waziri wa Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi wamechangia kwenye hii Wizara, ninawashukuru sana kwa michango yao ya dhati. Ninataka niseme jambo moja, Wabunge hawa wanamtendea haki Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Rais wetu ndiye kinara wa nishati safi ya kupikia, Rais wetu amepewa tuzo kwa sababu ya nishati safi ya kupikia. Waheshimiwa Wabunge, hasa wa Chama Cha Mapinduzi, wamemtendea haki kwa kutaja mazuri aliyoyataja katika sekta ya nishati safi ya kupikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu mama yetu aliweka lengo ifikapo 2034 zaidi ya 80% ya Watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia. Lengo hili aliliweka mwaka 2021 wakati huo tulikuwa na Watanzania asilimia sita tu wanaotumia nishati safi ya kupikia. Leo tunazungumza hapa zaidi ya 28% ya Watanzania wameshaanza kutumia nishati safi ya kupikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi jitihada anazozifanya Mheshimiwa Rais, sisi Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, ni

jukumu letu kuhakikisha tunazisema kwa ujasiri na tunasema kifua mbele. Ni juhudi za dhati za kusogeza mbele hili gurudumu la kupunguza muda wa wanawake wanaotumia jikoni, kwa ajili ya kupika, kuokoa afya za Watanzania na kama haitoshi kulinda mazingira ya Tanzania yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais mpaka sasa hivi amesambaza mtandao wa zaidi ya kilomita 56.4 za mabomba ya gesi nchini, ili tuweze kutumia nishati safi ya kupikia. Mheshimiwa Rais ameweka *billions of moneys* kuhakikisha tumesambaza mitungi zaidi ya 300,000, majiko banifu zaidi ya 49,000 na majiko ya umeme zaidi ya 7,000 nchi nzima. Wanawake wanapika kwa tabasamu, wanapika wakifurahi na wanaume wetu pia, wanapika wakifurahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili siyo jambo la kubeza. Ninasema Waheshimiwa Wabunge wamemtendea haki Mheshimiwa Rais, waendelee kutembea kifua mbele. Sote hapa tumesoma, zamani katika shule zetu, wale tuliosoma shule za bweni, ukienda jikoni kumtazama mpishi, mazingira anayopikia, lile jiko lina masizi, lile jiko lina Moshi, yaani ni mazingira magumu ya kupika. Leo tunavyozungumza taasisi zaidi ya 53 zimepelekewa majiko ya nishati safi ya kupikia na wale watu wanatoa ushuhuda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wangu aliniagiza pale Kondoa kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mariam Ditopile. Nimekwenda kuzindua ule mradi wa majiko ya kisasa kwenye shule, nimepewa mbuzi, nimepewa mafuta ya kupikia, ilikuwa ni sherehe. Wale watu hawaamini ile shule imejengwa tangu uhuru, nimepewa zawadi kwa sababu, hawakutegemea kama ipo siku watatumia majiko safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaahidi Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, katika hii bajeti wanayotupitishia tumepanga kupeleka kwenye taasisi zaidi ya 400, ili tuwatoe watu katika majiko na upishi wa kizamani wa kutumia kuni na mkaa. Mwendo ni mdogo, lakini ushauri waliotupatia tuutumie, sekta binafsi, tushirikishe Waheshimiwa Wabunge na tushirikishe vyama vyetu. Tumeupokea, tutaufanyia

kazi tutakimbia kwa kasi na mpaka tukirudi hapa kuomba bajeti nyingine tutakuwa tumepiga hatua kubwa sana, hilo ninaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu watuamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi wameongelea hapa habari ya upatikanaji wa umeme, hasa katika maeneo ya visiwa na hili ninaomba niliongelee kipekee kabisa. Ukienda visiwani kupeleka umeme ni changamoto kubwa sana, bado watu wanaishi kwenye maisha ya kutumia vibatari. Tunavyokuwa tunajinadi kwamba, tumefikisha kwenye vijiji vyote ilikuwa ni changamoto kubwa sana kupeleka kwenye maeneo ya visiwa, lakini Mheshimiwa Rais baada ya kuona changamoto ni kubwa, angalau tuwatoe watu kwenye vibatari na mishumaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika visiwa 143 vinavyokaliwa na watu mpaka sasa hivi tunavyozungumza visiwa zaidi ya 120 vimepelekewa umeme wa *solar*. Hili ni jambo la kuzungumza sisi Wabunge kifua mbele, wanasema maneno mazuri yasiposemwa, maneno mabaya yatatawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni maneno lazima tuyazungumze. Tumewatoa watu kwenye kutumia kibatari, Waheshimiwa Wabunge tumeweka ruzuku kuanzia 45% mpaka 75% nyumba za visiwani. Nimekwenda Jimbo la Ilemela, Kisiwa cha Bezi, lile jimbo watu hawakulala usiku kucha wananisubiri tukazindue mradi wa umeme jua, umeme wa *solar,* tuwatoe wale watu kwenye vibatari na mshumaa. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua Mheshimiwa Waziri wangu ataeleza mengi. Ninataka nimalizie na hili moja la mwisho, kubwa sana, ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza; la matumizi ya gesi katika magari na vyombo vya moto, ili tuondokane na adha ya mafuta, ambayo wote hapa Waheshimiwa Wabunge tumeona ilivyotuathiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana kabisa. Sisi tumebarikiwa rasilimali ya gesi, kama nchi na ni lazima tutumie rasilimali hiyo ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia. Ninawaambia Waheshimiwa Wabunge, Mwaka wa Fedha

2024/2025 tulikuwa na vituo vinavyoweza kujaza gesi kwenye magari tisa tu. Baada ya mwaka mmoja wa fedha sasa hivi tuna vituo 18, tume-*double in one year*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tunavyozungumza mipango ya Wizara yetu ni tunataka tuhakikishe katika huu mwaka wa fedha, kwenye mikoa ambayo haijapitiwa na bomba la gesi, tunapeleka *mobiles mean (LNG)* ambazo zitasadia magari ambayo yatabeba gesi, ili unapoendesha gari kutoka Dar es Salaam uweze kufika Mwanza kwa gesi na kurudi. Wale wanaotoka Kaskazini waweze kufika Kusini na kurudi. Hizo ndizo jitihada za Mheshimiwa Rais, kupitia kaka yangu Deogratius Ndejembi na sisi wasaidizi wake kuhakikisha Watanzania hawapati adha ya mafuta inapotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TPDC* kwenye Wizara yetu ndiyo imepewa dhamana ya kusimamia sekta hii ya gesi. Hivi tunavyozungumza wameshaongea na kampuni zaidi ya tano, kwa ajili ya kubadilisha gesi kuwa kimiminika, ili tuweze kuisafirisha kwenda kule mikoani ambapo sisi kule Shinyanga hatujafikiwa. Tarime kule hawajafikiwa, watu wa Kagera hawajafikiwa; tunaleta hayo magari na tumeingia mikataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wenzangu kazi yao ni kuishauri na kuisimamia Serikali, sisi kazi yetu ni kutekeleza mipango mizuri wanayoipanga ndani ya Bunge hili. Sisi milango yetu iko wazi asubuhi na mchana, wanapotuletea maoni yao, wakituletea wadau, tuko tayari kuwa-*accommodate*, tuhakikishe tunawatumikia Watanzania. Hilo ndilo lengo kuu la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie Waheshimiwa Wabunge, wengi wenu hapa wamekuwa wakinipigia simu, wamepata changamoto ya hapa na pale, mimi niko tayari kwa sababu najua ushindi wa Chama Cha Mapinduzi umeshabishwa na kazi nzuri zilizofanyika na nitakuwa sehemu ya wale ambao tutaleta ushindi huo kwa kishindo 2030.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana na ninawashukuru Wabunge wote kwa hoja nzuri walizozileta, Mwenyezi Mungu awabariki. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nimwite mtoa hoja Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, Waziri wetu wa Nishati aje kuhitimisha hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia kuwepo kwa siku hizi mbili hapa katika ukumbi huu wa Bunge hili Tukufu, tukijadili masuala mbalimbali kuhusu uendelezaji wa Sekta ya Nishati ambayo sote hapa tunakubaliana kwamba nishati ni kichocheo kikubwa cha uendelezaji wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, nitumie fursa hii pia kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ikiongozwa na Mwenyekiti Subira Mgalu, kwa taarifa yake iliyosheheni uchambuzi wa kina, pamoja na maoni na ushauri uliotolewa na Kamati kwa ajili ya kuendeleza sekta yetu hii ya nishati, kwa maendeleo ya Taifa letu na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaahidi, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti wa Bunge na Mwenyekiti wa Kamati yetu na Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini wote kwamba, tunachukua ushauri uliotolewa na Kamati ya Nishati na Madini, tutakwenda kufanyia kazi ushauri huo na kuleta mrejesho wa yale ambayo wameyashauri mbele ya Bunge hili Tukufu kupitia Kamati ya Kudumu ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru vilevile Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hotuba yangu ya bajeti ya Wizara ya Nishati, waliochangia hapa ndani, lakini wapo ambao vilevile wamechangia kwa maandishi na ninaahidi kwamba tutafikisha majibu yote mbele ya Bunge hili Tukufu, wale waliochangia hapa ndani na wale walioleta michango yao kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba yangu imechangiwa jumla humu ndani na Wabunge 45, ninaomba sasa nitoe ufafanuzi wa baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge, nitoe ufafanuzi na majibu ya baadhi ya hoja hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Nishati tumejipanga kuhakikisha kwamba, maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, vilevile maelekezo yaliyotolewa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi na vilevile mwelekeo uliowekwa kwenye Dira ya 2050 yanatekelezwa kwa vitendo na kwa haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo tulilowekewa ni kwamba mpaka mwaka 2030, tuweze kuwa tunazalisha umeme wa megawati 8,000. Nirudi nyuma kidogo, wakati Dkt. Samia Suluhu Hassan anaingia madarakani mwaka 2021, Taifa letu lilikuwa linazalisha umeme wa megawati 1,540, leo tunavyozungumza hapa tunazalisha megawati 4,500.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaona hatua iliyopigwa ndani ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan na kwa nini nimerudi nyuma kidogo, ni ili kutoa mwelekeo wa kwamba linawezekana kufika megawati 8,000 mpaka 2030 chini ya uongozi wake Dkt. Samia Suluhu Hassan. Wizara ya Nishati tumejipanga kuhakikisha tunapata megawati hizo, tutatumia vyanzo vyote ambavyo vinapatikana katika Taifa letu. Tukianza na vyanzo vya maji tuna umeme, Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Malagarasi, ambao mkandarasi yuko *site*, megawati 49. Kuna Mradi wa Kakono wa megawati 87, tuna Miradi ya Ruhuji megawati 358, tuna Mradi wa Rumakali megawati 222. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo malengo alizungumza Mheshimiwa mmoja hapa kwamba, tutumie *geothermal* kuzalisha umeme. Tumejiwekea malengo kwamba mpaka ifikapo mwaka 2030, Taifa letu liwe linazalisha umeme megawati 130 kutokana na *geothermal*. Vilevile, Taifa letu limebarikiwa kuwa na *deposit* kubwa ya makaa ya mawe. Tunashirikiana na sekta Binafsi kuhakikisha kwamba, tunaanza uzalishaji wa umeme wa zaidi ya megawati 2,000 kwa kutumia makaa ya mawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, imezungumzwa hapa kwamba kwa mara ya kwanza kwenye Taifa letu, tumekuwa tuna mradi mkubwa wa uzalishaji umeme kwa kutumia jua wa Kishapu Shinyanga. Hivi tunavyozungumza megawati 50 zipo kwenye gridi ya Taifa, lakini gridi hiyo itaongezwa megawati 100 kutoka hapo

hapo Kishapu. Tunachukua pia maoni yaliyotolewa na Mheshimiwa Pondeza ya kwamba, sasa twende tukawe na betri za kuhifadhi umeme mwingi zaidi. Pale jua linapokuwa kali, basi tunazalisha umeme mwingi tuna uhifadhi ili tuje kuutumia baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo Kishapu peke yake tunayo miradi ambavyo itakuja kwa ajili ya jua, Manyoni, tuna Zuzu hapa Dodoma, lakini vilevile tuna miradi ya upepo ya kuzalisha umeme ambayo itaenda kuwekwa Same, tunayo Makambako. Kwa hiyo, tunajipanga kuwa na *energy mix* kubwa zaidi katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuna Urani mwingi tunajipanga pia kuwa tunazalisha umeme kutumia urani ili kuweza kufikia malengo ya kuzalisha megawati 8,000 mpaka 2030, lakini siyo tu megawati hizo 8,000, tunalo lengo kufikisha megawati 70,000 mpaka ifikapo 2050, tunafahamu umeme ndiyo kichocheo kikubwa cha maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuzalisha umeme ni jambo moja, tunaufikishaje kwa wananchi ili waweze kuuona ukiwaka katika maeneo yao. Serikali hii ya Awamu ya Sita imejipanga kuhakikisha kwamba, tunatoa umeme katika maeneo ya uzalishaji, leo hii Bwawa la Mwalimu Nyerere linazalisha megawati 2,115, lakini tunajenga *lane* sasa ya kutoa umeme ule uweze kufika Dodoma, *lane* ya Chalinze Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme ule ukifika Dodoma, utaweza kuingia kwenye *lane* uweze kwenda mpaka hadi Ibadakuli kwa watani zangu Wasukuma kule na wao wataweza kupata umeme huu, watu wa Tabora, watu wa Singida, watu wa Kahama wote watapata umeme huu ambao unatoka Bwawa la Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo *lane* hii tu ya Chalinze – Dodoma, umeme huu ili uweze kufika katika kongani ya viwanda, lakini pia uende katika Jiji la Dar es Salaam, ambao ndiyo wanatumia umeme mwingi katika Taifa letu, tunajenga *lane* ya kutoka Chalinze – Kinyerezi – Mkuranga kuhakikisha kwamba

umeme mwingi zaidi unakwenda kule katika maeneo ya uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo *lane* hiyo tu ambayo inajengwa, hapa tumesikia Wabunge wa Kusini, ninamwona na rafiki yangu Ado yuko hapa, wana *lane* yao ya Songea, Tunduru, Masasi na Maumbika. *Lane* hii ilisimama kwa muda mrefu, lakini hata Mheshimiwa Ado Shaibu hapa ni shahidi ya kazi inayofanywa na Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nilitembelea Jimboni kwake, nilikuta mkandarasi anasuasua, hafanyi kazi, tulibanana na mkandarasi yule, alileta sababu za kwamba hajalipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliomba fedha katika Serikali hii sikivu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mkandarasi yule kwa hivi tunapozungumza amekwishalipwa bilioni 33 na amerejea *site* na anaendelea kusimika nguzo zile ili *lane* hiyo ya kilovoti 220 iweze kutoka Songea ifike Tunduru, ambayo ni kilometa kama 214 na itatoka Tunduru itakwenda Masasi kule kwa akina Mheshimiwa Akwilapo. Ikitoka Masasi pale hata rafiki yangu Mheshimiwa Nawanda jana alitishia kushika shilingi yangu, maana *lane* inatoka pale inakwenda Newala ya *KV* 33, ambayo mpaka sasa iko 81% inajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *lane* ambayo itendelea *KV* 220 ambayo itatoka Masasi mpaka jimboni kwa Mheshimiwa Nape Nnauye, Maumbika ambapo kuna kituo kikubwa pale. Umeme ule utapoozwa pale Maumbika na utaingia kwenda Mtwara, watu wa Dinyecha huko watapata umeme. Watu wa Lindi Kwautali watapata umeme na kilio cha katika katika umeme utakuwa sasa kimekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan iko kazini na sisi Wizara ya Nishati tutaishi maono yale aliyonayo Rais wetu Jemedari kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa amezungumza Mbunge wa Mbozi ya kwamba, kuna kukatika katika umeme kule. Nikiri hilo, watu wa Mbozi wanatumia *lane* inayotoka Mwakibete, ambao uwezo wake ni megawati 25. *Lane* ile inatembea karibu *kilometre*

83, ambapo njiani humo imeunganisha wateja wengi zaidi, lane ile imeshazidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa inatumia megawati 23, ni ziada ya megawati mbili tu, ndiyo maana umeme unakatika katika, lakini nimuahidi Mheshimiwa Mbunge wa Mbozi na Wabunge wote wa Mkoa wa Songwe kwamba, kuna *lane* ambayo inajengwa kutoka Tagamenda Iringa, itapita Kisada, itakwenda Iganjo Mbeya na itashuka itakwenda mpaka Nkangamo Mkoa wa Songwe.

Alizungumza kwamba, Nkangamo ni mbali umeme kurudi nyuma, lakini ile lane ni ya *kilovolt* 400, inapitisha umeme mwingi zaidi na ikifika Nkangamo kuna *lane* ambazo zitajengwa za *KV* 33 kurudisha umeme kwenda mpaka Mbozi, ambapo mahitaji ya Mbozi ni *megawatt* nne, watapata *lane* ambayo inafikisha karibu megawati 25 Mbozi peke yake, unaona namna gani ambavyo wataweza sasa kuweka viwanda na vikasukuma mashine bila ya changamoto yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mkoa mwingine ambao bado haujaingia kwenye gridi ya Taifa ni Mkoa wa Rukwa, lakini *lane* hii niliyoitaja, ikitoka Nkangamo inakwenda mpaka Malangali kwenye Kituo cha Kupooza Umeme Mkoa wa Rukwa, ambapo itakuwa ndiyo mkoa wetu wa mwisho kuingia katika gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka hivi tunavyozungumza 78% ya kazi zile zimeshafanyika, kwa hiyo, Mkoa wa Rukwa muda siyo mrefu wataingia katika gridi ile ya Taifa. Ukishausambaza umeme huu ni lazima sasa limfikie mlaji wa mwisho ambaye ni mwananchi wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania. Kwa sasa tunaunganisha wateja kama 500,000 kwa mwaka, lengo tulilonalo ni kufikia wateja 1,700,000 kwa mwaka, lakini tunafikiaje lengo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Wabunge wametoka kusema na kuchangia kwamba kuna maeneo ambayo ni manispaa, leo hii kwa Chinyele kule ukienda Chizomoche ni kijiji lakini wanasema wako Jiji la Dodoma. Leo hii watu wa Chahwa kwa Mavunde, utasema ni manispaa lakini ni kijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vivyo hivyo, ukienda kwa *Engineer* Maganga kule kuna kijiji ambacho ndani ya Kata moja vijiji viko vitatu. Vijiji viwili vinahesabika viko mjini, kijiji kimoja kinaonekana kiko kijijini. Serikali hii ni Sikivu, baada ya kusikia kilio cha Wabunge, nimewataka watalaam wa *REA* na *TANESCO* kuwasiliana na Wabunge wote wanaotoka katika maeneo ya namna hii na kuhakikisha tunapata vijiji vyote ambavyo vipo ndani ya manispaa, vipo ndani ya majiji, vipo ndani ya halmashauri za miji ili tuweze kutambua na kuja na mradi maalum wa kuhakikisha mpaka tunaposimama hapa mwakani kwa uwezo wake Mungu, vijiji hivi viwe vimeunganishwa na umeme kwa shilingi 27,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni sikivu na haiwezi kuweka matabaka ya wananchi, mtu amekaa ng'ambo moja analipa 27,000, ng'ambo ya pili ambayo bado ni kijijini analipa 320,000. Serikali imesikia na inaenda kulifanyia kazi na tutatenga fedha katika hizi mtakazotupitishia tutajibanabana, tutajikata kuhakikisha umeme unawaka katika vijiji ambavyo vipo katika miji. Katika hili hata kama Mbunge na lenyewe linanigusa, kwa hiyo, ninawaahidi tutalisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia siyo tu kusambaza kwa wananchi wa vijijini, tunaweka mikakati mahsusi ya kuhakikisha kwamba maeneo ya uzalishaji, alisema Mbunge wa Kigoma, kuna Kiwanda kule cha Maziwa hakipati umeme wa uhakika, anashindwa kuzalisha maziwa kwa kadri vile ambavyo kiwanda kina uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo kama Chunya ambayo tumeshafanya kazi kwa karibu na Waziri wa Madini, kuna wachimbaji wadogo wadogo wengi wanashindwa kufikia *potential* ya migodi yao kwa sababu hawana umeme wa uhakika. Kule kwa watani zangu Wasukuma kuna wachimbaji wadogo wadogo wanatamani kupata huduma ya umeme. Mkoa wa Mara, Tarime wanatamani kupata huduma ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweka mkakati maalum, sisi Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini, kuhakikisha katika

kusambaza umeme, umeme unafika kwa wachimbaji wadogo wadogo kwenye viwanda vidogo vidogo ili viweze kuzalisha, tuweze kukusanya mapato mengi zaidi kama Taifa ili tuweze kupiga hatua na kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo moja pia limesemwa sana hapa suala la taasisi. Serikali hii ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imejenga shule nyingi, imejenga vituo vya afya vingi, imejenga zahanati nyingi. Kuna taasisi za kidini zipo kwenye vijiji vyetu, ninawataka *REA* hapa kufanya tathmini ya kupeleka umeme kwenye taasisi zote zilizo za umma katika vijiji vyote tulivyofikisha umeme ili tuweze kuunganisha taasisi hizi, kwenye shule watoto wetu waweze kusoma muda wote, ndiyo faida ya umeme kwenye vijiji, wenye hospitali waweze kuwa na majokofu, mafriji na vitendea kazi kama *x-ray* na kadhalika vifanye kazi vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji imefanya kazi kubwa kufikisha maji, lakini saa nyingine kusukuma pampu za maji zinakuwa hazisukumi. Tuweze kufanya kwa tathmini tujue tunahitaji gesi gani ili kupelekea huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mafuta, Waheshimiwa Wabunge wamelichangia hili, changamoto ya mafuta tuliyonayo, ambayo imepelekea kupanda kwa bei ya mafuta ni janga la kidunia. Tarehe 28 Februari, vita ilianza kati ya Iran, Israel na Marekani, vita ile ilifanya mwezi Machi mafuta kupanda bei katika soko la dunia, lakini suala sasa si bei tu, suala ni upatikanaji wa bidhaa yenyewe ya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tunavyozungumza, Wabunge wakiwa wanafuatilia vyombo vya Habari, wataona *Strait of Hormuz* imefungwa, ambapo zaidi ya 20% ya nishati ya mafuta inatoka pale, lakini siyo tu nishati ya mafuta, hata *crude oil* - mafuta ghafi, ambapo tunachukua mengine India 40%. India wenyewe wanachukua *crude* kutoka *Strait of Hormuz*, ambapo ili waweze kupata *crude* hiyo lazima ipite pale kutoka zile Nchi za Falme za Kiarabu, Saudi Arabia, Kuwait, Bahrain iweze kupita pale kwenda India. Kwa hiyo, kufungwa kwa ile *Strait of Hormuz*,

kunaleta changamoto katika mnyororo mzima wa upatikanaji wa mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hii ni sikivu, Serikali hii inajali wananchi wake na ndiyo maana leo hii mnaona kwa jitiada kubwa za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hakuna kituo cha mafuta kina foleni. Tumeona maeneo mbalimbali ya ulimwengu, kukiwa kuna changamoto ya upatikanaji wa mafuta, kukiwa kuna foleni na kadhalika na kadhalika, lakini Tanzania shughuli zimeendelea kama kawaida, ni kwa sababu ya kazi kubwa iliyofanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili nichukue muda huu kuwashukuru *TAOMAC* wamefanya kazi kubwa, hawa ni chama cha waagizaji wa mafuta. Siyo *TAOMAC* pekee yao alikuwepo Katibu Mkuu wao Mgaya hapo, hata *TAPSOA* - Chama cha Wamiliki wa *Petrol Station* hizi, ninaamini Tino Mmasi yupo hapa. Chama hiki tumefanya kazi nao kwa karibu, kuhakikisha muda wote mafuta yanapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaahidi Waheshimiwa Wabunge; tunafahamu kuwa changamoto ni bei imepanda na hii inatokana na soko la kidunia; bado ndani ya Serikali tunaendelea kuangalia namna bora ya kufanya ili bei ziwe himilivu; na tunaendelea kulifanyia kazi. Kwa sasa tutahakikisha kwamba mafuta yanapatikana wakati wote ili shughuli za kiuchumi zisiweze kusimama.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ili kujipanga yasije yakatukuta tena baadaye Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, Mheshimiwa Rais alifanya uzinduzi wa ujenzi wa matenki ya kuhifadhi mafuta ambayo yatahifadhi zaidi ya lita milioni laki tatu sitini na tisa, ambayo yanajengwa Kigamboni Dar es Salaam. Hii itatusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, alizungumza Mheshimiwa Chiwelesa kuhusu suala la kuwa na mabomba ya kupitisha mafuta. Tuna mkakati wa kuhakikisha ya kwamba tuna bomba la mafuta linalotoka Dar es Salaam mpaka Tunduma. Bomba hili litakuwa lina matoleo Morogoro ili watu wa Dodoma, Tabora,

Singida, Shinyanga na nchi jirani za Burundi, Rwanda na Congo ubavu huu, wao wanachukulia mafuta Morogoro ama Dodoma. Vile vile kutakuwa kuna matoleo Makambako ambapo watu wa Njombe na Ruvuma watachukulia pale. Kutakuwa na matoleo Mbeya ambapo watu wa Malawi na Mbeya watachukulia mafuta pale na Tunduma kwa ajili ya wenzetu wa Zambia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii kwanza, itatupa faida kubwa moja, itafanya msongamano katika Jiji la Dar es Salaam kupungua; pili, tutaondoa mzigo mzito kwenye barabara zetu; tatu, tutakuwa tuna matenki ya kuhifadhia Morogoro, Makambako na Mbeya; tutakuwa tuna mafuta mengi zaidi ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na gesi; katika gesi asilia *TPDC* imefanya kazi kubwa sana. Wakati mwingine ni kwamba kwa sababu tuna mradi mkubwa wa kielelezo na kimkakati kama Taifa wa *LNG*, watu tumeweka macho yetu yote kwenye *LNG,* tunasahau kwamba kuna Visima vya Mnazi Bay, vya Songosongo; na hivi sasa kuna bomba kubwa ambalo linajengwa la kilomita 34 kutoka Ntoria kuelekea Madimba, ambapo Kisima cha Ntoria kitaenda kuunganishwa kwenye Kiwanda cha Kuchakata Gesi Madimba na kuweza kusafirishwa vile vile kazi kubwa inafanyika. Hivi sasa Mnazi Bay wamechimba kisima kingine ambacho kimekutwa na *deposit* kubwa ya gesi mara mbili ya ile ambayo ilidhaniwa mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kuna kazi kubwa ambayo inaendelea na *TPDC* kuna utafutaji wa mafuta Eyasi Wembere na maeneo mengine ambayo *TPDC* inayafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye mradi huu mkubwa wa kielelezo wa *LNG,* kwa sasa Serikali tumefikia hatua za mwisho kabisa za kwenda kuanza mradi huu. Sisi ndani ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumekwishamaliza kila lile linalowezekana na sasa ni jukumu la kampuni zile za Kimataifa kuja mezani na kusaini mkataba ili kazi ya kutoa ile gesi ianze.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makubaliano ya kibiashara yamefikiwa, makubaliano ya kikodi yamefikiwa; sasa tupo kwenye

makubaliano ya kisheria; ambapo ninaipongeza Ofisi ya *Attorney General* chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Hamza Johari ambayo imeshafikisha mkataba ule mbele ya wenzetu wale ili waweze kuupitia na waweze kuusaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina habari njema, ni Jumatatu au Jumanne viongozi wakuu wa taasisi zile *Equinor, Exon* na *Shell* watakuwa wamewasili hapa nchini kwa ajili ya hatua za mwisho za Mradi huu wa *LNG*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunasubiri wenzetu waje ili kukamilisha mazungumzo na Serikali yetu tayari tumeanza kazi zingine; kama ulipaji wa fidia ulishafanyika katika eneo la Likongo, kuna shule iliyojengwa. Hii ni kwa kushirikiana na hawa wenzetu wa *Exon, Equinor na Shell* wote tayari kuna kazi ambazo zimeanza. Hivi sasa tumewataka *TPDC* kwenda Mkoani Lindi ili kutoa elimu juu ya fursa ambazo zitapatikana kutokana na kuwepo kwa Mradi huu wa *LNG*. Siyo kwa Lindi tu, pia tumewataka *PURA* kuzijengea uwezo taasisi za Kitanzania za wazawa ili mradi huu utakapoanza waweze kushiriki katika *local content* katika ku-*supply* vitu mbalimbali katika mradi ule. Tayari kazi hiyo *PURA* wamekwishaianza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mengi ambayo tunaenda kuyafanya na kuyatekeleza kama Wizara ya Nishati chini ya maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Spika Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala, wewe Mheshimiwa Naibu Spika Mbunge wa Babati Vijijini. Ninafahamu kuwa una vitongoji vyako kama saba hivi ambavyo navyo vinaonekana kama viko mjini lakini viko kijijini navyo ni kati ya yale maelekezo ambayo tunaenda kuyafanyia kazi. Nikushukuru sana wewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana Wenyeviti wa Bunge; Mheshimiwa Najma Giga, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso na Mheshimiwa Deodatus Mwanyika ambaye na yeye ana *mini-hydro* kule Jimboni kwake Njombe ambayo na yenyewe tunaifanyia kazi. Niwashukuru sana Wenyeviti hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru vilevile Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Subira Mgalu na Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti Simon Songe, Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati wote ninawashukuru sana. Vile vile ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu. Imetujenga, imetupa njia na miongozo ya namna ambavyo tunakwenda kutekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi zilizokuwa zinatoka hapa kwa Wizara ya Nishati ninamwambia Mheshimiwa Naibu Waziri wangu, kwamba pongezi hizi ni deni. Kwamba, leo tumepongezwa, tusipotekeleza wajibu wetu yale matarajio ya Waheshimiwa Wabunge hawa yasipofikiwa mwakani hatutokuja hapa kupongezwa. Kwa hiyo niwaahidi, kwamba pongezi walizokuwa wanazitoa tunachukulia kama mzigo ambao tunaenda kufanya kazi ili mwakani tukirudi hapa, basi pongezi hizi ziweze kuzidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Salome yeye anasema Wiklif mimi ninawaambia hiyo ni Wycliffe; Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, Naibu Waziri na Mbunge wa Viti Maalum kwa sababu amekuwa ni Naibu msikivu, mchapakazi na ambaye ukimtuma hata usiku wa manane atakimbizana na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwa ninamwambia Mheshimiwa Naibu Waziri, kwamba Tanzania ni kubwa, hatutakiwi kukaa ofisini. Mimi kama Waziri peke yangu siwezi kuwa kila sehemu wakati mmoja; tuchape kazi tuzunguke watu waone kazi inayofanyika. Kwa hiyo nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri na nimshukuru kwa ushirikiano ambao ananipatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mtovu wa nidhamu na sitokuwa ninatenda haki nisipowashukuru wazee wangu Makatibu Wakuu wawili nilionao. Ninaye Injinia mbobezi kwenye masuala ya umeme na amekuwa mwalimu wangu sana kwenye masuala haya ya umeme; Injinia Mramba nimshukuru sana sana. Vile vile nimshukuru Katibu Mkuu wa Nishati anayesimamia masuala ya gesi na mafuta; naye ni mbobezi sana kwenye masuala haya,

Dkt. James Mataragio; naye amekuwa mwalimu wangu mkubwa katika masuala ya gesi na mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makamishna tuliona nao, Ndugu Luoga na Ndugu Shirima, niwashukuru sana na *management* nzima ya Wizara na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara. Nimezisikia pongezi hapa za taasisi. Pongezi hizi nazo ni deni kubwa kwa Wakurugenzi wa Taasisi zetu kuweza kwenda kufanya kazi usiku na mchana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo na kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge mbele ya Bunge lako Tukufu, ninaomba sasa kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana. Mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri tunashukuru, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Waheshimiwa Wabunge, tunawashukuru sana sana.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

*Hapa Spika (Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae. Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 58 – Wizara ya Nishati**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…………………………*Sh.* 7,431,789,000

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hiki ni kifungu cha mshahara Waziri na mpaka sasa hivi Kiti hakijapokea jina lolote kutoka chama chochote ndani ya Bunge. Hii inatokana na kazi kubwa iliyofanywa na Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri. Kwa kiasi, Wizara hii kila mwaka ina mshahara sio chini ya sita, saba. Hongereni sana. Kifungu hicho kinaafikiwa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.............*Sh.* 1,707,835,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*…………......*Sh.* 2,400,896,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*…………..................…*Sh.* 982,003,000
Kifungu 1005 – *Legal Services Unit*..…………….....…....*Sh.* 887,153,000
Kifungu 1006 – *Government Comm Unit*…....…….......*Sh.* 968,651,000
Kifungu 1007 – Procurement *Management Unit*..…*Sh.* 1,156,985,000
Kifungu 1008 – *Environment Management Unit*……...*Sh.* 757,657,000
Kifungu 1009 – *Management Info System Unit*……….*Sh.* 962,013,000
Kifungu 1010 – *Monitoring and Evaluation Unit*….....*Sh.* 1,193,371,000
Kifungu 3001 – *Electricity and Renewable Energy*..………………...*Sh.* 32,910,528,100
Kifungu 3002 – *Petroleum and Gas*………………..…*Sh.* 10,659,763,900
Kifungu 3003 – *Cleaning and Cooking Unit*.............*Sh.* 1,017,648,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Kamati yako ijielekeze kwenye Kitabu cha Nne, Miradi ya Maendeleo, ukurasa wa 245, Fungu 58.

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 58 – Wizara ya Nishati**

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*...................*Sh.* 3,000,000,000
Kifungu 3001 – *Electricity and Renewable Energy*.........................................*Sh.* 2,284,364,836,000
Kifungu 3002 – *Petroleum and Gas*.....................*Sh.* 175,000,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yako imekamilisha kazi.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 126(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025, ninaomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi yake. Ninaomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji kuhusu Hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Walioafiki wameshinda kwa sasa Bajeti ya Wizara ya Nishati imepita kwa kishindo. Nichukue nafasi hii kukushukuru sana Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu na watendaji wenu; lakini bado kuna changamoto ya nishati safi vijijini na kutokana na changamoto hii kuna baadhi ya vitu vinajitokeza. Kwanza wanaona ni gharama, lakini pili ku-*refill* mitungi ile ni shida sana kwao; lakini gharama kubwa tunaipata kwenye mazingira.

Jana nilikutana na Mkurugenzi Mkuu wa *ORYX* alikuja Ofisini kwangu tukajenga sana hii hoja na akataka kuunganishwa na Mkurugenzi Mkuu wa *National Housing*, kazi ambayo ambayo nimefanya leo. Tumewaunganisha na sasa wana mkakati wa kuweka *piping* za *gas* kwenye kila nyumba ya *National Housing* kwenye miji yote mikubwa Tanzania. Faida itakayopatikana hapo wata-*cross subsidy* kupeleka vijijini na kupunguza zaidi gesi na kuunga mkono jitihada za nishati salama na safi ya Mheshimiwa Rais Samia.

Kwa hiyo, huo ndiyo mkakati ambao wanakwenda nao sasa. Tunaomba Wizara mshirikiane vizuri pamoja na wahusika. Hii inafanywa na *private sector,* wala Serikali hamna haja ya ku-*involve* jambo lolote kwenye fedha zenu; ni kuunga mkono jitihada za *2050,* kwamba *private sector* waweze kuchangia 70% ya *vision* ya *2050.* Wanaanza *ORYX* na kampuni nyingine za gesi ambazo ziko nchini.

Tushirikiane nao ili kuhakikisha kwamba miji yote mikubwa kama Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza, Arusha na Kilimanjaro ipumue, iepukane na matumizi ya mkaa ambao unaharibu mazingira ya Taifa letu. Ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa michango mizuri sana. Mmeonyesha uwezo wenu weledi na kuelewa vizuri mahitaji na mpango kabambe wa Serikali katika kuhakikisha Taifa letu bila umeme hatuwezi kuvuka 2050.

Baada ya maneno hayo, niwashukuru tena wote; watendaji, Katibu Mkuu na wataalam wako, watu wa *TPDC,* kwa kweli mmetufurahisha kwa namna mnavyofanya kazi kwa pamoja na kwa utiifu na uzalendo. Baada ya maneno haya ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.18 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 24 Aprili, 2026, Saa Tatu Asubuhi)*

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA